

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Kwanza - Tarehe 2 Novemba, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwafahamisha kwamba katika Mkutano uliopita, Bunge hili lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ambao ni Muswada wa Sheria ya Fedha, unaitwa *The Finance Bill* na Muswada wa Sheria wa kuidhinisha matumizi ya fedha katika Bajeti ya mwaka huu, unaitwa *Appropriation Bill*. Taarifa ni kwamba Mheshimiwa Rais ameshatoa kibali chake kwa Miswada yote miwili na sasa ni Sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Kabla hatujaendelea napenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunao wageni wa Kimataifa, Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Burundi wako Wabunge tisa pamoja na Balozi wa nchi hiyo hapa Tanzania, wamekuja kusalimia hapa Bunge. *(Makofi)*

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatazo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

Upimaji wa Viwanja Dodoma

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Dodoma unakua kwa kasi kubwa na kwa kuwa ili kukidhi haja ya uhamiaji wa Makao Makuu hakuna budi kuwaondolea wananchi usumbufu wa maeneo hayo na kuwawezesha kujenga nyumba bora na za kisasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupima viwanja vya makazi katika vijiji vya Manispaa ya Dodoma ambavyo viro karibu na Mji, kama vile Nala, Ihumwa, Mkonze, Zuzu, Makutopora, Msalato, Nzuguni, Iyumbu, Mtumba na Ntyuka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo:-

Upangaji wa viwanja kwa ajili ya maendeleo ya mji unazingatia mpango kabambe wa uendelezaji unaoelekeza pia upangaji na upimaji wa maeneo ya matumizi mengine yasiyo ya kimji kama maeneo ya mashamba, ufugaji, misitu pamoja na maeneo ya vijiji vilivymo katika eneo la uendelezaji wa Makao Makuu, Dodoma.

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu imejielekeza katika upangaji na upimaji wa maeneo yanayohusika moja kwa moja na mahitaji ya mji unaopanuka haraka. Katika kipindi cha miaka ya 2002/2003 na 2003/2004, viwanja zaidi ya 9,000 vimepangwa na zaidi ya viwanja 6,000 vimepimwa.

Maeneo ya vijiji yanayofikiriwa na upanukaji wa mji yanaingizwa katika mfumo wa mpango wa mji. Vijiji ambavyo kwa sasa vimefikiwa na upanukaji wa mji na kuingizwa katika mfumo wa mipango ya mji ni Nzuguni, Mkonze na Ntyuka.

Maeneo ya vijiji ambavyo upanukaji wa mji utachukuwa muda mrefu kufikiwa, madaraka ya kupanga, kupima na kusimamia uendelezaji yamekasimiwa kwa Halmashauri ya Manispaa na vijiji vyenyewe. Kunapotokea suala lenye mahitaji maalum kama vile asasi za Kiserikali, ulinzi na usalama au miradi mikubwa inayolenga kuboresha uzalishaji kama vile miradi ya uboreshaji masoko ya mifugo (*TLMP*), waliojenga machinjio ya kisasa, mnada wa upili wa Kizota, Mamlaka husaidia ili kuiwezesha huduma kutekelezwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo Serikali inachukua ili kuendeleza maeneo ya vijiji vilivyo pembezoni mwa mji na vilivyo kandokando ya barabara zinazoingia Dodoma ni ushirikishwaji wa wanakijiji wenyewe kwa kuchangia fedha za upimaji na kutoa wataalam. Kwa mfano kama ilivyofanyika kwa maeneo ya Oyesterbay, Chang'ombe na Mailimbili.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Bunge hili lilipitisha Sheria ya kutoa unafuu wa vifaa vyta ujenzi ili kuharakisha ujenzi wa Makao Makuu, Dodoma. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Sheria hii ikitekelezwa wananchi wa Dodoma watanunua vifaa kwa bei nafuu ili kuharakisha ujenzi wa Makao Makuu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, ni kweli ulikuwepo utaratibu amba Serikali ilitoa upendeleo na unafuu wa vifaa vyta ujenzi katika Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lakini utaratibu huo umefutwa kwa sababu baadaye ilijulikana kwamba ultumika vibaya. Vifaa vile vilinunuliwa na hatimaye vilikwenda kujenga nje ya Dodoma. Kwa hiyo, Serikali ilifuta utaratibu huo na hivi sasa Serikali inaangalia upya Sheria na utaratibu na sera nzima ya kuhamia Dodoma na Sheria iliyounda *CDA* ili kuangalia majukumu ya msingi na muhimu ambayo *CDA* inaweza kufanya kwa sasa.

Na. 2

Televisheni ya Taifa - Singida

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari na Siasa) Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri alipotembelea Singida mwaka 2002 aliahidi kuwa *TVT* itafikishwa Singida mwaka 2004.

(a) Je, Serikali husika inalifahamu jambo hilo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba ahadi hiyo inatekelezwa kama ilivyopangwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia thabiti ya kuhakikisha kwamba ahadi ya *TVT* kufikishwa na kuonekana Singida inatekelezwa. Jitihada kubwa ya Serikali kujenga vituo vya Televisheni ya Taifa nchini kote inakwazwa na uwezo mdogo wa kifedha na ndio maana Serikali kwa makusudi iliamua kwanza kutumia mtandao wa *Satellite* kurusha matangazo nchi nzima.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Serikali imeazimia kujenga mtambo mmoja kwa kila Makao Makuu ya Mkoa ambako matangazo ya *TVT* hayaonekani kwa hivi sasa. Mikoa hiyo ni pamoja na Singida ambako mtambo unatarajiwa kujengwa katika Kilima cha Nyamikumbi. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambako Televisheni ya Taifa haionekani hivi sasa, wawe na subira wakati Serikali inafanya mikakati ya kutekeleza mpango huo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubaliana na mimi na kwa kuwa aliyekuwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii aliahidi mbele ya wananchi kwamba mwaka 2004 Televisheni ya Taifa ingepatikana Mkoa wa Singida na sasa hivi tuko mwezi wa kumi na moja maana yake mwana 2004 unaisha. Je, atawaambia nini wananchi ahadi yenye muda maalum ili wananchi wajenge imani na ahadi za Serikali? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli nilipokuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu nikishughulikia Siasa na Habari niliahidi kule Singida kwamba matangazo ya Televisheni yangefika. Lakini nadhani akumbuke vizuri Mheshimiwa Diana Chilolo nilisema ama, tutakuwa tumeshaweka *transmeter* ya *TVT* kuhakikisha yanafika, kama tutakuwa hatujaweza hilo basi angalau kuhakikisha *satellite* itakuwa imeshapatikana. Wale wenye *dish* zao wataweza kuipata Televisheni ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nina hakika wenye *dish* hizo wanaweza kuipata Televisheni ya Taifa. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Na. 3

Kupanda kwa Gharama za Umeme

MHE. PETER KABISA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inawahamasisha wananchi kutumia nishati ya umeme na kuachana na matumizi ya mkaa ambao hatma yake ni ukataji wa miti hovyo/kiholela na kusababisha jangwa na uharibifu wa mazingira, vyanzo vya maji vya ardhini na mvua na kwa kuwa Serikali inakwenda kinyume na hamasa hiyo pale inapoongeza gharama za

umeme kwenye uunganishaji kufikia shilingi 200,000/= na kuongeza gharama za umeme unaotumika majumbani maradufu na kwa wasomaji wa *meters reading* hizo wakati wa *billing* maradufu na kwa wasomaji wa *meters* kutokufuata *meter reading* hizo wakati wa *billing* kwa mfano, katika mji wa Dodoma *meter reading* na bili havioani hata kidogo na matokeo yake *TANESCO* inakimbilia kukata umeme ili faini ilipwe kama mapato ya ziada kwa Shirika hali inayoweza kuwafanya watumiaji wa nishati hiyo waache kuitumia na kurudi kwenye matumizi ya mkaa, kuathiri misitu na mazingira na hatimaye kurudi nyuma kimaendeleo:-

(a) Je, Serikali imeshindwaje kusimamia sera yake ili kuwaondolea wananchi kero na maudhi yasiyo ya lazima kwa kuwaelekeza wahusika gharama ya kuunganishiwa umeme au kuwaelekeza *TANESCO* wasambaze gharama hiyo ya kuunganishiwa umeme kwa zaidi ya miaka mitano ikijua kuwa mteja husika ni wao kama kampuni inayomiliki?

(b) Je, Serikali imeshindwa kuagiza *LUKU* kwa kila mteja ambayo itamsaidia kuwa na uhakika wa deni lake kuliko iliovyo sasa, ambapo mita zinasomwa lakini kwenye bili ni makisio tu yanatumika?

(c) Je, Serikali haitambui kuwa ikipunguza gharama za umeme itapata wateja wengi zaidi ambao watafidia hasara yoyote ile ambayo itajitokeza na hapo hapo kuhifadhi misitu na mazingira?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijashindwa kutekeleza sera yake ya nishati ambayo inaweka umuhimu katika:

- (a) Kufikisha umeme kwenye makao makuu ya Wilaya na sehemu zingine vijijini;
- (b) Kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya umeme;
- (c) Kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta ya nishati;
- (d) Kuongeza ubora na ufanisi wa nishati ya umeme;
- (e) Kufanya utafiti wa kusambaza umeme vijijini; na
- (f) Kuunda taasisi maalum kwa ajili ya kushughulikia umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kutokana na usimamizi mzuri wa Sekta ya Nishati:-

(a) Upelekaji umeme kwenye makao makuu ya Wilaya ulioahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, unatarajiwa kufikia asilimia 78 ifikapo mwishoni mwa mwaka ujao.

(b) Mheshimiwa Spika, aidha, ifikapo mwaka 2006, karibu asilimia 54 ya umeme hautatokana na vyanzo visivyokuwa vya maji.

(c) Mheshimiwa Spika, mojawapo ya malengo ya Sera ya Nishati ni kuwawezesha wananchi kupata huduma ya umeme kwa bei nafuu na kuwaondolea wateja kero mbalimbali zikiwemo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

(d) Kuhusu bei ya umeme, kwanza ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tangu Mei, 2004, bei za umeme zilirekebishwa kwa kuzingatia gharama halisi za uzalishaji umeme na za kumfikishia mteja huduma hiyo. Ongezeko hili la bei ya umeme lilikuwa la lazima ili kukabiliana na ongezeko la gharama za uzalishaji umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa lengo la kuwapatia wananchi umeme wenye bei nafuu utafikiwa baada ya mipango kadhaa ya kubadilisha sura ya vyanzo ya uzalishaji umeme, kutekeleza kikamilifu mpango kabambe wa uzalishaji umeme na kuongeza ushindani katika sekta ya umeme kukamilika

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili 2003 hadi 2004, uzalishaji umeme umekumbwa na tatizo kubwa la ukame. Katika kukabiliana na tatizo hili na kuhakikisha kuwa panakuwepo na umeme wa kutosha nchini, Serikali iliandaa mpango wa dharura wa kuepukana na mgao wa umeme na ambao umegharimu karibu shilingi bilioni 146. Fedha hizi zimetokana na Msaada wa Benki ya Dunia, mchango wa Serikali na uwekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi isingewezekana kutegemea msaada kutoka nje, bila wateja nao kuchangia kwa ongezeko halisi la gharama ya umeme kwa asilimia 4.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero mbalimbali alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini, aliitaka *TANESCO* kushughulikia malalamiko ya wateja hao mbalimbali kwa haraka. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *TANESCO* ilianza mpango wa kununua vifaa vingi vya kuunganisha umeme kutoka nje ya nchi na pia utaratibu wa kuwaelimisha wafanyakazi na wananchi kuhusu huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni Dar es Salaam na Pwani tu ndiyo yenye mita za *LUKU* hadi hivi sasa. Kutokana na gharama kubwa ya mita za *LUKU*, *TANESCO* inabidi ifunge *LUKU* kwa awamu. Hata hivyo katika juhudzi za kupunguza makisio ya baadhi ya ankara, *TANESCO* imeanza utaratibu wa kuingia mikataba na makandarasi binafsi katika mikoa minane ili waweze kusoma mita za wateja kwa wakati na kuziwasilisha *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa ushauri wake wa kuitaka *TANESCO* isambaze gharama za kuunganishia umeme kwa kipindi kirefu ili kuunganishia wateja wengi. Tayari ushauri huu unafanyiwa kazi na *TANESCO*.

MHE. PETER KABISA: Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza. Je, uunganishaji wa *Songas* umemletea mwananchi unafuu gani pamoja na *TANESCO*? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, moja ya mambo ambayo yametokea katika kipindi hiki ni kwa Serikali kuhakikisha kwamba hakuna mgao wa umeme kwa kuhakikisha kwamba umeme unazalishwa vya kutosha. (*Makofii*)

Songas kwa kuunganishwa tunahakikisha au mwananchi anafaidika kwa kuhakikisha kwamba kunakuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme visivyotegemea maji ambavyo wakati wa ukame tunapata matatizo ambayo tumeyapata katika miaka miwili iliyopita na hivyo mwananchi anafaidika kwa kuhakikisha kwamba mchanganyiko vyanzo mbalimbali vya umeme, umeme wa uhakika utaendelea kupatikana.

SPIKA: Nina nafasi ya maswali zaidi, atapewa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, ningombaa pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningombaa kujua kwamba pamoja na *TANESCO* kuboreshwa na kupewa wataalam wa kampuni ya kigeni kwa ajili ya kulientesha ili kuweza kuboresha utendaji wake. Kwa kuwa utendaji bado ni wa kusuasua na wa kuulizana maswali mengi, ningombaa kujua je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuleta sheria ndani ya Bunge ambayo itaanza kuruhusu wawekezaji binafsi katika sekta ya umeme ili waweze kuuza na kusambaza umeme na kuondoa ukiritimba wa msambazaji mmoja ambaye kimsingi anaonekana kushindwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nimeshawahi kutoa taarifa hapa Bungeni juu ya mafanikio yaliyopatikana katika uboreshaji wa Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*) na hatujasema kwamba kila kitu kimekamilika lakini tumetoa taarifa inayoonyesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kutohana na swal la Mheshimiwa Mbunge, kwanza kabisa mfano nilioutoa wa *Songas*, mfano wa *IPTL* na wawekezaji wengine ambao wanaingia hivi sasa nchini ni mifano dhahiri kwamba tayari Serikali katika nyanja ya uzalishaji umeme tayari imesharuhusu wawekezaji binafsi kuingia na kadri shirika linavyokwenda katika mpango wa uboreshaji na urekebishwaji ndivyo tutakavyoweza kufikia katika hatua hizo katika hatua tatu muhimu za uzalishaji umeme, usafirishaji na usambazaji na kuweka ushindani na hata katika jibu langu la msingi nimezungumzia juu ya umuhimu

wa ushindani na jinsi ushindani utakavyoweza kusaidia kupunguza hata bei za umeme hapo baadaye.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi kwa nini Serikali isiweke jitihada kubwa kufunga *LUKU* kwa Mkoa wa Dodoma kwa sababu zoezi hili ni la uhakika kwa wananchi kuhakikisha kwamba wanalipa kiasi ambacho wametumia. Ni nini kigugumizi hasa kinachofanya tusitumie *LUKU?* (*Kicheko/Makofî*)

SPIKA: Nadhani ulilijibu lakini endelea kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi katika swali la kuwafungia wananchi mita za *LUKU*. Kama nilivyosema katika jibu la awali kwamba mita za *LUKU* zina gharama kubwa, ni mara tatu ya mita za kawaida na kutokana na gharama hizi inabidi suala la kufunga *LUKU* iende awamu kwa awamu. Lakini hata hivyo katika mwaka 2005 *TANESCO* tayari imeshapanga kufunga *LUKU* 30,000 nchi nzima katika ufungaji wa mita 60,000 nusu yake itakuwa ni mita za *LUKU*.

Na. 4

Umeme - Vijiji vya Jimbo la Rungwe Magharibi

MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA (k.n.y. MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA) aliuliza:-

Kwa kuwa kasi ya usambazaji umeme katika Jimbo la Rungwe Magharibi ni ndogo na kwa kuwa vituo vya afya na zahanati ishirini katika jimbo hilo havina umeme hali inayosababisha watumishi wa afya kutumia vibatari, koroboi au mishumaa pale dharura zinazopotokea usiku na kwa kuwa umeme wa gridi umeshafika kijiji cha *Mbeya One*, Kata ya Isongole na transfoma imefungwa hata hivyo umeme huo unamnufaisha mtu mmoja tu ingawa wanakijiji zaidi ya arobaini wamefunga nyaya katika nyumba zao na shule ya Sekondari imefunguliwa mwaka huu katika kijiji hicho.

(a) Je, wakati wananchi wa jimbo wanasubiri umeme wa gridi, Serikali inasemaje kuhusu kupeleka nishati ya mionzi ya jua (*Solar Energy*) katika vituo hivyo?

(b) Je, ni gharama gani ya kupeleka nishati ya mionzi ya jua (*Solar Energy*) katika vituo hivyo?

(c) Je, ni lini wananchi wa *Mbeya One*, Kata ya Isongole wataunganishiwa umeme na ni kwa sababu gani hadi sasa hawajapatiwa umeme huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, Serikali imekubaliana na Mheshimia Profesa Mwakyusa, juu ya umuhimu wa kusambaza nidhati ya umeme vijijini katika kuleta maendeleo kadri uwezo wa kifedha unavyoruhusu.

Katika kufanikisha azma hii ambayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, tayari Serikali katika mwaka wa fedha 2003/2004 ilisambaza umeme katika vijiji 52. Aidha, katika kuongeza kasi ya usambazaji umeme vijijini, Serikali imeanzisha miradi minne, Mradi wa kwanza ni wa utafiti wa vyanzo mbalimbali vya umeme vijijini (*Rural Electrification Master Plan*) unaofadhiliwa na mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kiasi cha *Euro* milioni 3. Utafiti huu unaendelea na unatarajiwa kukamlika mwaka 2005.

Mradi wa pili wa *US\$ 2,250,000* unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), una lengo la kupunguza mambo yanaylorudisha nyuma matumizi ya umeme nuru kama vile gharama kubwa za kununua vifaa vya umeme nuru. Mradi huu unafanyiwa majaribio huko mkoani Mwanza na mradi wa tatu una lengo la kukuza biashara ya kueneza umeme nuru nchi nzima. Mradi huu wa *SEK* milioni 27, unatarajiwa kuanza hivi karibuni na utafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA*.

Mheshimiwa Spika, mwisho Serikali kama tunavyofahamu upo utaratibu wa kuanziasha mfuko na wakala maalum wa umeme vijijini kusimamia usambazaji umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, jimbo la Rungwe Magharibi, kama yalivyo maeneo mengine nchini, litafaidika na utafiti unaoendelea, ili kujua kama maeneo mahsusali aliyojataja Mheshimiwa Mbunge yana mwanga wa jua wa kutosha kwa mitambo ya umeme nuru kuweza kufanya kazi. Gharama za umeme nuru zitajulikana baada ya utafiti kukamilika. Hata hivyo, kwa ujumla, gharama hizi hutofautiana kulingana na kiasi cha umeme kinachohitajika. Kwa mfano, kuweka umeme nuru wa kuwasha taa mbili, redio moja, itahitaji *solar panel* moja, *solar battery* moja, *solar regulator* moja, taa za *DC* mbili zote zenye gharama ya shilingi 319,000/= pamoja na *VAT*.

Mheshimiwa Spika, juu ya maombi ya umeme ya wananchi wa *Mbeya One*, Kata ya Isongole, wananchi hao walichelewa kupata umeme kwa sababu ilibidi *TANESCO* waagize transforma nyingine kwa ajili ya wanakijiji hao. Isingewezekana kutumia transfoma aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ambayo ipo umbali wa kilometra mbili na hivyo kuathiri ubora wa umeme ambaa ungepatikana kutoka kwenye transfoma hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa hivi sasa *TANESCO* inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme kwenye kijiji cha *Mbeya One* kilichopo katika Kata ya Isongole ambapo nguzo zimeshajengwa katika kijiji hadi

kwenye shule ya sekondari aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Kazi ya kufunga nyaya za umeme inaendelea na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2004.

MHE. ISMAIL J.R. IWWATTA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba katika Kata ya Isongole ile transfoma moja ilikuwa haitoshi. Kwa hiyo, walikuwa wanafikiria kuagiza transfoma ya pili, je, ni lini hiyo transfoma sasa itafika ili hao wananchi waweze kupata hiyo huduma? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vifaa na mitambo ya umeme nuru ni aghali na hili limedhihirika katika semina ambayo tulifanya na wadau ambao ni wahusika wa huu mradi wa nuru juu huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu wanasema hivi vifaa ni ghali kwa sababu ya kodi kubwa na kodi ya *VAT* na matokeo yake wananchi wengi wanunuua hivi vifaa kutoka upande wa Kenya. Je, Serikali inaweza kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi ili hivi vifaa vipatikane kwa bei nafuu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu lini transfoma itafika, nimeeleza kwamba mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2004 na kukamilika kwa mradi maana yake transforma itakuwa imeshafungwa.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati wa kukamilisha mradi huu na transfoma itakuwa imeshafungwa ili kuwawezesha wananchi kupata umeme.

Kuhusu vifaa kuwa ghali. Nilitaja *VAT* kwa sababu sote tunawajibika kulipa kodi hii ya ongezeko la thamani. Lakini vifaa hivi ni ghali hata bila ya *VAT* na mimi nadhani tusubiri mipango yote na miradi yote ambayo imewekwa bayana hapa katika kujibu swali hili na Serikali ili tuweze kufahamu namna gani na njia gani basi tunaweza tukapunguza gharama hizi za kuhifadhi umeme nuru na kuweza kusambaza umeme nuru katika maeneo mengi nchini.

Na. 5

Uwekezaji wa Fedha za Benki

MHE. MARGARETH A. MKANGA aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kuwa Benki za hapa nchini zina fedha nyingi ambazo hazijawekezwa kwa lengo la kuendeleza uchumi wa nchi kwa ujumla:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?
- (b) Kama ni kweli, je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa fedha hizo zinawekezwa katika sekta mbalimbali za uchumi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Benki za hapa nchini zina fedha nyingi ambazo hazijawekezwa kwa lengo la kuendeleza uchumi wa nchi. Kama itakavyokumbukwa, tangu kuitishwa kwa Sheria ya Mabenki na Asasi za Fedha mwaka 1991, vyombo vya fedha hapa nchini vimekuwa vikifanya shughuli zake kibiashara katika mfumo wa soko huria. Kulingana na mfumo wa soko huria, Serikali haipaswi kuingilia shughuli za mabenki na taasisi za fedha nchini, isipokuwa tu pale yanapovunja sheria au taratibu zilizowekwa zinavunjwa.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kushirikiana na mabeki hayo katika kuboresha mazingira ya kibiashara na kiuchumi na kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo ili kuhakikisha kwamba sekta ya fedha katika mfumo wa soko huria inawanufaisha Watanzania. Aidha, masharti ya mikopo bado ni magumu na hii inatokana na udhaifu wa kimiundombinu katika maendeleo mbalimbali. Hata hivyo, Serikali kwa kuishirikisha na Benki Kuu, imekuwa ikiyashughulikia maeneo haya ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa mikopo kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya ardhi ambayo marekebisho yake yalipitishwa na Bunge hili ili ardhi itumike kama dhamana ya mikopo kutoka kuomba mikopo kwenye mabenki;
- (ii) Kuendelea kuboreshwa kwa Mahakama ya Biashara (*Commercial Court*) ili kuongeza ufanisi katika kutatua mitafaruku ya kibiashara ambayo inahusiana na mabenki;
- (iii) Kupunguza gharama kubwa za uendeshaji wa mabenki pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu kama vile umeme, maji na nyinginezo;
- (iv) Serikali kuanzisha *guarantee schemes* mbalimbali kwa ajili ya kudhamini mikopo ambayo bila kufanya hivyo isingepatikana; na mwisho
- (v) Kutekelezwa kwa mpango wa kurasimisha raslimali na biashara za wanyonge ambayo itasaidia kuongeza idadi ya wananchi watakaofaidika na huduma za benki.

Ni nia ya Serikali kuendelea kufanya kazi maeneo yaliyotajwa hapo kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi na hivyo kuyafanya mabenki yalegeze masharti na kupunguza riba za mikopo. Pia, Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya utamaduni wa kuweka

fedha katika mabenki, kubuni miradi yakinifu, kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati muafaka.

Na. 6

Mafao ya Wafanyakazi wa Mashamba yaliyobinafsishwa

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Mkonge imeshindwa kulipa mafao ya wafanyakazi wa mashamba yake yaliyobinafsishwa na kwa kutokana na ukweli huo Serikali imekubali kimsingi kulipa malimbikizo ya michango ya pensheni ambayo mamlaka husika haikuwasilisha kwenye shirika la *PPF*.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa msingi wa kanuni za pensheni inawajibika kulipa *penalty* ambayo *PPF* inashikilia kama kigezo cha kutowalipa pensheni za wafanyakazi wa mashamba ya Muheza na Mkonge *Livestock Limited*?

(b) Kwa kuwa *PPF* inasitisha kulipa pensheni za wafanyakazi hao kutokana na Wizara ya Fedha kutowasilisha fedha hizo *PSRC/PPF*. Je, lini Wizara ya Fedha itatekeleza wajibu wake ili wafanyakazi hao walipwe pensheni zao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imelazimika kulipia michango ya wafanyakazi wanaoachishwa katika mashirika mbalimbali ya umma ikiwa ni pamoja na riba inayotozwa kutokana na mashirika hayo kushindwa kuwasilisha michango hiyo kwa wakati unaotakiwa kisheria au kutoiwasilisha kabisa. Lengo ni kuwaondolea kero wafanyakazi husika na kuwawezesha kumudu maisha nje ya ajira.

Mheshimikwa Spika, kiasi cha michango pamoja na riba kilikuwa zaidi ya shilingi bilioni 25 hadi kufikia mwaka 2002 kwa mashirika 151 yakiwemo mashamba ya Muheza na *Mkonge Liverstock Limited*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Herbert Mntangi, kwamba kwa msingi wa kanuni za *PPF* zinavyoelekeza Serikali inawajibika kulipa adhabu au *penalty*. Hata hivyo, kutokana na uzito wa deni hili kwa Serikali, Wizara yangu ilifanya mazungumzo na uongozi wa mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) ili waondoe adhabu hiyo. Walikubali kuiondoa adhabu hiyo ambayo ni asilimia 5

inayotozwa juu ya riba ya asilimia 5 (*compunded*) kwa kila mwezi. Aidha, riba imeshuka hadi asilimia 2.5 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imepelekea deni kupungua kutoka shilingi bilioni 25 hadi shilingi bilioni 18.419.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ilikwisha tekeleza wajibu wake ili wafanyakazi hao walipwe pensheni zao kwa kufanya malipo kwa *PPF* katika awamu tatu. Awamu ya kwanza, shilingi bilioni 2.8 zililipwa mnamo mwezi Januari, 2004 na awamu ya pili, shilingi bilioni 2.2 zililipwa mwezi Machi, 2004 na awamu ya tatu shilingi bilioni 13.419 imelipwa kwa Hati Fungani (*Treasury Bonds*) baada ya kusaini mkataba wa maelewano (*MOU*) kati ya Hazina na uongozi wa *PPF* tarehe 8 Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hizo, uongozi wa *PPF* uliandaa mafao ya wafanyakazi wa mashamba ya Muheza na *Mkonge Livestock Limited* chini ya kampuni mama *Tanzania Sisal Board*. Baadhi ya wanachama wamekwishalipwa na zoezi la kuwalipa waliosalia linaendelea kupitia Bodi hiyo.

MHE. HARBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kukubali kulipa hizi *PPF* za wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge. Sasa ni kwamba baadhi ya wafanyakazi wameanza kulipwa na Serikali hapa imetamka kwamba malipo haya yatafanyika kwa awamu tatu.

(a) Je, ni lini awamu hii ya tatu itakamilishwa kwa kulipwa kutoka kwenye Bodi ya Mamlaka ya Mkonge?

(b) Kwa kuwa bado mashamba mengi ya mkonge na Mashirika mbalimbali na taasisi mbalimbali na ikiwemo pia Jumuiya ya Afrika Mashariki, yana madai ya msingi dhidi ya mafao dhidi ya Serikali. Je, ni lini Serikali itatekeleza wajibu wake wa kuwalipa wafanyakazi hao mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Serikali imeshafanya malipo yote kwa *PPF*. Awamu ya kwanza, ilitoa shilingi bilioni 2.8 mwezi Januari na awamu ya pili ililipwa shilingi bilioni 2.2 mwezi wa Aprili na zilizosalia katika awamu ya tatu Serikali imeshalipa tayari kwa kutumia Hati Fungani au *Treasury Bonds* kwa *PPF* kwa hiyo fedha zote ziko *PPF* na utaratibu wa kulipa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, swala la pili ni kuhusu malipo ya mafao kwa wote waliostaifu yanashughulikiwa na Wizara na Serikali na wafanyakazi wote watalipwa haki zao zote za kisheria.

SPIKA: Mheshimiwa Joel Bendera, nilikuona, ngoja ngoja kidogo kuna majibu ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea majibu mazuri ya Naibu Waziri kuhusiana na swali la mafao ya Watumishi wa Afrika ya Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ridhaa yake yenyewe, imeamua kuzungumza na waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa lengo la kufikia muafaka ili iweze kuwalipa hao wafanyakazi mafao yao. Mazungumzo yamekuwa yakiendelea kwa zaidi ya mwezi na wiki iliyopita tu nimekutana na baadhi yao na kuwahakikishia kwamba nia ya Serikali imebaki pale pale isipokuwa ni lazima wafanye mambo mawili:-

(i) Waondoe shauri liliko Mahakamani kwa sababu hatuwezi kuzungumza wakati shauri lipo.

(ii) Wawe tayari kuzungumza, kupunguza maneno tuzungumze haraka ili ikifika mwisho wa mwezi wa Novemba tuwe tumefikia maelewano fulani ndio au hapana. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba tutaendelea kuzungumza nao kwa utaratibu huo na misingi hiyo na kwamba endapo tutaelewa Serikali itakuwa radhi kulipa mafao ya waliokuwa Watumishi wa Afrika ya Mashariki. (*Makofî*)

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mwaka 1997 katika kikao cha wawekezaji wa Mkonge kilichofanyika Korogwe chini ya Uenyekiti wa Rais wetu. Rais aliahidi kwamba mafao yote ya wafanyakazi wa mkonge yatalipwa kwa awamu na alisema kwamba italipwa kwa awamu kama tatu.

Lakini yako madai ya wafanyakazi wengi mpaka sasa hivi bado hawajalipwa na hiyo imekuwa ni kero sugu katika maeneo yote ya mashamba yaliyokuwa chini ya Mamlaka ya Mkonge. Sasa katika jibu la Naibu Waziri alisema kwamba baadhi yao wamelipwa yaani *PPF* imeshalipwa lakini mafao mengine ya msingi hayajalipwa.

Je, Wizara inasemaje kuhusu hili kumalizia ambalo ni ahadi ya Mtukufu Rais?

NAIBU WAZIRI (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joel Bendera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba madeni ama mafao yote jumla mpaka mwaka 2002 yalikuwa shilingi bilioni 25 kwa Mashirika 151. Kwa hiyo, naamini kwamba hata mashamba mengine ya mkonge mbali na haya ambayo Mheshimiwa Herbert Mntangi, aliuliza yaani mashamba ya Muheza pamoja na *Mkonge Livestock Limited* pia yako katika hayo Mashirika 151.

Kwa mashamba ya Muheza pamoja na *Mkonge Livestock Limited*, nijibu kwamba utaratibu wa kutatua tatizo hili lilitokana na madai ya *PPF* kwamba lazima yalipiwe *penalty*. Serikali ilifanya mazungumzo japo yalichukua muda mrefu na *PPF* kwa ajili ya kuondoa ile riba. Hilo lilifanikiwa na ikabaki sasa Serikali kutimiza ahadi yake ya kuwalipa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema Rais aliahidi kwamba wangelipa kwa awamu tatu.

Awamu ya kwanza ilikuwa shilingi bilioni 2.8 zilishalipwa, awamu ya pili shilingi bilioni 2.2 na awamu ya tatu ilikuwa mwezi Aprili, 2004 shilingi bilioni 13.419 zililipwa kwa kutumia *Treasury Bond*. Kwa hiyo, fedha hizi zimeshalipwa na ziko kwenye *Tanzania Sisal Board* ambao ndio walipaji kwa hiyo, ni kati ya *PPF* na *Tanzania Sisal Board* na wahusika ndio Serikali kwa upande wake imeshamaliza wajibu wake kuhusu suala hilo.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akakubali kufuatilia suala hili kwa kuwa wanaouliza masuala hayo ni watu wa Mmbugu, Wabunge wa maeneo hayo ya mkonge wana hakika ya mambo wanayosema kwamba hawajalipwa. Anaweza akafuatilia hili kwa makini kwa sababu maandishi yanaweza yakauziwa mbuzi kwenye gunia? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Semindu Pawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa ushauri wake nitafuatilia na kujua kwamba hali ikoje.

Na. 7

Women Development Fund

MHE. TEDDY L. KASELLA- BANTU aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mifuko ya kuwapa wanawake na vijana mikopo bila kujali itikadi zao ambapo hupeana kwa zamu ili waweze kujikwamua kiuchumi; na kwa kuwa wapo watu wanaoshindwa kutofautisha mikopo na msaada:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaelimisha wananchi kuhusu jambo hilo?
- (b) Je, wale ambao hawalipi hiyo mikopo wanachukuliwa hatua gani?
- (c) Je, mikopo hiyo inatofautishwa vipi kiitikadi ili kuona kwamba hata wale wa Chama Tawala wanalipa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inalo jukumu la kuratibu Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake yaani *WDF* bila kujali itikadi za waomba mikopo. Serikali imeweka bayana kwamba fedha zinazotolewa na Mfuko huu ni mkopo na sio msaada. Ndiyo sababu tumewekeana mikataba na Halmashauri kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mfuko huo. Mikopo hii ina masharti maalum ambapo waombaji wanatakiwa wajunge kwenye vikundi, wapate udhamini ndipo wawepo mikopo. Masharti haya yanaonyesha wazi kwamba kinachotolewa ni mikopo na si msaada. Hali kadhalika asilimia 10 ya riba inawekwa maalum kwa kutoa mafunzo kwa wakopaji ikiwa ni pamoja na kusisitiza haja ya mikopo hiyo kurejeshwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitia wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Halmashauri za Wilaya zinafuutilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa vikundi vinarejesha mikopo hiyo kwa muda unaotakiwa. Baadhi ya mbinu zilizotumiwa na Halmashauri ni pamoja na Mabaraza ya Kata kudhamini vikundi vya wanawake ambapo Halmashauri hizo huchukua jukumu la kuwahamasisha warejeshe mikopo kwa muda uliopangwa.

Vile vile Halmashauri nyingine zinatumia utaratibu wa Benki Kata na Vyama vya Kuweka na Kukopa yaani *SACCOS* kupitishia mikopo ambapo waombaji wanabanwa na taratibu za taasisi hizo kuhusu ukopaji na urejeshi wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ulionzishwa na Wizara yangu ambao unazitaka Halmashauri zirejeshe mikopo kabla ya kupewa fedha nyingine ni mojawapo ya mikakati ya kuhakikisha vikundi vilivyokopa vinarejesha mikopo.

(c) Mheshimiwa Spika, mikopo hiyo kama nilivyosema hapo awali inatolewa kwa vikundi vya wanawake bila kujali itikadi zao. Vile vite ufuutiliaji wa urejeshaji wa mikopo hauangalii itikadi ya mtu au kikundi kinachokopa.

MHE. TEDDY L. KASELA - BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara katika Mkoa wa Tabora hususan Nzega na mimi nilikuwa mmojawapo wa kutembea naye katika ziara hiyo. Kwa kuwa tulionyeshwa vikundi vilivyopewa mikopo toka mfuko huu. Tulionyeshwa vikundi ambavyo walipata mikopo kutoka Mashirika mbalimbali na siyo kutoka kwenye mfuko huu.

SPIKA: Uliza swal.

MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU: Tulipewa taarifa katika makaratasi kwamba mikopo ilitolewa lakini hatukuonyeshwa kikundi hata kimoja. Sasa maswali yangu:-

(a) Je, mikopo ya Nzega ilitolewa vipi na kwa nani na inarudishwa vipi?

(b) Kwa kuwa lengo la mfuko huu ni kujikwamua kwa Wanawake kiuchumi na fedha hizi zinaonekana zimetolewa katika *invisible groups* yaani makundi yasiyoonekana kwa macho. Je, Serikali iko tayari kufuatilia kwa karibu mikopo hii ili fedha hizo ziwafikie walengwa na vile vile kuniweka mimi mmoja wa Wajumbe kufuatilia suala hilo?

WAZIRI WA MAENDELEO JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kama ifuatavyo:-

(i) Taarifa tulizonazo na ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezihakiki ni kwamba Wilaya Nzega kwa mwaka 2000 viliufaika vikundi 17, kwa mwaka 2002 vikundi 17, kwa mwaka 2003 vikundi 17 na jumla ya vikundi vyote vilivyonufaika ni 85. Kwa hiyo, sisi tunao uhakika kwamba vipo vikundi ambavyo vimenufaika.

Kuhusu alivyoviita *invisible groups* hivi ni vikundi ambavyo vipo na Mheshimiwa Naibu Waziri amevihakiki kwa hiyo hatuwezi tukaviita *invisible* labda vikundi ambavyo havikujitokeza kikaonekana kwamba ni *invisible* kwa maana ya Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu anavyosema.

Lakini kama nilivyokwisha kusema kwenye jibu la msingi, Halmashauri kwa taratibu ambazo zimejiwekea zinafuatilia, hali kadhalika wataalam wa maendeleo ya jamii wanafuatilia kuhakikisha kwamba kwanza vikundi vinavyoomba vinachambuliwa na kupewa mikopo hiyo lakini pia kuhakikisha kwamba vinarejesha.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, atakuwa na taarifa nyininge nje ya taarifa ambazo tumezipata hivi karibuni basi tutakuwa tayari kuzipokea na kuzifanya kazi.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Serikali yetu inajitahidi sana kuwasaidia wanawake kwa kuwapa mikopo, lakini kutokana na tatizo sugu la soko yaani bidhaa zao hazina soko jambo linalofanya wanawake hao kutokurudisha mikopo yao kwa wakati uliopangwa, je, Serikali inatatau vipi tatizo hili la soko?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna wakati ambapo bidhaa zinazotengenezwa na wanawake zinakosa soko. Lakini Serikali imechukua hatua kwa Mfuko huu wa Maendeleo Wanawake tumetenga asilimia 10 ambayo inatakiwa kutoa mafunzo. Mafunzo hayo yanalenga kukuza ubora wa bidhaa ili ziweze kuwa na soko zuri lakini pia mafunzo hayo yanatoa mbinu za uwekaji mahesabu, mbinu za utafutaji masoko ili waweze kupenyeza bidhaa hizo kwenye masoko.

Vile vile kupitia Wizara yetu ikishirikiana na vikundi mbalimbali kikiwemo kikundi au shirika lisilo la Kiserikali la *EOTF* kila mwaka tunapokuwa na Maonyesho ya Sabasaba, wanawake wafanya biashara hupata fursa ya kupata mafunzo kushiriki katika maonyesho ili na wao waweze kufungua macho na kuona ni bidhaa gani ambazo zinaweza kuwa na soko kubwa na za ubora wa namna gani.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu tuendelee kushirikiana katika kutoa taaluma hiyo ili bidhaa zinazozalishwa na wanawake ziweze kupata soko kubwa zaidi.

Na. 8

Watoto Kuongoza Kaya

MHE. VENANCE M. MWAMOTO (k.n.y. MHE. DR. LUCY S. NKYA) aliuliza:-

Kwa kuwa janga la UKIMWI linaongezeka siku hadi siku na kwa kuwa mojawapo ya athari za ugonjwa huo ni ongezeko la watoto yatima ambao wengi wao hawapati malezi na matunzo yanayostahili:-

- (a) Je, Serikali inatambua kwamba kuna watoto wanaoongoza kaya?
- (b) Je, Serikali inayo idadi ya kaya zinazoongozwa na watoto nchini?
- (c) Je, Serikali ina mipango gani ya kuwasaidia watoto hao?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lucy Nky, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali, inatambua kwamba zipo kaya zinazoongozwa na watoto hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo takwimu ya idadi ya kaya zinazoongozwa na watoto nchini mwetu. Kwa kuzingatia Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2002, tunatambua kwamba kuna watoto 66,371 Tanzania Bara na watoto 246 Tanzania Zanzibar wanaoongoza kaya. Mikoa yenyе idadi kubwa ya watoto hao ni Mkoa wa Dar es Salaam kwa Tanzania Bara, ambaо ulikuwa na watoto 5,805 na Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar ambaо ulikuwa na watoto 301 wanaoongoza kaya. Kadhalika Mikoa iliyokuwa na idadi ndogo ya watoto hao ni Singida (Tanzania Bara) ambaо ulikuwa na watoto 1,544 wanoongoza kaya na Mkoa wa Kusini Unguja uliokuwa na watoto 70.

Mheshimiwa Spika, ninayo idadi ya watoto hao kimkoa kwa mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo naweza kumpatia Mheshimiwa Mbunge baada ya kujibu swali hili.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mipango ifuatayo ya kuwasaidia watoto hao:-

(i) Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto inayoduruswa, ambayo imezingatia haki za mtoto za kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kutobaguliwa, Serikali imetoa tamko la kisera linalozingatia haja ya kuwezesha kaya zinazoongozwa na watoto, ambapo utekelezaji wake utahusisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Jamii na Asasi zisizo za kiserikali.

(ii) Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2003 hadi 2007, umeelekeza kutolewa misaada ya kiuchumi na kijamii kwa watu, familia na jamii zilizoathirika na UKIMWI wakiwemo watoto yatima na watoto wanaoongoza kaya.

(iii) Serikali pia ina mpango wa kuunda Kamati zitakazoshughulikia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu (*Orphans and Vulnerable Children*) utakaotekerezwa chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii.

Kamati hizo zitawajibika kudhibiti UKIMWI na kusaidia matatizo yanayojitokeza katika familia zilizoathiriwa na UKIMWI. Familia hizo zitahusisha pia kaya zinazoongozwa na watoto.

(iv) Kadhalika, Serikali iliendesha mafunzo kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI katika Halmashauri za Wilaya kuanzia tarehe 16 Machi hadi 26 Mei, 2004. Mada mojawapo iliyotolewa ilihusu mipango shirikishi kwa watu wanaosaidia familia zilizoathiriwa na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na watoto wanaoongoza kaya. Mpango huo unaendelea kutekelezwa na Halmashauri za Wilaya 29 za Tanzania Bara.

(v) Kwa kupitia Mfuko wa Dunia wa Kudhibiti UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, Halmashauri za Wilaya zimepewa fedha ambazo zitatumika kupambana na magonjwa haya ikiwa ni pamoja na kuwasaidia watoto yatima na wale wanaoongoza kaya.

SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto, jina la kimchezo Mheshimiwa Mwafire. (*Kicheko*)

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili.

Kwa kuwa Wilaya ya Makete, ni kati ya Wilaya ambayo waathirika wengi hasa watoto yatima wapo na kwa kuwa wapo baadhi ya watoto ambao pia nao wameathirika na UKIMWI na kwa kuwa Wizara ya Afya imetangaza kwamba ina dawa tayari ambazo zitaanza kutolewa.

(i) Je, Wizara yako itashirikiana vipi kuhakikisha wale watoto ambao ni wakuu wa kaya ambao wameathirika, kupata yale madawa kwa wakati unaotakiwa?

(ii) Kwa kuwa Wilaya ya Makete, kama nilivyozungumza ni Wilaya ambayo imeathirika sana na hawa watoto ambao watatumia hizo dawa wanahitaji kupata chakula, lishe ya nguvu.

Je, Wizara yako itawasaidiaje sasa hao watoto ambao ni wakuu wa kaya hawana uwezo wa kupata chakula kizuri ili waweze kutumia hizo dawa?

SPIKA: Mawaziri wanashauriana kwanza nani ajibu. Eeh Mheshimiwa Waziri wa Afya, naona kura imekuangukia. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu tu swali lile la kwanza tunashirikiana vipi?

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kumhakikishia Mheshimiwa Venance Mwamoto kwamba Serikali ni moja na mpango ni mmoja. Kwa hiyo, hakuna suala kwamba kuna watoto wanaongoza ni wagonjwa wote watashughulikiwa.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la (b) la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo.

Mheshimiwa Spika, *UNICEF* wametangaza Makete kama anavyosema Mheshimiwa Venance Mwamoto, ni kweli kama eneo la maafa. Kweli wale vijana wana matatizo siyo ya dawa tu na lishe kama alivyosema Mheshimiwa Venance Mwamoto. Kwa hiyo, Serikali hivi sasa inafanya utaratibu wa kuunganisha nguvu za wadau mbalimbali pamoja na Serikali yenye wekuangalia uwezekano angalau wa kuwasadia kero ya lishe wale watoto wa Makete. (*Makofifi*)

Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini huzalisha mazao ya chakula (hasa mahindi) kwa wingi sana na kwa kuwa hili lilitokana na upatikanaji wa mbolea na mbegu bora:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mpango wa mwaka 1976 wa kutoa ruzuku kubwa kwa mikoa hiyo ili izalishe kwa manufaa ya nchi nzima?

(b) Kwa kuwa ruzuku ya kusafirisha mbolea toka Dar es Salaam hadi makao makuu ya mikoa ni kidogo sana, je, Serikali isingekubali hili sasa lijadiliwe na kuwashirikisha wakulima ili waone njia nzuri ya kuimarisha uzalishaji?

(c) Je, mpango huo wa ruzuku una mwelekeo gani katika miaka ijayo kwa nia ya kumwendeleza mkulima kama wafanyavyo Ulaya, Marekani na baadhi ya nchi za Asia?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) (b) (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka wa 1976 na 1984, Serikali ilitekeleza mradi maalum wa Kitaifa wa kuendeleza zao la mahindi kwa kutumia mkopo kutoka *BADEA*.

(b) Mradi huo ulijulikana kama *The National Maize Project* na ulikuwa na lengo la kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi. Ili kufikia lengo hilo, Serikali ilitoa ruzuku ya kati ya asilimia 50 na 70 kwa bei za mbolea katika kipindi cha mradi huo.

Mradi wa mahindi wa Taifa ulikuwa na kipindi maalum cha kuutekeleza na ulikuwa na vyanzo maalum vya fedha. Haiwezekani, kwa hiyo, kuufufua mpango huo na Serikali haina mpango wa kuufufua. Badala yake Serikali imeanzisha mipango mbalimbali yenye malengo yanayofanana na yale ya Mradi wa Mahindi wa Taifa wa miaka ya 1976 hadi 1984.

Kuanzia mwaka wa 2003/2004, Serikali ilianza tena kutoa ruzuku kwa mbolea kwa kufidia sehemu ya gharama za kusafirisha mbolea hadi kwenye vituo vilivyoteuliwa kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Katika mwaka wa 2004/2005, mpango huo utapanuliwa kuhudumia nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu sehemu (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Serikali ilisitisha utoaji wa ruzuku kwa mbolea tangu mwaka 1994. Kuanzishwa tena kwa utaratibu huo mwaka 2003/2004 ni hatua inayostahili pongezi. Aidha, mwaka 2003 Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili katika Bajeti yake na katika mwaka huu wa fedha 2004/2005, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.244 zaidi ya mara tatu ya kiasi kilichotengwa mwaka 2003. Kwa vyovyyote vile, kiasi hicho siyo kidogo sana kama ambavyo baadhi ya watu wangetaka kionekane. Kadri uwezo wa Serikali utakavyoongezeka ndivyo Serikali itakavyoongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama wapo watu ambao wana mawazo juu ya njia bora zaidi za kutoa ruzuku ya mbolea, wanakaribishwa kutoa mawazo hayo ili mradi watambue kwamba kiasi cha fedha kinachotengwa na Serikali kinategemea uwezo wake katika kipindi kinachohusika.

Wakati huo huo, Serikali imechukua mikopo yenyе lengo la kumwezesha mkulima kupata pembejeo kwa bei nafuu. Chini ya utekelezaji wa Programu za Maendeleo ya Kilimo chini ya Mkakati wa kuendeleza Sekta ya Kilimo, Serikali imeanzisha Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo (*PADEP*), ulioanza kutekelezwa mwaka 2003 kwa mkopo wa shilingi bilioni 56.8 kutoka Benki ya Dunia. Chini ya mradi huo, wakulima watakopeshwa mbolea kwa ruzuku ya 50% ya bei na mahitaji mengine ya kilimo, kwa mfano zana za miundombinu kwa ruzuku ya asilimia hadi 80.

Mradi mwengine unaojulikana kama Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*DASIP*) utaanza kutekelezwa mapema katika mwaka 2005 na utaratibu wake ni kama ule wa *PADEP*. *DASIP* itatumia mkopo wa shilingi bilioni 60.9 kutoka *ADB*. Tunaandaa miradi itakayohudumia Wilaya ambazo hazihudumiwi na *PADEP* na *DASIP* na kwa kuanzia, uwezo wa Serikali utaelekezwa zaidi kwenye Wilaya hizo.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ametueleza kwamba katika miaka ya sabini, waliweza kutoa ruzuku ya *50 to 70 percent* na katika mipango ijayo anatuambia atatoa kwenye *80 percent*.

Je, anaona utata gani sasa kwa kipindi hiki ambacho Tanzania tunahitaji uzalishaji zaidi na tumefungua masoko kuweza kuongeza ruzuku badala ya kutoa ruzuku kwa ajili ya usafirishaji tu ambayo ni kama *token* kwa mkulima inaonyesha katika msimu uliopita?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu katika jibu la msingi, ni kuwa upo utaratibu wa kutoa unafuu katika misaada iliyosemwa. Kwa mfano, ule mradi wa *PADEP* mkopo ni wa shilingi bilioni 56.8 kutoka Benki ya Dunia. Chini ya mradi huo wakulima wanakopeshwa

mbolea kwa ruzuku ya asilimia 50 ile ile aliyoitaja ipo na vile vile siyo tu hii ya mbolea na vitu vinginevyo. Kwa mfano miundombinu kwa asilimia hadi 80 kwa hiyo, utaratibu upo na kwa sasa Serikali ina uwezo huu tuliotaja tutakapoongeza uwezo tutatoa nafuu zaidi kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Na. 10

Dawa ya Kutunza Mazao

MHE. MARTHA M. WEJJA aliuliza: -

Kwa kuwa, wakulima wa mazao ya chakula wanapata tatizo kubwa la mdudu anayeharibu mazao kama mahindi, kunde, mtama na maharage, aitwaye dumuzi na kwa kuwa dawa inayotumika kuhifadhi chakula/nafaka haifai kutunza chakula kwa mwaka mzima kwani baada ya miezi mitatu au minne mdudu huyo hujitokeza akiwa ameshabangua chakula chote hasa mahindi:-

- (a) Dawa inayoagizwa huwa imetengenezwa miaka mingapi huko inakotoka?
- (b) Je, Wizara itaanza lini kuagiza dawa nzuri inayoweza kutunza chakula kwa muda mrefu?
- (c) Je Serikali inatoa tamko gani kwa wenyewe maduka ya dawa ambazo muda wake wa kutumika umeshamalizika ili yasiuzwe kwa wakulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Wejja, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kuna madawa ya aina nyingi yanayoweza kutumiwa kudhibiti wadudu wanaoharibu nafaka akiwamo dumuzi. Aina tano za madawa ya unga ndizo zinazotumika zaidi humu nchini na yote yana uwezo wa kuhifadhi nafaka kwa muda wa miezi 12 iwapo masharti ya kuyatumia yatakuwa yamezingatiwa na kutegemea hali ya hewa. Kwa mfano, madawa hayo huisha nguvu haraka zaidi katika mazingira ya joto kali na unyevunyevu mkubwa. Madawa hayo yanajulikana kwa majina ya kibashara kama *Stocat Super Dust, Shumba Super Dust, Nafaka Dust, Super Grain Dust* na *Actellic Super Dust*. Madawa hayo hutofautiana na mchanganyiko wa kemikali na makampuni yaliyotengeneza.

Kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria ya Kudhibiti Visumbufu vya Mimea Na. 13 ya mwaka wa 1997 (*The Plant Protection Act, No. 13 of 1997*), madawa yanayoruhusiwa kuingizwa humu nchini ni yale tu yaliyosajiliwa baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo wa kutosha wa kudhibiti visumbufu vinavyohusika kwa kutumia utaalamu na mbinu zilizopo na ambapo yakitumika kwa usahihi hayataleta madhara kwa afya za binadamu na wanyama na

yatachafua maji na mazingira. Jambo muhimu ni madawa hayo kuwa na sifa zinazotakiwa yanapoingizwa nchini na mara nyingi huwa yametengenezwa katika muda usiozidi miezi 12 kabla ya kuingizwa nchini.

(b) Uingizaji wa madawa hufanywa na wafanyabiashara binafsi waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti Visumbu vya Mimea Na. 13 ya mwaka 1997. Wizara ya Kilimo na Chakula haiagizi madawa bali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo ili kuhakikisha kwamba madawa yenye sifa zinazostahili ndiyo tu yanayoingizwa nchini.

(c) Kwa mujibu wa kifungu Na. 20 cha Sheria ya Kudhibiti Visumbu vya Mimea Na. 13 ya 1997, mtu ye yote anayeuzwa madawa anapaswa kuonesha tarehe za mwisho ya kutumiwa kwa madawa hayo na iwapo itagundulika kuwa anauza madawa yaliyopita muda huo, atakuwa amevunja sheria na atastahili kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitatu au faini na kifungo kwa pamoja. Serikali inaagiza wafanyabiashara ya madawa wasiuze madawa yasiyokuwa na sifa zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na madawa yaliyokwisha muda wake.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la moja la nyongeza. Kwa kuwa madawa ya nafaka mengi ni mabovu kwenye maduka yetu yaliyoko mikoani na wilayani na Serikali iliwhi kutoa tamko hapa kwamba itafanya jitahada za kutosha ili dawa nzuri zifike huko, je, ni nani huwa anakagua haya madawa huko wilayani na mikoani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula ningeomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai, kama lifuatavyo: -

Kama kuna madawa mabovu basi wamekiuka baadhi ya mambo niyataje hapa ni kuwa madawa yamekaa muda mrefu yanapoingia nchini yanakuwa kamili kamili. Lakini baada ya kukaa muda mrefu bila kutumika kama nilivyooleza inaweza ikatokea hiyo athari uliyosema. Wanaokagua sasa ni Idara ya Kilimo, kule kuna wataalam wanaohusika na madawa hayo ambao kila wakati wanapita katika maduka kukagua, kuona madawa gani yamepitwa na wakati na yale wanayoyaona mabovu wanayaondosha. Wizara ya Kilimo na Chakula katika ngazi ya wilaya na mkoa wapo wataalamu hao. (*Makofii*)

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu kiasi fulani ambayo ni mazuri kutoka kwa Waziri lakini nilitaka niulize. Kwa kuwa madawa haya vifungashio vyake havionyeshi wazi tarehe ya *ku-expiry* au kuharibika na wananchi wanaponunua hawajui na hakuna mtu huko wilayani ambaye anawaelimisha hawa na dawa hizi zinaharibika na zinaharibika wakati mwananchi alikwishaweka mwaka mmoja au miezi sita.

Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hasara inayowapata wananchi inarekebishwa na wananchi wanalipwa fidia kwa hasara hiyo? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula napenda kujibu swali Mheshimiwa Henry Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida kiutaratibu tarehe inaonyesha, inaonyeshwa hakuna dawa inayoingia nchi isiyofuata masharti niliyoyataja, kwa hivyo ni jukumu la kila mwananchi na hasa mkulima kusoma yale maelekezo na nawaomba.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu la Waheshimiwa Wabunge tuwaelimishe wananchi wetu wasiathirike na mambo hayo. (*Makofi*)

Na. 11

Mradi wa Maji kwa Shirika la *World Vision International*

MHE. MUSA A. LUPATU aliuliza: -

Kwa kuwa, Shirika lisilo la Kiserikali la *World Vision International* limetoa msaada wa kujenga mradi wa maji katika Kata ya Bungu na Dindira, Wilaya ya Korogwe: -

(a) Je, mradi huo utagharimu fedha kiasi gani na utakamilika lini?

(b) Katika jumla ya gharama katika sehemu (a) ya swali hili, je, ni kiasi gani cha michango kinatolewa na Shirika hilo na ni kiasi gani kinatolewa na Serikali na vijiji?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo: -

Mwaka 1999, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ikishirikaina na wananchi ilibuni mradi wa maji kwa ajili ya kuwashudumia wananchi wa vijiji vya Bungu, Manka, Msasa, Ngulu, Kwemshai na Bungu Manka yenye jumla ya wakazi wapatao 17,160.

Mradi ulianza kujengwa mwaka 2002 kwa ushirikiano na Shirika la *World Vision International*, Halmashauri ya Wilaya pamoja na wananchi. Katika utekelezaji wa mradi, Shirika hilo linalo jukumu la kutoa vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mabomba na viungio vyake, wakati wananchi watatoa vifaa kama mchanga, mawe na kokoto pamoja na kuchimba mtaro, kulaza na kufukia mabomba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi. kama ifuatavyo: -

(a) Mradi unakadiriwa kugharimu shilingi 452,040,000/= na utakamilika mwaka 2006.

(b) Katika jumla ya gharama nilizozitaja, Shirika la *World Vision International* litatoa shilingi 431,931,902/= na wanachi wanachangia shilingi 11,244,498/= na Halmashauri itatoa utaalamu, ushauri na usimamizi kwa gharama ya shilingi 8,864,000/=.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuchukua nafasi hii kulishukuru na kulipongeza sana shirika la *World Vision International* kwa kushiriki vizuri sana katika miradi kadha ya maji nchi. Naomba waendelee na moyo wao huo. (*Makofi*)

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali hili nililouliza na pia mimi niwapongeze *World Vision* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa maendeleo ya wananchi wa Korogwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninalo swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wanachangia fedha na nguvu zao na kwa kuwa wananchi wanayo miradi mingi ambayo wanachangia hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya miradi kama huu wa *World Vision* amba ni wa maji, je, Serikali inaweza ikakubali kwamba katika mradi wa maji vijijini amba unaanza mwaka huu sehemu ya fedha hizo za mradi huo zitumike kusaidia nguvu za wananchi katika mradi huo?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musa Lupatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Korogwe kwa moyo wao wa kuchangia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa jinsi ambavyo katika mradi huu wamechangia vizuri na ni matumaini yangu mradi wa Benki ya Dunia unapokuja watachangia. Vilevile haiwezi kuwa mbadala, wataanzisha miradi mingine na watalazimika kuchangia. Kuchangia ni sera ya chama chetu na inafanya kazi vizuri tuiendeleze. (*Makofi*)

Na. 12

Huduma za Simu - Kisarawe

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO aliuliza: -

Kwa kuwa, Wilayani Kisarawe hakuna huduma za TTCL isipokuwa pale makao makuu ya Wilaya, Kiluvya na kandokando ya barabara ya Dar es Salaam na

Morogoro, na kwa kuwa upimaji wa vituo vyatya simu ulishafanyika katika vijiji vya Mzenga, Maneromango, Msanga, Chole na Masaki tangu mwaka 2002: -

(a) Je, ni lini Serikali itaweka simu katika maeneo hayo na mengine katika Wilaya ya Kisarawe?

(b) Kampuni ya simu za mikononi zitaamua lini kufikisha simu katika Wilaya hiyo na nje ya mji mdogo wa Kisarawe?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Mheshimiwa Waziri Mawasiliano na Uchukuzi, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, napenda nitoe ufanuzi mdogo ufuataao:-

Mheshimiwa Spika, upimaji wa vituo vyatya simu katika vijiji vya Mzenga, Maneromango, Msanga, Chole na Masaki, bado haujafanywa.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi huo sasa napenda kujibu swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Kampuni ya Simu inayo nia thabiti ya kupeleka simu za kisasa (pamoja na simu za vibandani) kwenye vijiji vyenye mwelekeo wa kibashara lakini utekelezaji wake unakwama kwa sababu ya uhaba wa fedha. Kila mwaka Kampuni inaazimia kupeleka huduma ya simu katika baadhi ya vijiji lakini Bajeti ni finyu.

Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma ya simu za kisasa vijijini nchini kote, Serikali ina mpango wa kuanzisha mfuko maalum ujulikanao kama *Universal Access Fund* kwa ajili hiyo. Ni mategemo yetu kuwa mara mfuko huo utakapoanza kutumika, tatizo la ukosekanaji wa huduma za simu za kisasa vijijini litapungua kwa kiasi kikubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni za Simu za mikononi zinaendelea kufanya tathmini maeneo mbalimbali nchini ili kuweka mitambo yao ya simu. Baadhi ya mambo muhimu yanayozingatiwa katika kuweka mitambo yao ni pamoja na gharama za kujenga mtambo wa simu, ubora wa eneo husika kibashara na urahisi wa kupata au kujenga njia za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa juhudzi zake za karibu za kufutalia shughuli za wapiga kura wake.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambaye siku zote anajibu vizuri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya Kampuni hizi za simu za mikononi nimezungumza nao wako tayari kupeleka simu kule lakini wanakwamishwa na ukosefu wa umeme kule vijijini, je, Serikali inafanya jithada gani kuhakikisha kwamba umeme umefika ili kuwezesha kampuni hizi ziweze kuweka mtandao wa mawasiliano?

Swali la pili, iwapo haiwezekani umeme kuwepo hivi karibuni, je Serikali iko tayari kuweka vituo angalau viwili tu vya umeme juu ambavyo vitawezesha kampuni hizi ziweze kusambaza mawasiliano katika maeneo ya Kisarawe? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Athuman Janguo, kama ifuatavyo:-

Mimi naamini maswala ya umeme vijijini sekta inayohusika itashughulikia ipasavyo na watahakikisha umeme unafika maeneo hayo. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kampuni za simu zinapoweka mitambo yake huwa wanaweka *Solar Panel* kwa lengo kwamba sehemu nyingine hakuna umeme kwa hiyo zile *Solar Panel* zinakidhi mahitaji hayo. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kule Kisarawe Kampuni ya *Mobitel* imepeleka huduma zake na wameweka mitambo yao kwa kutumia *Solar Panels* na tutawaomba Waheshimiwa wanao husika na sekta ya umeme waharakishe maendeleo ya umeme ili huduma za simu ziweze kutanuka. Ahsante.

Na. 13

Kitengo cha Majengo

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA aliuliza: -

Kwa kuwa kuna kitengo maalum kinachoshughulikia majengo kilichopo Wizara ya Ujenzi na Mikoani.

- (a) Je, kitengo hicho kimekabidhiwa kazi ya kupima viwanja kwenye maeneo ambayo Wizara ilipima maeneo hayo lakini haikujenga nyumba?
- (b) Je, viwanja vinavyopimwa na kitengo hicho inawauzia akina nani na ni kiasi gani cha fedha kinapatikana na nani anayedhibiti/kukagua hesabu hizo?
- (c) Je, inakuwaje Halmashauri husika ambako maeneo hayo yanapimwa hazishirikishwi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Katika muundo wa Wizara ya Ujenzi uliopitishwa na Serikali, hakuna Kitengo cha Nyumba kilichopo Wilayani na Mikoani isipokuwa kuna Wakala wa Majengo (*TBA*) ulioundwa chini ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1997. Wakala wa majengo una Ofisi Mikoani pia. Majukumu ya wakala wa majengo ni pamoja na haya yafuatayo: -

- (i) Kutunza nyumba za Serikali zinzomilikiwa na Wakala;
- (ii) Kutekeleza utaratibu wa kujenga na kuwauzia Watumishi nyumba za kuishi kutokana na fedha zinazolipwa na watumishi waliouziwa nyumba;
- (iii) Kutoa huduma ya Ushauri (*Consultancy*);
- (iv) Kuhakikisha kuwa Majengo ya Serikali yanajengwa na kutunzwa kwa kuzingatia viwango viliwyokubalika;
- (v) Kusimamia upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya matumizi ya Serikali; na
- (vi) Kupima maeneo yote ambayo yalitengwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo hayakupimwa lakini yamejengwa majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Wakala wa Nyumba (*TBA*) hauhusiki na kupima na kugawa/kuuza viwanja. Jukumu la kupima na kugawa ama hata kuuza viwanja liko Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na ndio wanaokusanya fedha za malipo ya viwanja. Halikadhalika kushirikisha na Halmashauri husika wakati wa kuandaa maeneo ya kupima viwanja.

Hata hivyo, Wakala wa Majengo (*TBA*) hupima maeneo yake ambayo Wizara imekabidhiwa kwa madhumuni ya kujenga nyumba za Serikali.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Spika, asante naomba kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa wakati wa Bajeti ya Wizara hii Waziri aliahidi kulifutilia hili jambo ambalo lilitokea Kibaha na nilieleza mpaka na jina ni nani, je, Waziri atatueleza alipolifutilia na viwanja hivi vinauzwa kwa watu binafsi badala ya kupeleka Serikali amechukua hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Ni kweli wakati wa Bajeti Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, alizungumza juu ya swala la mtaalamu wa Wizara ya Ujenzi ambaye anauza viwanja Kibaha. Tumefuatilia yeye hauzi viwanja vya Serikali kwa hiyo, baada ya kujua kwamba viwanja vyetu sisi tulivyopewa kama Wizara ya Ujenzi viko salama vingine havituhusu. (*Makofit*)

Na. 14

Ujenzi wa Barabara ya Mbeya - Makongolosi

MHE. PAUL E. NTWINA aliuliza: -

Kwa kuwa ni muda mrefu umepita tangu Serikali ianze mipango yake ya ujenzi wa barabara ya lami toka Mbeya - Chunya - Makongolosi, na kwa kuwa wananchi wangependa kuishauri Serikali kwamba kuiunganisha Mbalizi na kufanya Wilaya kuwa na mtandao mzuri wa barabara za lami kama ilivyo kwa Wilaya Mkoani Mbeya: -

(a) Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kwa kuziunganisha barabara hizo kungechochea sana maendeleo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbeya hadi Makongolosi yenyewe urefu wa kilometra 110 ni sehemu ya barabara Kuu ya Mbeya hadi Rungwe yenyewe urefu wa kilometra 295. Barabara hii ambayo inaunganisha mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani ya Singida na Tabora imejengwa kwa kiwango cha Changarawe. Serikali tayari inao mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara hii yenyewe urefu wa kilometra 110 yaani kutoka Mbeya hadi Makongolosi. Kampuni ya Uhandishi Ushauri ya BCEOM kutoka Ufarasa imepewa jukumu la kufanya usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni. Kazi hii imepangwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja yaani ifikapo tarehe 23 Februari, 2005 na itaigharimu Serikali kiasi cha shilingi milioni 780.264. Baada ya hatua hiyo kukamilika taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zitafuata.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi - Makongolosi yenyewe urefu wa kilometra 117.8 ni ya Mkoa. Barabara hii imejengwa kwa kiwango cha changarawe/udongo na ni kiungo muhimu kati ya makao Makuu ya Wilaya ya Chunya na Mkoa wa Mbeya kwa Kupitia vijiji vya Makongolosi, Saza, Mkwajuni, Galula, Mjele, Mapogolo, Mshewe na mji mdogo wa Mbalizi. Sehemu kubwa ya barabara hii inapita kwenye bonde la Ziwa Rukwa ambapo ardhi yake ni mchanga hali ambayo husababisha barabara kuharibika mara kwa mara kutokana na udhaifu wa tabaka lake la chini (*Subgrade*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo machache, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Kama nilivyoanisha katika maelezo yangu ya utangulizi, barabara kuu ya Mbeya - Chunya - Makongolosi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mara tu usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuini utakapokamilika.

(b) Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali imeweka kipaumbele cha kuweka lami kwenye barabara kuu kwanza, hivyo basi haina mipango ya karibuni ya kuiwekea lami barabara ya Mkao Makongolosi - Saza - Mkwajuni - Galula hadi Mbalizi. Nia ni njema lakini uwezo ni mdogo.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa nia ni njema ya kujenga barabara hii ya Mbalizi - Makongolosi na kwa kuwa katika jibu lake la msingi hakutaja sehemu ndogo iliyojengwa kwa lami. Katika awamu iliyopita walijenga sehemu korofi kwa lami.

(i) Je, atakubali zile sehemu korofi zijengwe kwa lami kama anavyojibu mara kwa mara au kwa kitu ambacho kinaweza ku-*stabilize* huo udongo ukawa mgumu?

(ii) Kwa nini Serikali haitumii njia kama zinazofanyika sehemu nyingine utaratibu ule wa kujenga barabara nusu lami na nusu udongo ili kama fedha hazitoshi waweze kumalizia eneo la pili wakati mwingine kama vile wanavyofanya Zimbabwe na Tunisia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe.

Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Paul Ntwina, jinsi alivyokuja safari hii juu ya barabara hii na kuifua tilia sana na bado naomba akubaliane na mimi majibu nitakayompa kwa sababu yatazingatia mambo yale yale tuliyozungumza ofisini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, barabara hii kuna sehemu korofi ambayo tumeitengeneza kwa lami kwa sababu ni korofi sana na ni kawaida yetu pale ambapo barabara inakuwa korofi na Serikali inaouwezo inapunguza ukorofi wa barabara kwa kutengeneza kipande hicho kwa lami. Kwa hiyo, ndio sababu kubwa tumetengeneza sehemu ndogo hiyo kwa lami sio kwamba tulikuwa tunaanza kutengeneza barabara nzima kwa lami na huwa tuna utaratibu huo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mbona hatfuatili utaratibu wa wenzetu, kwa mfano Malawi na kwingine kutengeneza barabara nusu lami nusu udongo. Mimi sijui utaratibu wao na sababu zao lakini sisi hapa utaratibu huo hatuna tunachojaribu ni kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami, kiwango cha changarawe na kiwango cha udongo. Sasa kiwango

cha lami na nusu udongo halafu lami kuweka vilaka kwenye barabara nafikiri sio utaratibu mzuri kwa nchi hii.

SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na yamekwisha kabla ya wakati wake kwa sababu swali ambalo lingekuwa la kumi na tano na la mwisho kwa siku ya leo liliondolewa baada ya kugundua kwamba halihusu Serikali ya Muungano bali linahusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kwa hiyo, sasa maswali yamekwisha tunaendelea na shughuli nyingine, kwanza matangazo, tuna tangazo moja la kikao cha Kamati nayo ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba leo tarehe 2 Novemba, 2004 kikao kitafanyika saa tano asubuhi chumba Namba 231 ghorofa ya pili.

Mwisho wa tangazo, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

Subiri kidogo nimeghafilika kwamba kwa huu ni wakati wa Ramadhan, inabidi tubadilishe saa za Bunge kukaa hasa saa za jioni ili tuweze kumaliza shughuli zetu saa kumi na mbili badala ya saa mbili kasoro robo kama ilivyokawaida.Kwa hiyo, ili hilo liweze kufanyika inatakiwa hoja itolewe ya kuomba ruhusa hiyo. Haya sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, *Chief Whip* wa Serikali atoe hoja hiyo.

KUTENGUA KANUNI YA MUDA WA KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 21 kifungu kidogo cha sita, naomba Bunge lako likubali kuahirishwa kabla ya muda wake kila siku saa kumi na mbili badala ya saa moja na dakika arobaini na tano ili Waheshimiwa Wabunge waliofunga wawayi kuswali naomba kutoa hoja.

SPIKA: Ngoja na kuanza, kuanza.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Kila siku Bunge lianze saa kumi jioni badala ya saa kumi na moja na liishie saa kumi na mbili badala ya saa mbili kasoro robo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Muda wa kuanza na kumaliza Kikao cha Bunge wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulipitishwa na Bunge)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 yaani The Written Laws (Miscellaneous Amendements) Bill, (No. 3), 2004

(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

(Kusomwa Mara ya Pili)

**Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004
(The National Economic Empowerment Bill, 2004)**

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Uwezeshaji wa Watanzania Kiuchumi sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaeleza maudhui ya Muswada, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, kwa kujadili na kuupitisha Mumswada huu. Ushauri wa Kamati ilikuwa hatua ya mwisho iliyowezesha kukamilisha kwa maandalizi ya Muswada huu kabla ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Serikali ya kurekebisha Muswada, mchango wa wajumbe wa Kamati umeiwezesha Serikali kuandaa jendwali la marekebisheshio yenyeh lengo la kuboresha maudhui ya Muswada. Ni imani yangu kwamba Wabunge wote wamegawiwa jedwali la marekebisheshio.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unatoa mapendekezo kuhusu kutungwa Sheria itakayowezesha Watanzania kushiriki kikamilifu zaidi katika shughuli za kiuchumi. Chimbuko la Muswada huu ni sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Watanzania ambayo ilizinduliwa na Serikali mjini Dodoma hapa Bungeni tarehe 19 Juni, 2004. Sera hii ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri, iliyoteuliwa na Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri wa Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 15 Desemba, 2000.

Kufuatia maagizo ya Baraza la Mawaziri chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamins William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kikao chake cha tarehe 4 Machi, 1999. Waziri Mkuu aliunda Kamati nyingine ya wataalamu ambayo aliipa kazi ya kutoa mapendekezo ya mikakati ya utekelezaji. Katika kutafuta maoni ya wadau, Kamati hizi zilijitahidi sana kupita mikoani na kupata maoni kutoka taasisi mbalimbali za nje na ndani na pia Kamati ilipata nafasi ya kupata maoni ya

Waheshimiwa Wabunge kuitia semina iliyofanywa hapa Bungeni tarehe 6 Februari, 2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua kadhaa za makusudi zilizochukuliwa na Serikali katika kuwawezesha Watanzania kushiriki katika shughuli za kiuchumi hadi sasa Serikali imedhamiria kuchukua hatua zaidi za kuwawezesha Watanzania washiriki kwa kiwango cha juu zaidi katika uendeshaji wa uchumi. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imedhamiria kuunda chombo cha Kitaifa ambacho kitabuni, kuratibu na kusimamia shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Baraza la Uwezeshaji litakaloundwa litakuwa na kazi ya kuainisha na kuratibu fursa mbalimbali zilizopo katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara na sekta zote zinazo fursa ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kuitia sera au kufanya marekebisho kadhaa katika sheria mbalimbali kama itakavyopendekezwa na Baraza la Uwezeshaji. Utaratibu mzima utafafanuliwa kwenye Kanuni zitakazotungwa kwa lengo la kufafanua na kutekeleza vizuri sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada huu ina ibara tatu ambazo zinahusu maelezo ya utangulizi kama vile jina, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya maneno hayo ni Waziri mwenye dhamana ya uwezeshaji kwa mujibu wa Muswada huu Waziri mwenye dhamana ni Waziri Mkuu, aidha, sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara tu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ina ibara kumi, yaani ibara ya nne hadi ibara ya 13. Sehemu hii inaweka masharti kuhusu uanzishaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi. Jukumu kubwa la Baraza litakuwa kutekeleza sera ya Taifa ya Uwezeshaji ambayo imeshapitishwa na Serikali.

Sehemu hii pia inafafanua kwa kina mbinu na mikakati itakayotumika katika kutekeleza jukumu hili. Aidha, Muswada unaeleza kwamba Baraza litakuwa na Wajumbe tisa, ambayo itajumuisha Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na Wajumbe nane watakaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Sheria hii ambaye ni Waziri Mkuu. Mtu atateuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza kwa miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kuwa Mjumbe kwa kipindi au vipindi vingine vyaa miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Baraza la Uwezeshaji, Muswada unapendekeza kwamba Baraza litakutana kila robo mwaka na unatoa maelezo ya utaratibu wa kufuatwa na Baraza katika kufanya maamuzi yake. Katika kuteua Wajumbe wa Baraza, Waziri atatakiwa kuhakikisha kwamba sekta ya umma na sekta binafsi zinawakilishwa kikamilifu kwenye Baraza.

Aidha, Wajumbe watakaoteuliwa wanatazamiwa kuwa na hadhi na uzoefu wa kutosha. Muswada unalipa Baraza uwezo wa kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Ofisi

yoyote ya Serikali, Mashirika binafsi au Taasisi inayoona inafaa. Katika sehemu hii Muswada unazungumzia pia suala la uajiri wa wafanyakazi wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu yenye ibara ya 14 mpaka ya 15 inahusu Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais. Katibu Mtendaji ndiye Katibu wa Baraza na Mkuu wa *secretariat* ya Baraza. Yeye atasimamia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza pamoja na shughuli za kila siku za Baraza la Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ina ibara ya 16 hadi ya 28, sehemu hii inaweka masharti kuhusu kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji utakaojulikana kama *The National Economic Empowerment Fund*, aidha, sehemu hii inaeleza madhumuni ya mfuko huu, chanzo cha mfuko huu utatokana na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada, mikopo na mapato yatakayozalishwa na mfuko wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 5 ina ibara ya 29 hadi ya 35 ambazo zinahusu usajili wa Taasisi na Mashirika yatakayoshiriki katika uwezeshaji wa Tanzania kiuchumi. Sehemu hii imeweka bayana masharti kuhusu kusajili Taasisi na Mashirika, taratibu hizo za usajili pamoja na majukumu ya Taasisi na Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ina ibara ya 36 hadi ya 40 na inahusu mambo mawili makubwa. Kwanza ni mapato na matumizi ya Baraza na pili uwekaji wa hesabu na ukaguzi wake. Kila mwaka Baraza litawasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Waziri. Baraza litafanya hivyo kwa kuzingatia Sheria ya fedha ya umma ya mwaka 2001, hesabu na vitabu vitakaguliwa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali. Kwa kuitia kwa Waziri, Baraza litawasilisha Bungeni taarifa ya kila mwaka yaani *annual report* vile vile Sheria inalipa Baraza uwezo wa kuwasilisha taarifa nyingine zozote muhimu kwa Waziri juu ya jambo lolote linaloweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba inajumuisha ibara ya 41 hadi ibara ya 44. Sehemu hii inaweka masharti kuhusu mambo kadhaa madogo madogo yaani *Miscellanies Provisions*. Yapo majedwali mawili. Jedwali la kwanza ni fomu namba NEE01 kwa ajili ya maombi ya usajili wa shughuli za kiuchumi na jedwali la pili ni fomu namba NEE02 ambayo ni cheti cha usajili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyosema hapo mwanzo Serikali imefanya marekebisho kadhaa katika Muswada huu kama mlivyoona katika karatasi ya marekebisho kama ifuatavyo:-

- (i) Baraza la uwezeshaji litakuwa na hadhi ya kisheria.
- (ii) Bodi ya dhamini imeondolewa.
- (iii) Marekebisho madogo madogo yenye madhumuni ya kuboresha uandishi hususan mtiririko wa namba za ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Tuna wasemaji waliokwishajiandikisha 15, kwa hiyo, tunafikiri watatosha kwa muda huu uliotengwa kwa ajili ya Muswada huu. Sasa namwita msemaji wa Kamati, ye ye yuko hapa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala atoe maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa mwaka 2004 (*The National Economic Empowerment Bill, 2004*). Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati yangu ilikutana Dar es Salaam tarehe 20 Oktoba, 2004 kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika kutafakari, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu adhma yake ya kuleta Muswada huu kama alivyoeleza mtoe hoja. Aidha, katika utaratibu wa kusikiliza maoni ya wadau, Kamati ilipata fursa pia ya kusikiliza maoni ya mdau kutoka kituo cha Sheria na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni namba 70 kifungu kidogo cha pili Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nikianza na maoni ya jumla ni kwamba Kamati inaridhika kuwa malengo ya Muswada huu ni mazuri na kama Sheria ikianza kutumika itasaidia sana kuwawezesha Watanzania wengi kiuchumi kuanzia wale wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, ukiacha maoni hayo ya jumla, Kamati yangu iliupitia Muswada huu ibara kwa ibara, katika kufanya hivyo Kamati haikusita kutaka ufanuzi katika maeneo kadhaa. Kati ya maeneo hayo ni maelezo yaliyotolewa na Serikali kuwa Muswada huu utatumika Tanzania Bara kama ilivyoelezwa katika ibara ya pili ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni Kamati ilitaka kuona kuwa Muswada huu unahusisha pande mbili za Muungano. Maelezo ya Serikali yakawa suala hili si la Muungano, lakini kwa kuzingatia maingiliano ya kibiashara na kiuchumi yaliyopo katika pande zote mbili za Muungano ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Kamati yangu inaona kuwa Sheria hii itawanufaisha Watanzania wote kisera popote pale walipo ndani ya Muungano. Kwa hiyo, Serikali ya Muungano iwasiliane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu Sheria hii ili waone jinsi ya kuitumia kulingana na mazingira ya kwao.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilitoa tamko kuwa kisera Sheria hii itawasaidia Watanzania wote na kwamba itafanya jitihada kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama tulivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati ilionyesha wasiwasi wake ni kuhusu kuiweka Sheria hii chini ya utaratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu wakati tayari kuna Ofisi ya Rais, Mipango na Ofisi ya Makamu wa Rais Kuondoa Umaskini, ambazo kimsingi zote zinashughulika na kumwezesha mwananchi kiuchumi kwa namna moja au nyingine.

Kwa hiyo, Kamati ilitaka ipatiwe maelezo kuhusu usimamizi wa pamoja bila kuwepo na migongano.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe ufanuzi wa kina kuhusu nia yake ya kuiweka Sheria hii chini ya utaratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na kuithibitishia Kamati kuwa hapatakuwa na migongano. Kamati iliridhika na ufanuzi uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya saba ya Muswada, Serikali ilileta pendekizo la uteuzi wa idadi ya Wajumbe saba watakaokuwepo kwenye Baraza la Uwezeshaji la Taifa. Kamati imebaini kuwa, uteuzi huu unawalenga zaidi watumishi wa Serikali wenye ujuzi wa uzoefu katika masuala ya biashara, kilimo, viwanda na fedha. Kwa kuzingatia suala zima la uwezeshaji kiuchumi linakwenda pamoja na dhana nzima ya biashara huria, Kamati yangu inaishauri kuwa watakaoteuliwa wawe pamoja na Wajumbe kutoka nje ya Serikali. Kitendo ambacho kitaungana na ile dhana ya Serikali kujitaa katika mfumo wa soko huria.

Mheshimiwa Spika, ibara ya tisa ya Muswada inaweka muda wa miaka mitatu kwa Mjumbe wa Baraza kufanya kazi. Kamati ilitafakari kwa makini muda huo na kuona kuwa ni mfupi kwa chombo kizito kama hiki kumwezesha mjumbe kutekeleza wajibu wake ipasavyo, hivyo nashauri muda huo uongezwe na kuwa miaka mitano. Hata hivyo Serikali ilifanua kuwa kutokana na uzoefu uliopatikana, miaka mitatu ndio inafaa kwa kazi kama hizo, hivyo iliomba ubakie kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 14 ya Muswada inayoelezea kuwepo kwa nafasi ya Katibu Mtendaji atakayeteuliwa na Rais. Kamati inaona kuwa kumpa Rais jukumu hili ni kuzidi kumuongezea mzigo. Pili endapo atateuliwa na Rais hataweza kuwajibika ipasavyo kwenye Baraza. Hivyo Kamati inashauri kuwa ama aajiriwe na Baraza na kuwajibika huko moja kwa moja au apendekezwe na Baraza na jina lake lipelekwe kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliangalia uhusishaji wa sera ya uwekezaji na huduma ambazo hutolewa na Benki zetu hapa nchini. Kamati imebaini kuwa masharti mengi ya mikopo yaliyopo katika Benki nyingi yanakuwa ni kikwazo kwa shughuli za uwezeshaji na hata zile chache za makabwela zilizopo zinatarajiwaa kubinafsishwa.

Kamati inashauri kuwa Baraza liweke utaratibu unaoeleweca na kuondokana na vikwazo hivyo ili kupata fedha za kuwasaidia wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 33 ibara mpya 29 kifungu kidogo cha tatu, kama ilivyosomeka kwenye jedwali la marekebisho iliyowasilishwa kwenye Kamati. Kamati yangu inashauri kuwa Serikali iangalie madaraka iliyopewa Baraza ya kudhibiti Taasisi au asasi zinazoshughulika na masuala ya kiuchumi ambazo zipo chini yake.

Kamati inapenda kueleza wasiwasi wake kuwa masharti iliyowekewa taasisi au asasi zitakazoshindwa kutimiza hadi kufikia hatua hata kufutiwa usajili na kutopewa fedha, ni magumu mno ambayo yanapingana na lengo zima la Sheria hii la kumwezesha mwananchi. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali iangalie upya ndani ya usimamizi yaani *supervision* inavyojitokeza katika Muswada huu, ikiwezekana iondolewe na badala yake ijitekeze sana zana ya uvezeshaji yaani *facilitation*.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 35 kifungu kidogo cha kwanza A ya Muswada, ibara mpya ya 31 kifungu kidogo cha kwanza A kama ilivyo kwenye jedwali la marekebisho ilijoletwa kwenye Kamati. Maneno jukumu la Taasisi au asasi kutayarisha taarifa yake ya utendaji kazi ya shughuli na mipango ya kiuchumi hayako wazi. Kamati inashauri kuwa kifungu hiki kiangaliwe upya ili jukumu hili liwekwe bayana.

Mheshimiwa Spika, haya ndio maeneo ambayo Kamati iliyatolea ushauri. Yapo maeneo mengine ya kisheria yaliyofikishwa kwenye Kamati yangu na mdau ambaye Kamati ilielekeza Serikali iyafanyie kazi na bila ajizi yalipokelewa na Serikali na kuahidiwa kufanyiwa kazi.

Aidha, Kamati imefarijika sana kupokea taarifa kutoka kwa Serikali kuwa ingawa Muswada huu ni mfupi, lakini mambo mengi yatafanuliwa kwenye kanuni zitakazo andaliwa na Waziri Mkuu kwa mujibu wa Muswada huu na hivyo kutatua baadhi ya wasiwasi ulioelezwa na Kamati na Serikali iliahidi kuwasilisha rasimu ya kanuni hizo kwenye Kamati yangu, kuzihakiki kabla hazijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa yale ambayo sikuyagusia, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu watapata fursa ya kuyazungumzia watakapopewa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi adimu. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na timu yake ya wataalam kwa maelezo ya kina na ya ufasaha mbele ya Kamati yaliyowezesha Kamati yangu kutoa michango ya kina.

Aidha, namshukuru mdau, Bwana Clariance Kipobota kutoka kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kwa mchango wake, ulisaidia pia Kamati. Napenda nichukue nafasi hii pia nimshukuru Mkurugenzi wa kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Bibi Hellen

Kijo Bisimba, kwa kuitikia wito wa Kamati hii kila mara tunapohitaji mchango wa wadau.

Mwisho naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kutoa michango yao ya kina, iliyoboresha Muswada huu kufikia hatua inayoonekana na naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa *Chief Abdallah Fundikira*, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Ramadhani hashim Khalfan, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Dr. William Slaa na Mheshimiwa Nimrod Mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru pia Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kuihudumia vizuri Kamati. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati wa hii Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Charles Mloka, kwa huduma zao kwa Kamati na kuandaa maoni haya kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa mwaka 2004 (*The National Economic Empowerment, Bill 2004*).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu. Lakini hata hivyo Kambi ya Upinzani pamoja na kusikia taarifa ya Kamati kwamba kutokana na ufanuzi wa Serikali kwamba kuna utata, lakini bado inauona Muswada huu kama vile unaelea hewani bila kujulikana mwenyewe ni nani na hivyo kututia mashaka juu ya kuwepo dhamira ya kweli ya kutekelezeka kwake au huenda unatungwa Muswada kwa makusudi ya kukidhi kwa haraka mahitaji ya kundi fulani la watu jambo ambalo halitawasaidia Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaamini kwamba suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi ni suala linalolenga kuwaondolea wananchi umaskini. Sera ya uwezeshaji na Sera ya kuondoa umaskini lazima viende sambamba. Hivi sasa Ofisi iliyopewa dhamana ya kushughulikia umaskini ni Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo imepewa Mawaziri kamili

wawili. Inakuaje suala hili linaloletwa katika Muswada linawekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida hivi sasa kila jambo lenye mshindo mkali na mguso, kukimbiziwa kwenye kapu moja la Ofisi ya Waziri Mkuu. Kambi ya Upinzani pamoja na kuelewa kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndicho kiungo cha shughuli zote za Kiserikali, lakini ni vyema pia kukawepo mgawanyo wa kazi katika Wizara na Idara mbalimbali za Serikali kama tunataka utendaji wenyewe tija.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na jukumu kubwa la kuratibu shughuli zote za Kiserikali ambazo kimsingi ni nyingi. Pia imebebeshwa mzigo wa kuangalia mambo ya UKIMWI, mambo ya habari, Vyama vya Siasa, maafa, shughuli za Bunge, pesa maalum za uimarishaji kilimo na shughuli nyingine nyingi ambazo kwa hali halisi ya namna mambo yanavyokwenda bado zinahitaji msukumo zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata ukisoma kwenye kifungu cha tatu cha Muswada, kinachozungumzia tafsiri ya maneno yaliyotumika kwenye tafsiri ya neno *Minister*, inaeleza kwamba: “*means the Minister charged with the coordination of the economic activities for the purposes of economic empowerment.*” Tunapenda kuelezwa iwapo kimajukumu Waziri Mkuu ameshapewa dhamana hii au atateuliwa Waziri wa kushughulikia mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ufanuzi, sehemu ya kwanza katika kifungu cha pili kinachozungumzia *application*, kwamba Sheria hii itatumika na kufanya kazi upande wa Tanzania Bara. Pamoja na *amendments* ambazo zimewasilishwa hapa mezani leo asubuhi na ambayo ilikuwa ina *contradict* na kifungu cha nne, kinachozungumzia Baraza kufanya shughuli ya kuorodhesha hisa za Makampuni katika soko la hisa ndani ya Jamhuri ya Muungano.

Lakini Kambi ya Upinzani bado inalionjambo hili la kuwawezesha wananchi ni jambo linalowahu na kuwagusa wananchi wote wa Tanzania Bara na Visiwani. Mikakati inapaswa iwe ya pamoja na ndio maana tukaona ni vyema shughuli hii iwekwe chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Muswada huu wa kuanzisha chombo cha kuratibu, kusimamia na kuendesha shughuli zote za uwezesajili wananchi umeletwa wakati tumeshauza na kubinafsisha karibu kila kitu cha maana kwa wageni. Kwa jinsi hali ilivyo, Watanzania watawezesha kumiliki uchumi wa mambo ambayo ni madogo madogo na ambayo ni tegemezi kwa wawekezaji wakubwa ambao ni wageni.

Kwa namna moja au nyingine uchumi watakaoumiliki ni wa kuendelea kuwa watumwa na vibarua wa wawekezaji wakubwa wa nje ambao tayari wameshatengenezewa mazingira mazuri ya kuwekeza mitaji yao na kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, ni vyema wakati mwininge kweli Serikali ya CCM ni wajuzi wa kuandika mambo mazuri na matamu, lakini bila ya mikakati sahihi ya kuyatekeleza

hayo mambo. Ukipitia maandishi ya mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, ya uwezesaji wa kiuchumi wa Wananchi ukurasa wa 34 ibara ya 51 inasema hivi: "Katika kutekeleza sera hii, imebainika kuwa kuna ugumu wa kuifanikisha kutokana na ukweli kwamba Watanzania, Waafrika huko nyuma hawakupewa nafasi ya kushiriki katika uchumi wa kisasa wa kilimo, viwanda na biashara ndani na nje.

Kwa vile Waafrika waliachwa kwenye sekta ya uchumi wa jadi wa kilimo, ufugaji na uvuvi na kuwa vibarua na soko la sekta ya kisasa hadi leo wanaendelea kuwa pembezoni mwa sekta ya kisasa ya uchumi wa nchi yetu. Kwa ujumla hawana uwezo wa kumiliki na kuendesha uchumi huo, wala mitaji na uzoefu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio matamshi mazuri na yenye kuelekea kuwa na harufu ya kuwajali na kuwakumbuka Watanzania wasio na uwezo. Lakini ni hapo nyuma mmojawapo wa wana-CCM, alipozungumza juu usawa ambao ndio huo huo wa Afrika unaotajwa kwenye mwelekeo wa Sera hiyo, alipigwa kelele kwamba ni ubaguzi wa rangi. Lakini tukubali ukweli bila kipingamizi, kwamba Watanzania, Waafrika walio wengi ndio tabaka kubwa linaloongoza kwa umaskini. Kama tunataka kufaulu katika kuwawezesha kiuchumi watu wetu lazima tuwe wazi kama Afrika ya Kusini amba baada ya kutokomeza ubaguzi wa rangi, hawakuona haya walipoamua kujitoa na sera ya uwekezaji wa watu weusi.

Taasisi za Mabenki na za kifedha kwa kushirikiana na Serikali ya ANC zimeweka malengo ya kuwawezesha Waafrika kufikia mwaka 2010, wawe wanamiliki asilimia 25 katika nyanja za uchumi. Makampuni yameelekezwa na kukubaliana kwamba, kufikia mwaka 2008, asilimia 23 ya Wakurugenzi Watendaji wa Makampuni watakuwa Waafrika na katika hiyo asilimia, asilimia nne lazima wawe wanawake weusi.

Hivyo hivyo kwa nafasi zote hadi za chini kumewekwa malengo na mambo mahususi ya kufikiwa na sio sheria zenyelugha za jumla jumla na imeelezwa bayana kwamba Makampuni yatakayokwepa kutimiza malengo hayo yataadhibiwa kwa kunyimwa biashara ndani ya *tender* za Serikali, mikopo, mikataba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatujui kanuni zitakazotungwa na Waziri katika kuitekeleza Sheria hii zitakuwa na mwelekeo gani, lakini ni wazi bila mambo hayo kuwekwa wazi ndani ya Sheria kuna kukwama huko mbele na tusilipate lile tulilolikusudia.

Mheshimiwa Spika, ukichunguza vizuri Muswada huu ulioletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, utaona kwamba unalenga zaidi katika kuwapa Watanzania mikopo na nyenzo nyingine za kushiriki katika uchumi. Kambi ya Upinzani haiamini kwamba kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kuwapa mikopo na mitaji tu. Watanzania wanapaswa pia kutayarishiwa na kutengenezewa mazingira yatakayo wawezesha kuukamata na kuendesha uchumi. (*Makofi*)

(i) Lazima Sheria na mipango tunayopanga iwe ya uhakika na isiyo na hila wala mizengwe.

(ii) Lazima tuangalie wapi tumetoka, wapi tuko na wapi tunaeleke. Bila hivyo kuna maeneo ya nchi yetu yatatelekezwa. (*Kicheko*)

(iii) Lazima tuangalie kwa makini madhumuni tuliyoyakusudia na mbinu za namna ya kuyatekeleza ndani ya mazingira tuliyomo na yanayotuzunguka.

(iv) Tuangalie na kupanga vizuri raslimali na fedha tulizonazo, tujue tunaanza na lipi katika mipango yetu na tunaishia na lipi? (*Makofi*)

(v) Lazima Sheria hii tuijengee mazingira mazuri ya Utawala Bora, Demokrasia ya kweli na upambanaji wa kweli wa vitendo vya rushwa na ufisadi vilivyopo hivi sasa. Vinginevyo mpango mzima utatekwa nyara na kuwafaidisha wenyewe uwezo wa kimaamuzi au ushawishi ndani ya vyombo vya maamuzi.

(vi) Elimu kwa wananchi wetu na upashwaji habari, ni jambo la msingi ili angalau wananchi wapate uelewa wa jumla wa namna mambo yanavyokwenda katika dunia ya utandawazi.

(vii) Watanzania wengi waliokuwa na moyo wa kuwekeza na ustadi na kuwa na ustadi wa kufanya biashara miaka ya huko nyuma, walikatishwa tamaa na programu za Azimio la Arusha, Vijiji vya Ujamaa, Uhujumu Uchumi na kadhalika ambapo wengi walipoteza mali zao na wengine hata uhai wao. Wengi wanaiona Serikali ya CCM na Sheria zake havitabiriki, vinabadilika wakati wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili tuwarudishie Watanzania hawa moyo wa imani kwa Serikali yao, ni vyema wote waliodhulumiwa mali zao zilizopatikana kwa jasho lao na juhudhi zao, warejeshewe au kufidiwa na kitakuwa kianzio kizuri cha kuwawezesha. Wapo baadhi hapo nyuma waliofidiwa lakin zoezi lenyewe liliendeshwa kiubinasi, kwa upendeleo na kwa usiri mkubwa kisha likasitishwa. Bila ya kuyaangalia mambo hayo Muswada huu unaelekea kutuanzishia Baraza la kuwawezesha wale wenyewe nacho ili waongozewe zaidi na wale wasio nacho hata kile kidogo walichonacho wanyang'anywe wapewe walicho nacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Baraza linapaswa kuangalia yale masalia yaliyobaki hasa Mashirika yanayouzwa au yanayofungwa kwa *voluntary liquidation* wafanyakazi wawezeshwe namna ya kuyanunua au kupewa uwezo wa kuanza maisha. Wakulima ambao ndio asilimia kubwa nchi hii, lazima wapewe ruzuku kwa mazao wanayoyazalisha ili bei zifikie gharama halisi za uzalishaji. Hii itawaongezea uwezo wa kimapato na uchumi wa soko na hasa hile *purchasing power* yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine tunaloliona ndani ya Muswada huu, ni mwendelezo wa mambo chungu mzima ambayo hubuniwa na kuanzishwa na Serikali bila kuanza kufanya utafiti ulio makini. Matokeo yake huwa ni uanzishaji Sheria na mipango mipyka kila kukicha inayosemekana inalenga katika kuwaondolea au kuwapunguzia

Watanzania umaskini au lugha mpya ya Muswada huu kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mipango ya awali hatuelewi inakuwa imeishia wapi au imekwama wapi? Na kwa kuwa Tanzania ni watu tuliobatizwa katika utatu wa utulivu, amani na umoja wa Kitaifa, huwa tunakubali na kupita bila kuulizana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa enzi hizo tumekwenda tunazipiga nakshi ili ziwe chachu ya kuwaletea Watanzania maendeleo ya kweli, tunaomba Serikali kama inataka kufanikiwa katika Muswada huu itufafanuliwe kwanza, wakati unapoingia kwenye enzi mpya za kuanza kuwezeshana kupitia hilo Baraza.

Je, mipango ya mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana kwa kila Halmashauri. Suala la *Privatization Trust Fund*, Benki ya kuwakopesha makabwela NMB, mfuko wa pembejeo, mpango wa *Import Support*, mfuko wa kuwakopesha wanafunzi na kadhalika vinaendeleaje au vimefia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, walioifanya mipango hiyo ikwame au ichelewe wanasemaje au wamechukua hatua gani? Kwa nini mipango mingi haianzi Au haifanyikazi vizuri kutokana na usimamizi?

Mheshimiwa Spika, tunavyofikiri Kambi ya Upinzani mipango mingi haianzi au imekufa au haifanyi kazi vizuri kutokana na usimamizi mbovu, ubinafsi, ubadhirifu au kukurupuka katika kuianzisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka sheria hii ifanye kazi vizuri lazima pia tuangalie sheria zingine zilizopo ili ziende sambamba na lengo zima la uwezeshaji kiuchumi wananchi, sheria hii pekee haiwezi kujisimamia yenyewe, mfano sheria ya mifuko ya akiba ya wafanyakazi, sheria za kibenki, sheria ya uwekezaji ambapo wawekezaji wageni hupewa *Tax Exemption* na *Tax Holiday*, Sheria ya Ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, dalili za mvua ni mawingu, kwa vile Muswada huu hauonyeshi bayana namna utakavyokita mizizi yake hadi kwa mkulima na mwananchi wa kawaida wa huko Kakongwe, Kigoma, Kambi ya Upinzani bado inahisi kwamba chombo hiki kinachoanzishwa chini ya Muswada huu ni cha kuwasaidia wakubwa na ni njia ya kutaka kuwawezesha wachache kujichotea mamilioni ya pesa toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ni Mtanzania gani wa kawaida atakayekuwa na uwezo wa kulifuata Baraza mjini Dar es Salaam ili limwezeshe na hasa tukizingatia ukweli kwamba Baraza litakuwa na mtandao wa utendaji kazi zake nje ya pale linapokutania.

Mheshimiwa Spika, ni wazi wakati wakubwa wachache watakapokuwa wakiendelea kufaidika na kula vizuri kutokana na Muswada huu, Watanzania walio wengi amba ni wa hali ya chini watakuwa wakiishia kunawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

SPIKA: Msemaji wa kwanza katika mjadala wa jumla atakuwa Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ismail Ivvatta jiandae vilevile na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, jiandae.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuanza mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tatizo la nchi hii, lazima tuelewane kwanza tumekwisha wafanya Watanzania wote wakawa sugu ya kuwa wao ni maskini, hii *terminology* ya umaskini imewaingia Watanzania na kila unayemkuta anasema yeze ni maskini, tumeunda mpaka Wizara ya Kuondoa Umaskini lakini umaskini unaendelea na watu wamekwisha kuwa masikio yao wanajua ni umaskini tu.

Mheshimiwa Spika, hatujaunda Wizara ya kuleta utajiri, ingekuwepo Wizara moja ya kuleta utajiri sambamba na umaskini, kuna watu wengine ukiwaambia ni maskini watacupiga, mmasai ukimwambia ni maskini na ana ng'ombe zake atakupiga, kuna makabila ya namna ile lakini sasa kuna makabila mengine wanapenda kuitwa maskini.

Mheshimiwa Spika, nchi imeendelea kuwa maskini kwa sababu tunajiita maskini, hatutaki kujiita sisi ni matajiri, tuna utajiri wa maliasili, tuna utajiri wa watu, tuna utajiri wa kila kitu lakini tunajiita maskini, jamani hili neno la maskini kwa nini tusilionde katika msamiati wetu? *Psychologically* watu wamekwishajifanya ni maskini hata tungepitisha sheria elfu moja wakati watu wanajidai ni maskini, wataendelea kujiita ni maskini tu.

Lakini njia mojawapo ya kufanya watu wabadilishe zile fikra ni lazima tujaribu kutafuta njia kuwaambia wao ni matajiri na wawe matajiri katika nchi yao yaani tunajiletea umaskini wa kujitakia, nitakupeni mfano mdogo tu, hizi simu za mikononi, zimesambaa Tanzania kuna zaidi ya simu za mikononi milioni mbili tuseme iwe *very conservative* wakitumia watumiaji milioni moja ni dola milioni moja zinasafishwa kutoka kwa wananchi *everyday* na hizi pesa zinatoka nje hazirudi, watu maskini tunazidi kuwafanya wawe maskini wa kutupwa, utamkuta mtu hana hata mshahara ana *ki-mobile phone* chake hafanyii biashara, lakini anadiriki kukosa chakula lakini apige simu atupe dola moja.

Mheshimiwa Spika, tunajenga bomba la kubeba pesa zote katika nchi hii, tunajenga bomba ambalo linanyonya, linatuletea umaskini halafu tunakuja kusema tunataka ku-*empower* Watanzania ili waweze kuingia katika biashara.

Mimi nikiwa Bungeni hapa Waziri wa Fedha aliwahi kusema tuna pesa nyingi sana Benki, hakuna watu wa kukopa na ziko nyingi, nani aende akakope *in the first place* hata kukopa nako ni tatizo, kukopa unakopa pesa unalipa *interest* ambayo huwezi kufanya biashara ya kulipa zile pesa, unazidi kumfanya yule aliyekopa awe maskini na

hii inaweza kufika mahali vile vile hata hawa watakaokwenda kuchukua mikopo kwenye hii tunaizungumzia watachukua pesa, watakuwa maskini zaidi kwa sababu hata walicho nacho watakiweka dhamana na wao watakuwa maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, tunaposema tunataka ku-*empower* Watanzania tufikirie mazingira ya nchi yetu kwa ujumla siyo kukopa pesa tu ndiyo kunamfanya mtu tajiri, kuna njia nyingi za kufanya mtu awe tajiri na kwanza ni ile ari ya mtu mwenyewe kutoka moyoni mwake itoke moyoni mwake yeye siyo maskini akatae maana yake inakera kuitwa maskini mpaka nchi nzima inaitwa maskini.

Mimi nilikuwa nasoma gazeti jana sijui juzi, kuna wahindi wanataka kuja kuwekeza kilimo katika Tanzania kwa kuwa hatujui kulima, ni aibu wanataka kuhama kwao kwa sababu hawana mvua, nchi imekuwa *desert*, wanataka kuja kwa elfu ili waje hapa waje wakawekeze katika kilimo.

Tumekuwa tukipiga kelele hapa tangu zamani tangu Bunge hili limeanza jamani tukitaka kujikomboa katika umaskini tuwekeze katika elimu, *number one* tuwekeze katika kilimo. Hivi vitu viwili ni *very vital* ni vitu vya msingi ambavyo kwa kweli vitamwondolea Mtanzania wa kawaida umaskini kwa sababu tusisahau hili tunalizungumza hapa ni umaskini, namna ya kumwondolea Mtanzania umaskini.

Mashirika ya kutoa fedha hapa Tanzania tunayo mangapi? Tuna NSSF, tuna National *Micro Finance Institution* nyingi tu na Serikali inakubali pesa zipo nyingi za kukopa lakini nani Mtanzania anaweza kwenda Benki, hata mimi nikienda benki wananyima pesa. Nani mtu wa kawaida ambaye anaweza kwenda benki akapata pesa, hata hii *bill* tunayoizungumzia kweli hebu tujaribu kugeuza mawazo yetu tufikirie namna ya kumfanya Mtanzania awe *comfortable* katika nchi yake, siyo lazima awe ni mtu tajiri sana lakini awe *comfortable* apate milo miwili aweze kushiba alale. Ndiyo utajiri tunaoutafuta huo, siyo kwenda kukopa mapesa mtu apate mlo wa kutosha apate nyumba ya kulala apate na nguo za kuva.

Mheshimiwa Spika, hebu tufikirie ni mazingira gani ambayo tutayafanya Mtanzania afikie namna ile siyo kuendeleza watu kwa kusema ni kukopa kukopa, kukopa ni umaskini, tutakopa halafu mwisho wake tutakuja kuomba tusamehewe vilevile na tutaua vile vyanzo, maana yake nchi yetu imekopa na tunasamehewa na hao wanaokopa mabenki watafika mahali na wao wasamehewe. Tunalionia hilo lakini?

Mheshimiwa Spika, mimi nalizungumza kwa sababu nakaa kijijini kule naona maisha ya Watanzania yalivyo na hali inazidi kuwa ngumu, hali inazidi kuwa ngumu na Serikali haiwezi kujenga matajiri ili kuondoa maskini, Serikali haiwezi. Haiwezi kabisa hata ikikopesha, mtu kama hajui kujiondolea umaskini hata ukimpa pesa atazitupatupa zitakwisha, lete mabilioni katika nchi hii wagawie Watanzania baada ya mwezi mmoja zote zitakwisha zile pesa, zitakwisha zote lazima awe na ile *idea* ya namna ya kuzitumia zile pesa ziongezeke. Kama hana hiyo ni kazi bure hata haya tunayazungumza yatabakia katika mafaili na hayatamsaidia Mtanzania na tutabakia tukisema zimebaki kule kama hayo Mashirika mengine au pesa zitakuwepo lakini hazitatumika kwa mtu mwingine

yeote labda kwa hao wengine ambao labda watakaofaidi kwa kupata mishahara. Siwezi kusema zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu sasa, najua utawasaidia sana Watanzania ambao sasa hivi wana ari ya kujiendeza na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, ila kwanza ningeomba Mheshimwa Waziri anapohitimsha hoja yake atueleze sisi Watanzania huu mfuko utakuwa wa namna gani, je, utakuwa kwenye mfumo wa kibenki, kwa sababu ukishaingia kwenye mfumo wa kibenki kwa kweli wale wanyonge wa vijijini wataendelea kupata taabu ya kupata hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba Waziri atuambie huu mkopo unahu su kuwakopesha makundi gani, kwa sababu sasa hivi kuna makundi ambayo yana uwezo wa kukopa kutoka kwenye mabenki makubwa.

Mimi nafikiri huu mfuko ungelenga kuwakopesha wafanyabiashara au wakulima wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kwenda kwenye mabenki makubwa kwa sababu hawana majumba makubwa, hawana vitu vya kuweka kama dhamana. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Serikali huu mfuko ulenge kwa wale Watanzania wenyе kipato kidogo ambao watakopa walime, wafanye biashara zao na warudishe bila matatizo, lakini ukishawachanganya na wafanyabiashara wakubwa tayari wale Watanzania wenyе kipato cha wastani na cha chini watakosa mikopo hii.

Halafu ningeomba Waziri atufafanulie huu mfuko utakuwa na Wajumbe tisa, utaeneaje mikoani na tuna imani kabisa hao Wajumbe watakuwa Dar es Salaam, wale wananchi wa Iramba Mashariki, wale wananchi wa Kagera, wale wananchi wa Lindi na Babati watafaidika vipi?

Kwa hiyo, sisi tungeomba kuwe na mtando, kwanza mimi nisifie kwa sababu uko ofisini kwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ana mtando mpana sana, mtando unafika mpaka vijijini. Kwa hiyo, mimi ningeshauri waangalie jinsi ya kuwashudumia watu walioko kule chini.

Mheshimiwa Spika, pia ningewomba Mheshimwa Waziri atuambie amesema kwamba hizi pesa zinapitishwa na Bunge, basi itajwe ni asilimia ngapi ya Pato la Taifa litawekwa ndani ya mfuko huu ili watu tuwe tunajua kabisa isiwe mambo ya kufichaficha.

Mheshimiwa Spika, imeanzishwa mifuko mingi hapa kwetu, kama mfuko wa pembejeo, mfuko wa *Import Support* hii mifuko ilianzishwa kwa nia njema na ilikuwa inafanya kazi vizuri sana kule nyuma lakini sasa hivi baada ya kuwekwa chini ya mabenki Watanzania wanyonge wameanza kupata taabu tena ya kupata hii mikopo. Sisi

tunashauri huu mfuko usigeuzwe tena kwenda kushirikisha na benki tena benki ambazo wana-*charge* riba kubwa.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu nina imani utawakomboa wananchi, sasa hivi mabenki karibu yote yaliyokuwa yanatoa mikopo kwa wakulima yamejitoa, sasa hivi imebaki *CRDB* tu ambayo mtaji wake siyo mkubwa wa kutosheleza wakulima wote na vyama vyetu nya ushirika. Sasa mimi ningeomba huu mfuko usaidie sana katika kuleta maendeleo kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu umeanzishwa wa kutekeleza mikakati sahihi ya Chama cha Mapinduzi ya kuwakomboa Watanzania wanyonge, mimi ningeomba sisi kama wawakilishi wa wananchi wetu tusiwe tunabadilisha badilisha maneno, pale mahali ambapo Serikali inafanya vizuri ni lazima tuipongeze. (*Makofii*)

Kwa kuanzisha mfuko huu kwa kweli wananchi wa Tanzania wanyonge watafaidika sana, mimi nisingependa kumaliza muda mrefu, nilikuwa nataka tu Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha Muswada huu anijibu niliyoyauliza. Nakushukuru sana, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ISMAIL J. R. IVWATTA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja huu Muswada ili sheria iweze kuanzishwa na wananchi waweze kunufaika na kuanzishwa kwa hii sheria.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa hii sheria pamoja na Watanzania wengi watafaidika na kuanzishwa kwa hii sheria, lakini nilikuwa naomba tu ielevete kwamba katika kuanzisha hii sheria Watanzania walio wengi ambaao ni 80% ni wanakijiji ambaao ni wakulima wapo vijijini.

Sasa nilikuwa naomba kwamba katika kutekeleza hii sheria basi hao watu wakulima ambaao ni wanavijiji wajaribu kuangaliwa vizuri na hii sheria na kwa sababu hawa wanaoishi vijijini ni wakulima na shughuli yao kubwa ya kiuchumi ni kilimo nilikuwa naomba watazamwe kufuatana na mazingira yao ambayo ni ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wa vijijini ni wakulima walio wengi wanaendesha kilimo bila utaalam, sasa ili waweze kufanikiwa katika uwekezaji wao katika kilimo kama ndiyo shughuli yao ya kiuchumi, nilikuwa naomba suala la kuwawezesha hawa wakulima kupata maafisa kilimo au wataalamu wa ugani liangaliwe vizuri ili waweze kufanya shughuli yao ya kilimo kiuchumi hii ikiwa ni pamoja na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ukiwaliza kama wana wataalam vijijini watakwambia kweli

wanao, lakini sina uhakika na sijaona mahali popote takwimu zinazoonyesha kwamba Afisa Ugani mmoja kwa upande wa kilimo au mifugo anatakiwa ahudumie wakulima wangapi. Kwa hiyo, napata wasiwasi kwamba inawezekana katika maeneo mengine wakulima wanakuwa wengi lakini Maafisa Ugani wanakuwa wachache, kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo litazamwe.

Lakini pamoja na kuangalia idadi ya Maafisa Ugani huko vijijini, suala la kuwawezesha hawa Maafisa Ugani vilevile liangaliwe, maafisa wengi wanalazimika kuhudumia vijiji vingi hasa ukizingatia kwamba kuna kipindi hawa maafisa walipunguzwa huko vijijini. Kwa hiyo, wanalazimaka kuhudumia vijiji vingi, lakini wanaposafiri kwenda kufanya kazi katika maeneo mengine huwa hawawezeshwi kujikimu wanapokuwa katika vijiji ambavyo ni nje ya vituo vyao nya kazi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hilo liangaliwe lakini vilevile wanaposafiri wakati mwengine wanakuwa hawana vifaa nya kuwawezesha kufika katika maeneo wanayotakiwa kufanya kazi, kwa hiyo, suala la vyombo nya usafiri nilikuwa naomba nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine sambamba na hilo ni kwamba suala la barabara huko vijijini kwa ajili ya wakulima waweze kupeleka pembejeo zao kwa urahisi na kubeba mazao yao kwa urahisi nalo nilikuwa naomba liangaliwe.

Halafu suala lingine ni kwamba katika suala la upatikanaji wa pembejeo sasa hivi hizi pembejeo za kilimo ama za mifugo zinauzwa katika utaratibu wa soko huria ni kwamba wanaofanya biashara ya hizi bidhaa ni watu binafsi na hawa watu binafsi mara nyingi wanapenda kuendesha shughuli zao mahali ambapo gharama za usambazaji ama gharama za uuzaji hazitakuwa kubwa sana kwa hiyo, mara nyingi wanakuwa wapo katika maeneo ya mijini, miji ya Mikoa ama miji ya Wilaya.

Kwa hiyo, kwa huko vijijini ambako hawa wanavijiji wanakuwa hawawezi kupata hizi huduma vizuri nilikuwa nashauri kwamba na wao katika kuwawezesha basi wasaidiwe kuanzisha vyama nya ushirika vitakavyowawezesha kupata hizi pembejeo kwa bei nafuu.

Katika huu Muswada pia suala la kutoa wito kwa wananchi kuanzisha utamaduni wa kujiwekea akiba kwa ajili ya kuweka akiba limetiliwa mkazo, lakini huwezi ukawa na utamaduni wa kujiwekea akiba kama utakuwa huna vyombo nya fedha. Mabenki mengi tunayakuta yako mijini huko vijijini hakuna, utakapomwambia huyu mwananchi ajenge utamaduni wa kujiwekea akiba ataziweka wapi, aziweke chini ya godoro ama chini ya mto kesho aingiliwe na majambazi.

Sasa ili kujenga huo utamaduni, nilikuwa naomba basi na vyombo vinavyojishughulisha na utunzaji wa fedha na utoaji wa huduma za fedha uweze ukatolewa kwa hivi vyombo waweze kupeleka mpaka katika vijiji au katika maeneo ambako wananchi wengi wa vijijini wanaweza wakafaidika na kuanzisha huu utamaduni wa kujiwekea akiba.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuwawezesha wananchi kuanzisha shughuli zao za kiuchumi na za kibiashara, suala la utoaji na upatikanaji wa taarifa pia limetolewa wito kwamba kutakuwa na utaratibu wa kuwapatia taarifa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuko katika wakati wa teknolojia ya mawasiliano wakati wa kufanya mawasiliano ya kutumia sanduku la posta kwa kweli unaonekana kupitwa na wakati, sasa hivi mawasiliano ya kutumia *internet* na utumiaji wa vyombo kama vya *computer* unaonekana kuanza kuenea zaidi duniani.

Sasa nilikuwa naomba kwamba katika suala hili la kuwawezesha wananchi basi vyombo vya mawasiliano ya *internet* na vile vile hata na mafunzo ya *computer* badala ya kuwa yanafanyika katika miji mikubwa basi yazidi kuendelezwa kupelekwa katika ngazi za Wilaya na ikiwezekana hata katika ngazi za tarafa ili hawa wananchi waweze kuwa wanapata hizi taarifa ambazo zitawasaidia katika shughuli zao za kiuchumi na biashara.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia katika kazi za Baraza la uwezeshaji kuna mahali wanazungumzia katika suala kutoa mikopo wanasema pale katika kifungu cha 5(2)(o), wanasema Baraza litaangalia je, katika kutoa mikopo je, hapa wanaweza wakaangalia watoe masharti ama mahali pengine wasitoe masharti.

Mimi nilikuwa naomba kusiwe na suala la kuangalia kwamba hapa mtu ana uhuru wa kuweka masharti ama ya kutokuweka masharti, mimi nafikiri mikopo yote inapotolewa ni vizuri ikawa na masharti ili kuhakikisha kwamba yule anayechukua mkopo anarudisha huo mkopo.

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mizuri sana kwamba katika sehemu zetu nyingi za kazi tumeanzisha vyama vya Akiba na Mikopo ambazo ni *SACCOS* na zimefanya kazi nzuri sana katika nchi hii na hivi sasa kazi nzuri iliyofanywa na hizi *SACCOS* ndiyo inatupelekeea kuhimiza na wakulima vijijini waanzishe lakini hizi *SACCOS* pamoa na kufanya kazi nzuri wanachama wake wamekuwa na wao wanapata hiyo mikopo kwa masharti na masharti wanayotoa ni kwamba kwanza yule mfanyakazi ambaye ni mwanachama anakuwa na dhamana, dhamana moja ni mshahara wake kwamba atakaposhindwa kulipa mshahara wake utakatwa kufidia deni ambalo ameshindwa kulipa lakini sharti la pili ni kwamba amana ama mafungu yake aliyonayo katika chama na yenyeewe yanachukuliwa kama ni dhamana kwamba atakaposhindwa basi yale mafungu yake yafidie kulipa ule mkopo.

Kwa hiyo na hii mikopo ambayo itakuwa inatolewa hapa nilikuwa naomba vile vile lazima iwe na masharti tusije tukaanza kujenga dhana kwamba hii *National Economic Empowerment Fund* basi itakuwa kama ni chombo au itakuwa msalaba mwekundu basi mtu atakapokuwa amechukua huo mkopo hatarejesha. Nilikuwa naomba hilo tusije tukalijenga, kwa hiyo nilikuwa naomba hii mikopo itakayokuwa inatolewa basi ni vizuri ikarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nashauri kwamba huu mfuko au hii sheria tunaianzisha ya kuwawezesha hawa wananchi na hii mikopo ambayo watakuwa wanapewa mimi naona ni kama kitu ambacho tunatoa kama ni huduma ya mwanzo kwa wananchi wetu kwamba tunawajengea utamaduni kwamba waweze kufaidika, waweze kuwa wanachukua mikopo lakini baadaye tunatarajia hawa wananchi wakishakuwa na uwezo waweze kujitegemea wao wenyewe kwenda kuchukua mikopo katika vyombo vyaa kifedha kama mabenki na vyombo vingine na vilevile hatutarajii kwamba hawa watu waendelee kuwa wafanyabiashara wadogowadogo, tunatarajia wawe ni wafanyabiashara wakubwa baadaye ikiwezekana waweze kufanya hata biashara za kimataifa

Sasa ni vizuri tukawajengea utamaduni ambaa utawawezesha kukua na baadaye kuweza kujitegemea kwa hiyo, ni vizuri tukawajengea utamaduni wa kuweza kuwa wanafuata masharti na baadaye kuwa na taratibu nzuri za kuweza kufanya kazi.

Sasa tukirudi kwa upande wa wakulima, kwa sababu wakulima ni wengi na wamesambaa, nilikuwa nashauri kwamba kuna mazao kwa mfano zao la Tumbaku na mazao mengine wakulima wake huwa wana vyama vya ushirika kwa hiyo, mikopo yao mara nyingi na dhamana zao huwa zinaendeshwa kupitia vyama vyao vya ushirika. Sasa kwa wakulima ambaa mazao yao hayana vyama vya ushirika nilikuwa nashauri kwamba wakulima wa aina hiyo washauriwe waanzishe vyama vya ushirika na watakapoanzisha vyama vya ushirika basi hata mikopo yao ipitie katika hivyo vyama vyao na kama ni udhamini uweze kufanywa na hivyo vyama vyao vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu mdogo lakini naomba kurudia kusema kwamba naunga mkono sheria hii. Ahsante sana.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu wa uwezeshaji.

Mimi vile vile niipongeze Serikali kwa kuweza kuleta Muswada huu ambaa kwa kweli ni muhimu sana katika kuinua hali ya kiuchumi ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, suala hili tumelizungumzia mara nyingi sana kwamba ni namna gani tunaweza tukaweka sera na sheria za makusudi za kuwainua Watanzania ambaa uwezo wao wa kujikwamua kiuchumi ni mdogo, na mimi nafurahi kwamba kuna mambo kadha wa kadha ambayo yamechukuliwa na Serikali na mojawapo ikiwa ni kuleta sheria hii lakini vile vile mikakati mingi imewekezwa katika kuhakikisha Watanzania na wale wenye bahati ya kuwa na mali ambayo kwa sasa ni mali mfu, mali zile zinafanywa kuwa hai kwa maana ya kuweza kuwazalishia mali zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa labda niseme kwamba katika nchi yetu tumekuwa tukizungumza kwamba kuna tabaka la matajiri sana na tabaka la maskini sana, uzoefu unaonyesha duniani kote kwamba matajiri sana hawawezi kuwasaidia maskini sana.

Kwanza, ni kwa sababu matajiri sana mara nyingi ni wachache na maskini ni wengi mno. Hata kama wangependa kuwasaidia maskini sana haiwezekani. Sasa ili maskini sana waweze kusaidiwa kiuchumi kuna tabaka la katikati hapa ambalo hili ndilo tabaka pekee linaloweza kuwasaidia wayonge, unaweza kusema wayonge wenzao ambao kidogo wana uwezo hao wa kati. Sasa ni utajiri au uwezo wa hawa, hili tabaka la katikati ndilo tunalotakiwa tulikuze ili wawe na uwezo mkubwa zaidi kuliko hapo walipofikia na kwa sababu wao ni wengi kuliko matajiri sana basi wataweza ule utajiri wao mdogo kuupeleka hadi chini kwa wenzao ambao ni maskini sana.

Sasa mimi hii sheria ninavyoiona ni sheria ya kuwawezesha hawa walioko katikati wenye uwezo kiasi. Mtanzania ambaye yeye peke yake au kwenye vikundi au wakiwa wawili, watatu, wanne, watano wana uwezo angalau wa kuanzisha Kampuni au biashara na biashara kama hizi ni nyingi. Sasa ni biashara hizo au Makampuni hayo ndiyo tunataka kuona ni namna gani tunaweza tukayakuza yawe na uwezo mkubwa, yawewe kuajiri walioko wengi hawa maskini na vilevile kuhakikisha kwamba ule utajiri wao angalau unakwenda chini. Kwa hiyo, kwa kweli ni sheria ya kuwawezesha Watanzania wenye uwezo wa kati ili waweze kuwasaidia wale wa chini.

Mheshimiwa Spika, sasa tukishakubaliana hivyo sera hii ni nzuri, lakini naona kwamba hakuna utaratibu au hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba wenye uwezo mkubwa na wenyewe wanachangia kuwawezesha hao wa kati ili na wenyewe wainuke kiuchumi na uchumi wao uweze kwenda mpaka chini. Sasa vifungu ambavyo vinawalazimisha matajiri wakubwa zaidi sivioni.

Mimi naona huu Mfuko utakaonzishwa kwa namna ulivyo bila kuwa na mbinu na namna ya kuwalazimisha au kuwashurutisha hao matajiri wakubwa kusaidia tabaka hili la kati kuinua uchumi wao, kuinua Makampuni yao ili yaendelee yapanuke, sijaona.

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba lazima sheria iwe na makusudi kabisa ya kuwainua kiuchumi Watanzania ambao wana uwezo kidogo hao wa kati na kwa kufanya hivyo tufanyeje? Mimi nashauri tufanye kwa makusudi kabisa tuwalazimishe hao wenye uwezo mkubwa wachangie. Sasa wanachangiaje?

Kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza kwamba kwanza mchango wa Serikali, ile *grants* ambapo kutakuwa na mchango ambao tunauthibitisha hapa Bungeni uonyeshwe kwamba kutokana na pato la Serikali tutachangia nusu asilimia na mimi ningependekeza asilimia hiyo ionyeshwe waziwazi kama ambavyo tunasema Vyama vya Siasa tutachangia asilimia mbili hatujafika huko, lakini basi nusu ya asilimia ya Pato la Taifa ionyeshwe kwenye sheria kwamba litakwenda kwenye Mfuko huo. Hilo ni moja.

Lakini pili, Makampuni na Mashirika makubwa na yenyewe yalazimishwe kuchangia tuseme kwa Kiingereza *compulsory/contributions*. Sasa kwenye sheria unaona michango haikuonyeshwa au kwa Kiingereza *contributions* na mimi nasema neno hilo napendekeza liongezwe na likishaongezwa basi tuseme kwamba hii ni michango ya lazima ambayo ni hizo *compulsory contributions* zichangwe kwa namna fulani na mimi

napendekeza kwamba Makampuni yote makubwa ya nje yaliyosajiliwa Tanzania na yanafanya biashara Tanzania, lakini yanamilikiwa kwa asilimia 100 na watu wa nje, faida wanayopata hapa Tanzania asilimia tatu wachange kwenye Mfuko huo. (*Makofi*)

Lakini vile vile, Makampuni ya nje ambayo nusu yanamilikiwa na Watanzania na nusu watu wa nje, lakini watu wa nje wanayamiliki kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo, bado ni Makampuni ya nje pamoja na kwamba kuna Watanzania ndani, tunawapa unafuu kwa sababu kwanza kuna Watanzania ambao vile vile wanamiliki basi hawa faida wanayopata hapa Tanzania Makampuni yanayomilikiwa na Watanzania na watu wa nje asilimia mbili ya faida baada ya kodi wachangie kwenye Mfuko huu. (*Makofi*)

Lakini vile vile Makampuni ya Tanzania ambayo yanamilikiwa na Watanzania matajiri na hapa tuonyeshe utajiri huu kwamba wewe ni Mtanzania peke yako au peke yenu Watanzania mna Kampuni mnayofanya biashara nchini Tanzania na kwa mwaka mauzo yenu ambayo nasema ni *gross income*, mauzo yenu yanazidi bilioni moja kwa mwaka basi asilimia moja ya faida mchangie kwenye Mfuko huu. Tunasema nyie ni Watanzania, lakini ni matajiri kama mnawenza mkatengeneza bilioni moja kwa mwaka basi changieni ingawaje ni Watanzania. Lakini wengine wote ambao mauzo yao kwa mwaka ni chini ya bilioni moja na ni Watanzania tunasema hao ndiyo tunataka kuwajenga na kuwapanua na kwa hiyo, hawatakuwa na haja ya kuchangia kwenye Mfuko huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, mimi nashauri kwamba kuna Makandarasi na washauri na wauza bidhaa wa nchi za nje ambao hawakusajiliwa Tanzania, kwa hiyo, Makampuni yao hayako Tanzania, lakini kwa sababu tunatangaza Zabuni za Kimataifa wanaomba kazi ya Ukandarasi, za ushauri, za kuuza bidhaa nchini kwetu kwa kutumia fedha ama za wafadhili ama za Serikali kupitia Sheria ya Manunuzi hawa ambao Makampuni yao hayakuandikishwa Tanzania wachangie asilimia mbili ya bidhaa za Zabuni zao zile, thamani ya Zabuni asilimia 2 wachangie kwenye huu Mfuko. Kwa sababu ukisema anafanya kazi Tanzania atasema bwana mimi sifanyi Tanzania na sijasajiliwa Tanzania. Lakini amepata kazi Tanzania kwa kufuata Sheria ya Manunuzi basi asilimia mbili ya thamani ya Ukandarasi wako au uuzaji wa bidhaa au Ushauri changia kwenye Mfuko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani kwamba tukifanya hivi tunaweza tukaona kweli ule Mfuko unakua kwa kiasi kikubwa, na hata lile jukumu la kutoa mikopo na kutoa misaada kwa makampuni haya kutakuwa na uwezo mkubwa zaidi. Bila kufanya hivyo uwezo wa Mfuko huu utakuwa mdogo na watakoakuja kuomba misaada na mikopo, Makampuni hayo ya kati ambayo tunataka tuyaendeleze ili yawaendeleze na watu maskini watakuwa ni wengi mno na ule Mfuko utakuwa hautoshi. Lazima tufanye utaratibu wa makusudi kwa kuweka viwango hivi ili kwa kweli Mfuko huu ukue na uchangiwe siyo kwa hiari, lakini kwa kisheria kama ambavyo tutakuwa tumeainisha.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nadhani kwamba kuna haja ya kutaja kwa makusudi kabisa ndani ya Sheria pamoja na kwamba kwenye Sheria nimesoma imesema Sheria zingine lile Baraza litaangalia utekelezaji wa sheria zingine ili kuweza kwenda

sambamba na utekelezaji wa sheria hii. Lakini kuna haja ya kutaja ndani ya sheria kwa makusudi kabisa kwamba sheria ya Ununuzi ya mwaka 2001 na najua kabla ya Bunge hili labda tutakuwa na sheria mpya ya mwaka 2004 lakini tusizungumzie hilo. Tuzungumzie hiyo sheria iliyopo mpaka sasa ya mwaka 2001, kuna vipengele vinavyotoa upendeleo kwenye Makampuni au bidhaa zinazonunuliwa Tanzania au wale Makandarasi wa Kitanzania, itajwe kwenye sheria hii kwamba Baraza hili vilevile litaangalia na kusimamia utekelezaji wa vipengele hivyo vinavyotoa upendeleo katika manunuzi ndani ya Serikali ili kipengele hicho bila shaka labda kitaboreshwani kusaidia Watanzania wengi kupata kazi za Ukandarasi, za Ushauri na Uuzaji wa Bidhaa kwenye nchi yetu ili waweze kupanua biashara zao. Kwa sasa hivi Makampuni ya katika hapa Tanzania ni vigumu sana kupata tender au Zabuni ambayo inashindanishwa kwa Zabuni za Kimataifa kwa sababu hawana uwezo.

Sasa ule upendeleo ambao utawekwa na sheria ya Manunuzi usimamiwe na Baraza ili kuhakikisha kwamba Makampuni yetu angalau yanapata kazi. Sasa hivi Makandarasi wa barabara zetu zote na kazi zozote zenyetane zaidi ya milioni 100 au milioni 200 Makampuni ya Kitanzania haya ambayo tunataka tuyaboreshe ili tuweze kupanua kazi zao waweze angalau kuwa na uwezo wa kuajiri Watanzania zaidi na kutoa misaada kwa Watanzania walio wengi ili waweze kuinuka wanashindwa kupata hizi kazi kutokana na vifungu hivi vya kupendelea Watanzania au Makampuni ya Kitanzania kutokuweko na umakini.

Mheshimiwa Spika, mimi nimalizie kwa kusisitiza kwamba ni muhimu na nakubaliana na uanzishaji wa Baraza na nimefurahi kwamba wametoa ile Bodi iliyokuwepo mwanzoni kwa sababu tulikuwa tunashindwa kuelewa kwa nini kuna Baraza halafu kuna Bodi na sasa wameiondoa tunafurahia. Uanzishwaji na utekelezaji wa majukumu yake. Lakini suala la kuboresha Mfuko huu uwe ni mkubwa kweli kweli lazima viwango vya kuchangia vionyeshwe kwenye sheria kama kweli tunataka Mfuko ambao utakuwa ni mkubwa na utakaosaidia Watanzania kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata Kanuni namba 70(4) ilikuwa nilete mapendekezo hayo kimaandishi, lakini kutokana na utaratibu kutokamilika mapema. Hata hivyo, kabla mjadala haujaisha mapendekezo yangu hayo kwa kila kifungu yote niliyozungumza nitayawasilisha kama mchango wangu kwa Mheshimiwa Waziri ili waangalie wakati wa mawasilisho waone kama wanaweze kuyachukua kama mchango. Kama ile Kanuni nitakuwa sijaitimiza kwa maana ya kuleta mchango huo kwa maandishi kabla ya *Order Paper* kutoka lakini nitauwasilisha kama mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuchangia katika Muswada huu. Naungana na wengine katika kuongeza mawazo kwa sababu nimeusoma Muswada huu kwa kina, lakini nadhani ulikuwa haujaiva vizuri, kwa sababu kuna mawazo nadhani yalihitajika kutoka pembe zote za nchi na kutoka kwa wadau. Nitaambiwa wamechangia, lakini nadhani *definition* yake

na *scope* yake si kubwa kiasi ambacho tulitarajia kufuatana na title ya Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Spika, neno kuwezesha lina maana kubwa na unaweza ukalenga makundi mbalimbali. Unaweza kutaka kumwezesha mtu binafsi na mtu binafsi kwa Tanzania tuko milioni thelathini na ngapi katika kuwa ubinafsi kwetu. Unaweza kutaka kuwezesha familia, kuwezesha kijiji, kuwezesha Wilaya au kuwezesha Mkoa au kuwezesha Taifa kuweza kufanya mambo yake katika shughuli za kiuchumi.

Sasa nilipokuwa nikiangalia Muswada huu kuna mambo yalikuwa yana pwayapwaya kidogo na hii inatokana na kuwa na programu nyingi. Kwa mfano, tumetunga sheria hapa ya mwaka 1999 ya Ardhi, tuliitunga tukifurahia kwamba tunataka kuwawezesha Watanzania waweze kuweka ardhi kama *Collateral* kwenye mabenki. Lakini ukiangalia viwanja vinavyopimwa huko Wilayani na mashamba ya watu kwa kweli havipo na bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nayo ni kidogo sana na wataalam hawapo. Sasa hilo tangu mwaka 1999 mpaka sasa hivi imepitia miaka mitano. Sidhani linatekelezeka na linapimwa kwa kiwango gani kwamba watu wale wamepimiwa mashamba yao na nyumba zao zimepata *title deed* na vitu vingine. Sasa haya mambo tunayoyafanya tunarundika hili, tunarundika hili ndiyo yanayotufanya wakati mwingine tukose *balance* na *focus*.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilitembelea Tarime kule Rarya, sasa kule wana pombe na wanaivisha togwa, sasa nilipofika wakasema babu babu, hebu tupe pombe, aah, sasa nikawaambia niwape pombe eeh, walikuwa na gongo pale, nikawambia lakini hiyo gongo mnayokunywa ni haramu. Wakasema aah, wewe tununulie, lakini wakasema wakati mnagombea si huwa mnatununulilia?

Sasa nikasema si mngeniuliza mnataka soko, lakini hamwezi kupeleka gongo haramu kwenye soko, lazima kwanza tunaiweka kwenye mitambo tunai-*distill* vizuri tunaondoa ile *gas* inayoua watu halafu inakuwa nzuri. Halafu mnauza na Mwanza, mnapeleka na Nairobi mnapata soko. Kwa hiyo, pale tutakuwa tunawawezesha wanauzua gongo nyingi kuliko niwanunulie hapa mlewe halafu mfe. Ni katika kuwezeshaji. Sasa nikawaambia Mbunge mnanidai gudulia la pombe, halafu akishakununulilia na kampeni zikiisha akikaa hapa anasema pombe ile ni haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naelewa katika haya ninayotaka kusema sisemi wauze pombe haramu, lakini tuangalie hizi bidhaa walizonazo watu, kwa sababu najua pombe wanaivisha huku kwingine na inaua watu ndiyo maana wazungu waliipiga marufuku. Lakini najua magari yanababishi ajali nyingi katika Tanzania na dunia hii lakini hawajazuia yasiende. Ila ninachojua wameweka sijui gavana na sheria na UKIMWI unaua, lakini tunaweka kondomu. Sasa kama tunataka kuwawezesha hawa tungeweza kuangalia wa nini hawa watu wa Rarya pale wana gongo yao sisi tunawapiga virungu. Hivi hakuna njia za kisayansi na kiteknolojia za kuwasaidia na gongo yao hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuna wafugaji wengine wako huko ukivuka ukaenda pale *DRC* kilo moja dola 10 ya nyama na soko halipo, lakini kuna watu wa ng'ombe huko. Sasa tunawawezeshaje na haya ya kwenye Muswada sisi tunazungumzia kukopa, kukopa hela, unajua ukitaja hela kila mmoja masikio yanasmama hivi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, unajua Tanzania na Watanzania ni kama watu ambao wanasaafiri baharini. Nakumbuka mwandishi mmoja wa Kiingereza wa Mashairi, TS Corige aliandika shairi akasema: “*Water water everywhere nor no drop of water to drink.*” Sasa alikuwa baharini maana baharini maji ni ya chumvi, sasa anasaafiri maji kila mahali lakini sasa hakuna hata tone la maji ya kunywa. Sasa wewe nchi kama hii ukianzia Rarya kule ni dhahabu mpaka kule Mtwara, ukianzia kule Kigoma dhahabu mpaka Tanga, maji sijui tuna bahari, tuna maziwa mangapi tunakwenda kuomba chakula kule Ethiopia.

Sasa hizi raslimali sisi ambao tunadhani ni maskini tunazizungumzaje katika Muswada huu, tutumie hizi tuache kuwa Taifa la maskini alilokuwa analisema Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. Utajiri kila mahali lakini umaskini kila mahali.

Mheshimiwa Spika, sasa ndiyo nikawa naangalia Muswada huu. Kwa mfano, madini imezungumzwa hapa dhahabu mwaka 2003 wameuza dhahabu ya karibu shilingi bilioni 500 na Tanzania tukapata kupidia mrahaba na kodi zote bilioni 45. Kwa hiyo, kwa miaka 10 wao watakuwa wameuza dhahabu karibu ya trilioni 5, halafu sisi tutapata bilioni 450 ambayo wala siyo robo ya bajeti ya Tanzania kwa miaka 10. Kwa sababu wao wana teknolojia na walikuwa na mtaji, trilioni 5 zote zimekwenda, sisi tunapata bilioni 450 kwa miaka 10 kwa projection ilivyo kwa mahesabu hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inakuwa kama mtu ana mbuzi na kisu, lakini hana moto, hana chungu, hana binzari, hana nyanya na viungo, sasa unakabidhi mbuzi wako na kisu ili mwenye moto na sufuria na maji anapika anaunga, anakula nyama zote wewe anakuachia michuzi ndiyo maana yake.

Mheshimiwa Spika, hii katika uwezeshaji nilipokuwa nasema uwezeshaji wa ngazi ya Kitaifa maana hata hizo fedha wanakopa kule kuja kuwekeza hapo kwenye mitambo. Katika nchi nyingine kama Botswana badala ya kununua yale ma-*bulldozer* na mitambo mizito mizito wanunua mle nchini, lakini sisi hakuna hata kipuri hata nati, vyote wanakwenda kununua kule Ulaya. Kwa hiyo, hata zile fedha wamekopa huko zinarudi huko na dhahabu inakwenda huko na kila kitu kinaenda huko. Lakini humu kwenye Muswada hatuwezi kusema na tunacheka. Nadhani Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa sahihi alipokuwa anasema wanakupa kichupa unawapa dhahabu.

Sasa tunaposema kuwekeza hapa ku-*empower* hii Serikali ambayo tunafika hapa hivi tunadhani kuna mtu atakuja kutujengea viwanda vya msingi. Nakumbuka wakati ule wa Chama cha Mapinduzi wakati wa Ujamaa walikuwa wanazungumzia viwanda vya msingi sijui wanaita *Primary Industries* sijui wanaitaje? Viwanda vya Msingi kwamba una watu wanataka kuwekeza waje kwako wanunue vipuri na mitambo mizito mle. Mimi sidhani kama kuna mwekezaji atakuja kutujengea hapa.

Sasa sisi kama Taifa tunajiwezesha vipi kujenga hata hilo na pale ambapo wawekezaji wengine hawataki maana yake wanakimbilia kwenye vitu ambavyo ni *very simple*, wanakimbilia kwenye simu alikuwa anasema hapa Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, anafyonza zote ana simu na wanaiza akili pale, sasa sisi teknolojia tunapuuza. Maana *handset* ya simu wala siyo kubwa kuliko redio, redio ni shilingi 20,000/=, *handset* ndogo hivi wala hakuna chochote mle ni akili tu shilingi 500,000/= halafu tunachecha. Sasa tunapotaka kujiwezesha katika sheria hii sisi hilo tunaliangaliaje?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia humu ndani ya Sheria wana *define* hapa *Minister* wala *Minister* hawasemi yule anayeondoa Umaskini na Kitengo cha Kuondo Umaskini kiko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, sasa hii wanataka kupeleka kule kwa Waziri Mkuu, Sera huko, Maafa huko, sijui kufanyaje na kilimo niliona ilipelekwa huko kwenye Bajeti juzi, hivi kwa nini tusigawane na Makamu wa Rais akapata hapo ili huyo Waziri aliyepo akatajwa hapa, maana yake huyu Waziri anayetajwa hapa ni hewa labda Mheshimiwa Rais akimteua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii kazi ya kujilimbikizia majukumu na kuyalimbikizia sehemu moja si vizuri ndiyo maana tunafika mahali tunakwama. Naungana na waliokuwa wanapendekeza kwamba tujue ni *percentage* ngapi na *sources* za *hizo funds* tunazipataje? Maana tunaanzisha hapa tunafurahi Muswada mzuri, Muswada mzuri, lakini *ultimately* tunapimaje matokeo ya kile ambacho tulikusudia na tukapoteza muda hapa tunajaribu kutunga.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kusoma *functions* zingine *without prejudice* ni ukurasa wa nane *to the generality of subsection (1), the Council shall have the duty to.*

Sasa anazungumza mambo mengine ya ushirika hapo, Wizara ya Ushirika na Masoko, anazungumza mambo sijui *Business Investment*. Kuna vitu vingine anavirudia rudia humu na anachukua majukumu ya Taasisi zingine ambazo zipo na hawajaziimarisha, lakini wanarukia vitu vingine. Kwa hiyo, tungkuwa tunaomba kwamba kwa kweli wawe *more specific* na tujue wanachopaswa kukifanya ni nini na ukiiangalia hii kama mtu anataka kuwezeshwa sijui anatoka Rorya, sijui anatoka Kyerwa kule inabidi aje huku, wale watalaam sijui wana nini hapo. Kwa hiyo, tungeomba yale mapendekezo yaliyokuwa yanatoka yaweze kuwekwa katika sheria hii ili tuweze kuelewa tunachokifanya ni nini.

Mheshimiwa Spika, niungane kwa mara nyingine tena na aliyeshauri kwamba kuna watu wame-*invest* hapa wakachukulia *advantage* ya sisi kutoelewa biashara kubwa za Kimataifa zinafanyika namna gani, kutoelewa wakatufyonza kama hao wa kwenye madini na wengine wanaofanya shughuli kubwa. Tuwawekee humu sheria kwamba tunajua mnatunyonya na kwa sababu wanajua wanatunyonya wao tuwawekee sheria tuwakamate. Maana inafika mahali inakuwa kama mfalme mmoja ana mashamba makubwa huko ya miti na miziga ya asali huko anampa mtu anakwenda anarina asali mapipa na mapipa yamejaa halafu anaiba yecheza glasi moja utamu tu ndiyo

anaita watu anawatangazia kwamba asali ni tamu kweli na ile glasi yake. Halafu mapipa yote yanaselekwa kule na watu wanashangilia asali tamu tamu.

Sasa kuna watu kwa kweli wamewekeza huko tuwambie *we have to study, we have tell the facts*, tuwe na takwimu tuambie kwamba kwa kweli tulikuwa na sheria hii, tunadhani sisi tulikuwa hatujajua *the mechanism, the dynamism of liberalized Economy*, lakini tunadhani mnachukua *the lion share* na hapa na nyie lazima m-contribute hiki na hiki ili tuweze kuweka kwenye Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani kwa upande wa Serikali wamesikiliza sijui sasa watafanyaje, kwa sababu muda umetubana, lakini nadhani mawazo yaliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kweli ni ya msingi wangejaribu kuongeza ongeza humu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofî*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti

MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Muswada huu. Muswada huu ni Muswada muhimu sana na ingekuwa ni vyema kama tungepata muda wa kuufanya kazi zaidi. Lakini kwa sababu umeshafika hapa na kwa sababu ya umuhimu wake na kwa sababu sheria huwa haikatazwi siyo msahafu tunaweza yale tutakayoyasema yakaletwa baadaye kama mabadiliko ya sheria, lakini sheria hii ina umuhimu wake katika dunia ya leo tunavyokwenda.

Kwanza kabisa, ukiangalia *title* yake *the National Economic Empowerment Act*. Nadhani ile ndiyo inatuchanganya wengi wetu kwa sababu *title* ni nzito na ndani ya Muswada tulipaswa kuwa na uzito huo huo kwa sababu *National Economic Empowerment* ni suala zito sana hasa wakati huu ambapo tunajaribu na sisi kama nchi kuingia katika utandawazi. Lakini pia kuweza ku-compete kwa mfano, katika maeneo tunayoshirikiana wenzetu kama Jumuiya ya Africa Mashariki, Umoja wa Afrika, dunia nzima na kuna masuala mengi tu bila kupitisha Muswada kama huu tunaweza tusishiriki kwa nguvu ambayo tunatakiwa kuwa nayo.

Moja, ambalo ninafikiria ni la umuhimu kulizingatia ni tafsiri ya *Economic Empowerment*, unataka kumpa nani uwezo. Sheria hii nadhani ilikuwa inakusudia sasa kwenda kumpa Mtanzania uwezo wa kuendesha uchumi wa nchi yake na hapo kuna phase. Kwa sababu kama tukiangalia historia ya Tanzania tulipitia katika historia ya kuwa pamoja na kuzalisha kwa pamoja. Tumeondoka hapo tukajenga mashirika, viwanda na tukasema viwanda hivi viko mikononi mwa umma. Tumebadilisha tukasema wakati umepita wa Serikali kumiliki baadhi ya njia kuu za uchumi lazima ziwe mikononi mwa watu binafsi na bahati mbaya watu binafsi hao ikawa ni wagoni akija mgeni anapata hivyo vitu tulivyokuwa tumevijenga vikiwa ni njia kuu za uchumi kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kukawepo pia na mchanganyiko kidogo wa kutoeleza vizuri unaposema ubinafsishaji maana yake ni nini?

Mimi nafikiria Muswada huu kidogo unaanza kuleta matumaini tukiuweka vizuri ya kwamba tulitoa kila kitu tulichokuwa nacho. Ubinafsishaji maana yake ikawa ni ugenishani yaani ukimpa mgeni ndiyo umebinafsisha. Sasa tunarudi mahali labda tulihitaji hiyo hatua ili tuweze kusonga mbele kwamba hivi tulivyokuwa vimedorora mikononi mwetu tunawapa hao wageni sasa tunaanza kujipanga upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Muswada huu una maana hiyo ya kwamba sasa tunaanza kujipanga upya kama Watanzania kwenye kuendesha uchumi wa Tanzania naunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya *Economic Empowerment* iwe ni tafsiri ya kwamba Watanzania tunajipanga upya na tunatumia nguvu zetu zote sasa kuwawezesha Watanzinia. Ipo mifano, mimi nimekaa India nikiwa Balozi, Wahindi wale wamefanya juhudji kujiondoa kwenye umaskini lakini wakihakikisha ya kwamba ni Wahindi ndiyo wanaendesha uchumi wa India na wale wengine wanakuja kuongeza nguvu tu za teknolojia, lakini Mhindi ndiyo ameshikilia. Ukienda kwa wenzetu Nigeria pamoja na mazonge zonge yao ya hapa na pale, uchumi mkubwa wanaendesha Wanigeria wenye. Kwa hiyo, ukienda hapa jirani zetu wa Kenya pia na Uganda wanaoshika uchumi wao naona ni Wakenya wale ambao unaweza ukasema *this person matters in the economy of Kenya or Uganda* anakuwa ni Mganda ama ni Mkenya na wageni wanakuja kuongeza.

Sasa mimi alipokuwa anapendekeza Mheshimiwa Mbunge mmoja kwamba watakaochangia ni pamoja na Watanzania wenye uwezo, mimi siwaoni ukiangalia mara nyingi tunakimbilia kumwona Reginald Mengi, lakini katika muundo wa uchumi wa dunia hii Reginald Mengi naye anahitaji kuwezeshe ili atupeleke mbele zaidi. Bado yuko katika hata siyo *middle class* ile ni *middle class* kulingana na Tanzania.

Lakini *middle class* ya kwenda kwenye utandawazi hatujajenga Watanzania kweli watakaoweza kuhimili vishindo hivyo. Nitatoa mifano, *AGOA* ambao ni mpango wa Marekani kuruhusu bidhaa kwa kuota zipelekwe katika soko la Marekani bila vikwazo. Sisi tumeweza kiasi gani tusingeweza hata kama tungepewa hiyo fursa ya kupeleka bila hata malipo ya usafirishaji kwa sababu tulikuwa hatuna cha kusafirisha.

Kwa hiyo, nadhani sasa tunajipanga upya. Baada ya kusema tunajipangaje huu Muswada una maana wa kumkopessa mtu mmoja mmoja kama *SACCOS* tukienda nao hivi tutapoteza lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu lazima tukubali siyo wa *SACCOS* wala siyo vikundi tunavyo viunda sisi akina mama wala siyo kwa ajili ya watu ambao anataka kuanza mradi wa vitumbua au mradi wa kuuza mitumba, mimi Waziri utanisaidia sidhani Muswada huu ni wa namna hii. Muswada huu ni wa kuweka nguvu ya kwamba sasa hivi tumefikia mahali ukiangalia Bajeti yetu pesa zetu kubwa zinaenda wapi kwa sababu sisi hapa ukiangalia Bajeti yetu tunaweka kwenye *construction* mabilioni yanaenda kwa nani.

Ndiyo tunapashwa kujibu huu mfuko ni lazima uwezeshe *construction industry* inayoendeshwa na Watanzani ili kama tunaposema ni bilioni mia moja zinaenda kwenye barabara tunauhakika zimezunguka zimetoka Hazina zimekwenda kwenye mikono ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo za kugawana kwenye mifuko ya *SACCOS* hiyo tuitafutie utaratibu mwingine. Nitatoa mfano mwingine tuna Dr. Massawe, Mtaalam wa Upasuaji moyo, kijana huyu amehangaika hatumwezeshi. Hao ndiyo wataalam ambao unasema sasa kama wewe unauweza ambao ni maalum unatafuta tu kujenga hospitali unatafuta tu vifaa kwa sababu vifaa vya moyo vingine vinauzwa kwa bilioni tatu za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kipande cha *bypass* ni dola elfu nne ili aweze kukufanya *bypass* kuokoa moyo wako. Huyo sasa unamtenga kwa sababu atapunguza gharama za kupeleka watu nje kupasuliwa mioyo. Ndiyo nadhani mfuko huu mimi ninavyo ufikiria ya kwamba siyo wa kugawana sisi kwenye *SACCOS* kwa hiyo, ukisha sukuma huko utapata na wengine wa wataalam ambao tunalalamika wako nje watajitokeza, watakuja kuwezesha kwa hiyo wataikwamua Tanzania katika eneo hili.

Tuna wataalam wengi *specialists* katika teknolojia, tutasukuma huko ili kusema sasa katika uundaji wa teknolojia wapo watu tumewawezesha wanaweza kutengeneza ama kutusaidia kuunda teknolojia zitakazo sukuma uchumi ambao sisi sasa tunaupita kwenye *SACCOS* na mahali pengine tunaweza kutumia uwezo huu, uwezo wa kurudisha uchumi wa madini mikononi mwa Watanzania. Tumeshawapa kwani tumewapa moja kwa moja tumewapa lakini mfuko huu ndiyo wa kujipanga upya. *Geologist* Watanzania wako wapi tuwawezeshe warudishe madini mikononi mwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ya mfuko huu, mambo ya kutizama samaki na uvuvi *as an industry* siyo mvuvi mdogo mdogo yule atawezeshwa kwa sababu umeshaweka *industry* ya Watanzania inayoweza sasa ikapokea mazao ya hawa ikayasindika ikayapeleka katika hali ambayo ni bora zaidi.

Kwa hiyo, mimi langu Mheshimiwa Waziri ambalo nitaliomba kutaka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lile la kusema kwamba tafsiri ya hii haikuzingatiwa vizuri katika Muswada kwa maana hiyo tusipopata *council* nzuri inayoundwa watafikiria wamepewa kugawanya pesa hawatakuwa na dhana ya kwamba wamepewa kazi ya kuwezesha ili Watanzania baadaye waje washike hatamu za uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapo sasa tumerudi kwenye ujamaa na hata Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, amekubali, ndiyo hiyo ilikuwa maana ya ujamaa ya kwamba tunawawezesha Watanzania, Watanzania wanashika hatamu huko kote tumeaiti tunayumbayumba sasa Muswada huu ndiyo ulikuwa wa muhimu na ndiyo maana nilikuwa nasema Mheshimiwa Waziri kama itawezekana tuupitishe lakini mapema iwezekanavyo tuurudie tena, tuurejee kuangalia ni namna gani tunaweza kuupa nguvu Muswada huu kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema dunia inavyokwenda tunachelewa na Muswada huo tusiuchanganye na *SACCOS*, tusiichanganye na vikundi, tuisichanganye na mikopo midogo midogo lakini ielekezwe katika kujenga.

Mwisho tunajua sitataja majina kuna makundi fulani tutakapojenga ndiyo watakaopewa, wa rangi fulani, wa urefu kiasi fulani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu usirudiwe tena, tumewawezesha vya kutosha, tusione aibu kufika pale ilipofikia kwa kutamka *South Africa* iliposema *Black Empowerment*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mmoja hapa alipotamka uzawa wote tukaguna guna, lakini *he was right* hakujeleza vizuri tu ni lazima tufike mahali tuone hizo pesa tunazomchukulia za dhahabu na samaki anapewa nani. Naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Omari Mjaka Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Muswada huu muhimu. Kwanza nataka niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu na nataka nitamke kwamba naunga mkono asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia Muswada unatueleza kwamba chimbuko la kutunga sheria hii inatokana na historia na hali halisi ya maisha ya Watanzania kwa hiyo hapo nataka niipongeze sana Serikali kwa kuliona hili na kwa kuliunganisha hili nataka niungane na maneno ambayo amemaliza Mheshimiwa Getrude Mongella, sasa hivi kwamba lazima tuangalie ame-*quotehapa* kwamba Watanzania, kwa hiyo ni vizuri tukajipanga vizuri tukaangalia hali ya maisha ya Watanzania wetu kuwainua kiuchumi na kimaendeleo. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Serikali itasimamia na kuona umuhimu wa Muswada huu kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine pamoja na kwamba Muswada huu tunaujadili na kidogo nimeshtuka kuambiwa Muswada muhimu kama huu kwamba utahusu Tanzania Bara. Sikuvunjika moyo na nashukuru kwamba Muswada huu umepitia katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ningeomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inahusu Tanzania Bara tu ikaangalie tena Muswada kwamba ungahusu kwa Tanzania nzima. Zanzibar ni nchi maskini sana, Serikali ya Zanzibar hivi sasa inavyokwenda nyote mnajua uwezo wa kiuchumi hatuna kwa hiyo, ni vizuri yanapotokea mambo mazuri kama haya mngeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote ile inaendeshwa kutokana na kodi za walipakodi katika nchi yake, siamini kama Zanzibar inawalipa kodi wa kutosha ambao

inaweza kuendesha ile nchi. Kwa hiyo, ni vizuri wananchi wanategemea kupata misaada katika Serikali yao ni pamoja na Miswada kama hii. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala hili ikaliangalie tena, kwa sababu tunapozungumzia maisha ya Watanzania ni pamoja na wale walioko Zanzibar. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kutaka kuwapatia Watanzania maendeleo ya kiuchumi basi ni ligusane na suala zima la elimu katika maeneo yote. Tunafahamu mpango mzima wa Serikali ulivyoandaa mkakati kutoa elimu mashulen, shule za msingi na sekondari lakini kuna eneo moja kubwa sana tunalisahau, kwa wakulima wetu na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanastahili wapate elimu ya kutosha ili kuweza kujenga nguvu zao za kiuchumi na kimaendeleo kwa maisha yao na kwa faida ya Taifa hili kwa hiyo, vile vile niombe Serikali sambamba kwamba inavyoimarishe katika shule ya msingi na sekondari lakini eneo la wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo waliangalie na walijengee mikakati ya kuwapatia elimu kwa faida yakuwajengea misingi mizuri ya kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa ushahidi kamili nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, ambayo ametoa siku ya sherehe ya Walimu Duniani iliyofanyika Kisiwani Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alizungumza kwamba tumekutana hapa kukiri huu umuhimu wa elimu katika maendeleo ya Taifa letu na watu wake. Lakini sehemu ya pili vile inasema kukua kwa uchumi wa maendeleo ya Taifa letu nako kutategemea sana uwezo wetu na kutoa elimu bora.

Kwa hiyo, tuisianglie upande mmoja tu wa wanafunzi lakini wakulima wetu nchi yetu ni kubwa ina ardhi kubwa tuna maji mengi lakini suala la kilimo wananchi wetu elimu kwao ni ndogo sana. Kwa hiyo, tuwawezeshe wataalam wetu hata wale ambao wamestaafu kama watajitolea kwenda vijiji kuwaelimisha wananchi juu ya kilimo bora ili kutoa mazao ya kuendeshea kimaisha na kuuza nje ni vizuri tukaliangalia eneo hili tukaweza kuwasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kwenda kwenye kilimo hatufiki, tutazungumza tu hapa juu juu na mimi nina ushahidi, mara moja nilialikwa mahali na nilipokwenda ulipokuja ule ujumbe wa wale wajumbe kutoka *EU* nikamwuliza yule mmoja katika hizi nchi za *European Union* ni nchi gani ambayo imeendelea kiuchumi akasema Ufaransa na sababu kubwa akasema kwa sababu wana ardhi kubwa.

Kwa hiyo, tuangalieni wenzetu wanavyoitumia ardhi kuwakomboa wananchi wao kimaendeleo kwa hiyo, nimelizungumza hili kwa ushahidi kamili. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ikaliangalia suala hili kwa mapana sana ili kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni lazima tujenge mipango mizuri katika utawala bora, sera zetu kama tutaimarisha maeneo hayo katika utawala bora na tukaweka sera nzuri nataka nikuhakikishie kwamba Taifa letu litafikia mahali pazuri na haya malengo ambayo tumeyakusudia inawezekana tukaweza kufanikiwa.

Mimi nadhani niitahadharishe Serikali tusiwe wazuri kuleta Miswada kama hii tukaizungumza lakini tuwe wazuri tunapojadili masuala kama haya yaweze kuleta mafanikio makubwa kwa taifa letu. Mfano hai katika elimu tumeona mabadiliko makubwa katika *TASAF* tumeona mabadiliko makubwa lakini suala la kilimo na mifugo tuone kiasi gani wananchi wetu wanatoka katika umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inanishangaza kwamba watendaji wa vijiji na Serikali wanashindwa kuwashawishi wananchi kujijengea nyumba bora wakati mtu anamiliiki mifugo karibu 4,000 pengine akiuza ng'ombe hamsini tu anaweza kujenga nyumba na kwa Tanzania hii wenzetu ni wataalam wa kupiga yale matofali ya kuchoma kwamba gharama yao itakuja kwenye kutafuta saruji labda ya kulipia fundi na kununua batii. Kwa hiyo, moja la kumtoa Mtanzania katika unyonge ni kupata mahali pazuri pa kuweza kuishi. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali Kuu kuwaelekeza watendaji wake wa Vijiji wa Majimbo, wa Wilaya, wa Mikoa na Taifa kusimamia suala hili kwa faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ningeiomba Serikali kupitia Muswada huu ikaliangalia zaidi, tusije labda kuwezesha wananchi ni kuwakopesha fedha tu labda watafanyabiashara hivi mnamfanyabiashara nani? Lakini mazingira mazuri ya kuishi ni kitu cha msingi hilo, lingine nataka nilichangie hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna mwenzangu mmoja hapa ame-*quote* gazeti la juzi na mimi niliona kwamba kuna wakulima kutoka India wanataka kuja kuwekeza Tanzania lakini nilishtuka sababu kubwa waliozungumzia kwenye lile gazeti inasema kwamba ni kutokana na hali ya ukame ambao umewakumba kule kwao na watu wengine waanza kufa kutokana na hali ile ya njaa. Kwa hiyo, Serikali inavyopokea watu kama hao iwe waangalifu sana isije leta migogoro na migongano katika maeneo leo watafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushahidi huu kwa sababu wanaweza kuja wawekezaji tukaona labda ni wawekezaji wakubwa kwenye Taifa letu lakini ikawa ni makundi ya kijasusi katika Mataifa ya Kimataifa na tukiangalia stori ya lile kundi la mafia ambalo sasa hivi linaenea katika sehemu kubwa ya dunia lilianzia hivi hivi tu. Lilianzia Italy limesambaa karibu nchi zote za Japan na Marekani na maeneo mengine. Kwa hiyo, Serikali inapoweza kuwapokea wawekezaji kama hawa iweze kuangalia wana uwwezo gani na watasaidia vipi Taifa si kuja kuodhi ardhi tu ambao itawatia unyonge wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ili kuwawezesha wananchi tunahiji umoja wa Kitaifa katika Taifa letu hili. Sisi viongozi sote tuwe wakweli kuwaeleza ukweli wananchi wa taifa hili, ni nini majukumu yao kwa Taifa lao. Lakini kama itakuwa si

viongozi huyu ana sera hizi huyu anasema hivi tunawababaisha wananchi hawajui misingi gani wafuate itakuwa bado hatujawafanya haki wananchi na haya tunayopanga kama miswada na sheria hizi kwa kweli hayatofika popote. Kwa hiyo, hilo kama Watanzania tungepaswa kuliangalia kwa mapana na marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nimtakie mafanikio Mheshimiwa Waziri lakini vile vile Serikali iangalie yale maeneo ambayo sasa hivi yameanza kupata ukame, kwa sababu inaonekana sasa hivi tunakwenda kwenye uchaguzi tukaja tukasahau kama kuna maeneo wameanza kuathirika kwa ukame. Sasa tunazungumzia kuwatoa wananchi katika kuwapatia maisha na kuwaendeleza kiuchumi lakini wengine wanakufa kwa njaa tuangalie kweza ku-cover yale matatizo ili yasijetokea kama yale yaliyotokea pale kipindi cha nyuma.

Mwisho naunga mkono Muswada huu, nautakia mafanikio lakini ombi langu kwamba Zanzibar muiangalie, hatuna uchumi kwamba ikiwezekana katika Muswada huu hasa huko Ofisi ya Waziri Mkuu umesikia na Waziri Kiongozi tusaidie. Ahsante sana naunga mkono.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika muswada huu. Kwanza kabisa naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Lakini vile vile ningependa kuungana na Mheshimiwa Getrude Mongella, kwamba mambo haya makubwa mnakuwa na mahala pa kuanzia mimi nitahesabia kwamba Muswada huu ulivyokuja unakuja kama kuanza lakini ile *thrust* ya *empowerment* vyote havijazingatiwa yote kama inavyochukua katika Muswada huu.

Ukizingatia uzito wake, kwa mfano kwenye *preamble* ya Muswada naomba uniruhusu niusome kama ulivyoandikwa ule ukurasa wa tano ile *paragraph* ya tatu kutoka juu inasema hivi: “*Now therefore with a view to promoting rapid economic growth that will facilitate broader economic ownership by Tanzanians deliberate to measures are taken to establish structures and mechanism to redress the existing economic inequalities among various sections of the population.*” Sasa ukisoma hii unaridhika lakini ndani kule hakuna kitu kwa maana hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili mambo haya ambayo ni *obvious* yaani ni wazi hivi hakuna haja ya kuona haya kuyasemea kwa sababu mkiona haya mtafanya vile ambavyo mtakuwa mmefanya kama kuogopa na hamtaki kuwa wakweli. Kwa mfano hakuna asiyejua Tanzania nani ambao wako nyuma na Muswada huu ambao tunauzungumzia ungezaa kutazama Miswada yote itakayokuwa inaletwa katika bunge. Kwa mfano ule Muswada unaokuja wa *Procurement* nao pia ungefananafanana na *empowerment* kwa watu wetu. (*Makofi*)

Kwa mfano uko ujanja mkubwa sana unaotumika katika *tender* yako, makampuni ya watu wakubwa ambao kibiashara walishapiga hatua wana makampuni zaidi ya moja na utakuta kampuni moja ndiyo inafanya kazi zingine tano au sita zimewekwa kwa ajili

ya kungoja *tender*. Kwa hiyo, familia moja inaweza ikaomba *tender* moja kwa kupeleka makampuni yao kumi. Kwa hiyo, Watanzania wa kawaida, mimi nimejaribu, nimefanya utafiti wa hakika *tender* zote ukichukua kwa mfano mtu akikwambia nani tajiri Tanzania wote tuseme ni Serikali ya Tanzania. Kwa utajiri wa Serikali ya Tanzania sasa hivi baada ya miaka michache mtanona unamilikiwa na makampuni ya familia zisizozidi kumi katika nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hiyo inatoka wapi, inatoka kwa fedha ya Serikali hizi hizi za Bajeti zilizopitishwa katika Bunge hapa. Kwa mfano, tuliweka Bajeti, nitoe mfano tu trillioni tatu, hii trillioni tatu zitakwenda kwenye *tender* ya barabara zitakwenda kwenye *tender* ya vyakula na kadha wa kadha. Wanaoomba hawazidi kumi katika nchi hii na ujanja ni wa kampuni moja zaidi ya kampuni moja. Kwa hiyo, utajiri wa nchi unakwenda kwa mikono ya watu wachache tu. Sasa *procurement* yenye we itakuwa tusubiri isije sasa mpaka tuangalie kama kweli inazingatia *empowerment concept* ya sheria, lakini inapokuja pale watanufaika wale wale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulisema ni hivi ziko raslimali ambazo ni ya haki yetu Watanzania na hizo ndizo zilitakiwa tuanzie nazo ukitazama *concept* nzima ya hii ni kama tunaanzisha shirika la umma. Mimi sidhani kama shida ya Bunge ni kuanzisha shirika la umma litakaloanzishwa kwa mfano utazama ibara ya 23 na 24 inazungumza habari ya *promotion* na habari ya kumiliki mimi nisingekubaliana kwamba chombo hiki nacho kianze kumiliki lakini kingeweza kuchukua mfano wa *South Africa* wenzetu wanachombo kinachoanzisha kwa niaba na kukabidhi. Mnakuwa na watu ambao mnajua ni *disadvantage* lakini wanauwezo kwa mfano sekta ya utalii, sekta ya kilimo na kadha wa kadha mnakuwa watu mnawajua na mna-data benki ya Watanzania ambao mkizungumza, kwa mfano mtu akizungumza kilimo ukimuweka Mzindakaya hujakosea maana hii ndiyo sekta yangu. (*Makofî*)

Lakini mimi nataka niishukuru Serikali ya Tanzania kwamba katika jambo hili imeanza kufanya vizuri sana na mimi mwenyewe naweza kusema ni mfano kwa sababu katika hili mimi siwezi kulalamika nimewezeshwa kwenye kilimo lazima niseme ukweli Bungeni mjue ukichukua Ubunge *South* itaishukuru Serikali. (*Makofî*)

Sasa ninachosema nataka tufanye hivyo hivyo tena bila kuona haya kwa sababu gani kule kwa wenzetu *South Africa* nitoe taarifa kidogo hapo Mheshimiwa Mwenyekiti juzi tulikuwa *South Africa* na kiongozi aliyeongoza ujumbe wa Watanzania kwenda kukutana kwenye *conference* ya wawekezaji alikuwa *Prime Minister*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwa heshima kubwa Waziri Mkuu wetu alitujengea heshima kubwa sana katika ule mkutano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa sana, ulikuwa na watu, *participants*, washiriki mia mbili na kitu hotuba ya Waziri Mkuu ilifanana heshima ya Tanzania alisema vizuri sana. Mawaziri waliokwenda pia Waziri wa Kilimo na Chakula, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nishati na Madini wote walifanya vizuri na tunataka na heshima kubwa. Baada ya mkutano ule ambao ulikuwa na mchanganyiko Wa-*South Africa* weupe na weusi baadaye

Prime Minister amekutana na weusi tu na wakamweleza jinsi wao kule wanaita kabisa Black Empowerment.

Sasa inajulikana kwamba *South Africa* matajiri ni wazungu na hata hapa hata usiposema Bungeni kwa sababu sisi tumelelewa na Nyerere hatutaki ukabila ungeweza ukatumia maneno yaliyotumika ya kistaarabu ni kwenye Muswada ile ibara ya 22, *paragraph two F*, imesema hivi *immoveable*, inazungumza habari *more properties* halafu inazungumzia habari ya *therein* halafu mwisho kuna maneno sitaki kuwapotezea muda, inasema hivi: “*undertake and promote the education of the historically disadvantaged persons,*” sasa ukishawatamka hawa basi lazima uwe na mipango ya hao *disadvantages*.

Hapa hatutaki kutumia maneno *Black* ipo kwa sababu tumelelewa katika mfumo wa kukataa ubaguzi lakini tungeweza tukasema wazi wazi kwamba *disadvantage* zipo hawa waelezwe ujulikane. Maana wakati wa kutekeleza tutapata matatizo itakwenda kwa wale wale mimi ninao ushahidi hawa wachache wanaotajirika wamepata kutumia lugha chafu. Kwa mfano, mimi mtu mmoja aliniambia waziwazi, akasema bwana Mzindakaya ninyi mnatu-offend bure sisi hatuna Waziri hatuna Katibu Mkuu katika Serikali yenu na benki zenu zote na mashirika yote mnaendesha ninyi, ninyi wenyewe ndiyo mnatupa sasa mnatu-blame kwa ajili ya nini.

Mnatupa ninyi wenyewe na waswahili humu wote wenye madaraka, wawekezaji na hawa wote wakija wanatetemekewa kweli hakuna hata mswahili mmoja atashirikishwa. Huu Muswada ultakiwa vile vile useme kwamba kuhusu raslimali za nchi hii hakuna atakayeingiza raslimali yake bila kuona Mtanzania kwa mfano katika kilimo mbona hatusemi tutakavyo shirikisha Watanzania. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo utajiri wetu, mimi sina pesa ardhi ninayo, sasa akija mwekezaji anakwenda na nani, tungetakiwa tuseme humu humu kwamba *no investor shall invest in land without a local partner.* (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iseme ndani ya Muswada ndiyo uwezeshaji madini, madini kuna viji vyetu viko katika maeneo ya madini tutaje *a village near by the area* ambayo itakuwa *discovered with gold* au chochote itakuwa *partner* waziwazi tuseme kwa nini tunaona haya na mali ni yetu. (*Makofit*)

Kuhusu uvuvi vile vile, maziwa ni yetu ndiyo haki yetu aliyo tupu Mungu, uwindaji niwaeleze Waheshimiwa mimi nimefanya *study* na naendela kuikamilisha, wawindaji wote wenye *block* nzuri na nyingi ni *foreigners* kwenye kuwinda, kwenye hivi vitabu vya kuwindisha *investment* yake ni chini sana lakini utajiri unaotoka kwenye uwindaji ni mkubwa sana na hela zote zina kwenda hivi wawindaji wote hakuna anayewekeza Tanzania wanawinda wanakwenda na mali yetu sasa uko ndiko tungeweka tingesema hakuna kitalu cha kuwinda atakachopewa nje bila kutazamia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu ndiyo aliyopandia zawadi yetu mbona hatukuweka huu uheshimiwa sasa tutaweka lini hii ndio mali tuliyopewa na Mungu, akili tunayo sana siyo ndogo kwanini tumefuata kumuuzi katika jambo hili. Kwa mimi nasema

kama walivyosema Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, mimi naomba tukubaliane hapa kwamba kutoka sasa lazima Serikali muanze kuandaa kama mkichelewa sisi baadhi yetu tutaleta mapendekezo ya kufanya *amendment* katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuacha hivi kama ulivyo haujazingatiwa matakwa ya *national empowerment* kuna upungufu. Kwa hiyo, ndiyo ningependa niseme hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vile vile nigependa niseme jambo lingine kwamba aina ya biashara kwa mfano wenzetu nchi zote ukienda India ukienda *ASN country* zote kuna biashara ambayo wametaja ndani ya sheria kwamba mgeni hatafanya, itafanywa na *local people* maana hebu semeni hata hii *empowerment* Watanzania wangapi wataingia kwenye miradi mikubwa tutaanza kidogo ndiyo tukue sasa huko ambako ni kudogo tungesema hapa *foreigner's fine*, kwa mfano uchimbaji wa madini mdogo mdogo wafanye Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge niwachekesheni, *breweries* ni kampuni kubwa kule *breweries* wameanzisha *subsidiary company* za *breweries security* ni wao wenyewe wameunda jina la kampuni yao inafanya kwao na kwa makampuni mengine. Makampuni yote ya *South Africa* yanafanyiwa na kampuni ndogo ya *security* iliyoundwa na *breweries* kuziba matairi na kuuza matairi wana kampuni, *subsidiary breweries* sasa watu wetu watafanya nini. Kule kwenye madini sawa wafanye hayo makubwa lakini hata kuuza sukari na nyanya wanafanya wenyewe. Kwa mimi nilisema lazima tuseme vitu hivi watafanya Watanzania tu hakuna mtu wa nje kufanya ndani ya sheria yenewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wote Waheshimiwa Wabunge tumetembea, mimi nimekwenda Arabuni nchi zote za Arabuni wakubwa wanakwenda *ku-invest* wala hawakatai lakini huwezi kufanya bila *procurement* wale Waarabu wengine hawakuweza hata kuja lakini lazima uende nae pamoja ye ye anakaa nyumbani anakula kahawa wewe utapeleka fedha maana yake ana *participation* ya *share hands upon 25*. Sasa sisi kwetu ilikuwa *signing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningependa nirudie kusema tena kwamba nchi hii ni ya Watanzania wanaoichagua Serikali yetu. Tuji-*address* kwa watu walio wengi zaidi wala tusione haya katika jambo hili. Sasa hao wachache kila siku watakwenda na Serikali iliyopo, *this thing can happen any time*. Serikali yote kwao ni sawa tu. Ndiyo. Sisi hatuwezi kusema kila Serikali, tuiseme Serikali bila ya kuongozwa na Watanzania. Lakini wafanyabiashara *any government they have money*. Lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge mnaweza kusema *any government*?

WABUNGE FULANI: No!

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Watanzania wa kawaida wanaweza kusema *any government*. Haiwezekani, wale wafanyabiashara *any government*. (*Makofi*)

Mtaona hata katika Uchaguzi watapamba moto. Wakiona mtu ambaye ana mwelekeo mzuri watapambana wataingia hapo hapo. *Any government.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono. (*Makofi*)

MHE. LEONARD M. SHANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niongee kidogo kuhusu Muswada huu.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Muswada huu wakati muafaka. Muswada mzuri lakini nitakayoongea mimi sitarudia wenzangu ambao wameongea.

Katika ukurasa 29 wa Muswada huu ukiniruhusu nitanukuu inaanzia kuhusu madhumuni ya Muswada huu kuhimiza na kuhamasisha Maendeleo Vijijini ambako ndiko zaidi ya asilimia 70 ya wananchi Watanzania wanaishi. Mikakati hiyo ina lengo la kuendeleza harakati za kuondoa umaskini, kuongeza ajira kwa vijana, kuongeza nafasi za elimu, mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali, kuongeza vyanzo vya mikopo na kuongeza masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeuona Muswada huu ni mzuri na ukifuata *definition* yake unalenga hapo ambapo kweli sisi tulitaka kusikia. Lakini ukitazama undani wake nimeona kama ni *outline* tu kwa sababu hatujaona yale mambo ambayo yanalenga hawa asilimia 70. Kama unavyoolewa asilimia 70 ya watu Vijijini ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Lakini hali yao ni mbaya kwa sababu ya mazingira hayajawekwa sawa. Miundombinu ya kuwawezesha wao waweze kufanya kazi zao, shughuli zao za kimaendeleo haipo, miundombinu hiyo haipo. Sasa nilitegemea katika Muswada huu wa *National Economic Empowerment* inalenga kwamba kuleta mazingira ya wale asilimia 70. Inalenga kuhakikisha kuwa ile miundombinu inayotakiwa hawa wafanye kazi za kujiendeleza na kutokomeza umaskini imewekwa sawa. Lakini ukitazama sasa hivi Muswada huu umegusagusa mahali pengi tu. Tunavyoolewa kuwa wakulima wetu, kilimo chao kipo cha kutegemea mvua tu na kama hujaweza kubadilisha mfumo wa kilimo hawa wataendelea kuwa maskini. Sasa tunapoongelea kuwa tunataka kuwawezesha kiuchumi (*Economic Empowerment*) tutawapa kwa namna gani kama hatutawawekea miundombinu ambao wanaweza kufanya kazi zao.

Sasa mimi ningeshauri hapa suala la kuwa na *National Economic Empowerment Programme* iwekwe katika makundi makundi. Kwanza kabisa suala la watu wa Vijijini walengwe wao hasa matatizo yao yako tofauti na watu wa mijini na wafanyabiashara wadogo wadogo walioko mijini au wenye viwanda vidogo vidogo. Tukilenga hawa na tukiawezesha hawa utaona mabadiliko ya uchumi na watu wataweza kutokomeza umaskini. Miundombinu hii ni pamoja na kuziawezesha taasisi zilizoko Vijijini na hasa Wilayani, Halmashauri. Serikali ilianza vizuri kutoa ruzuku na kuwezeshe kusaidia Halmashauri kufanya kazi zao. Lakini hapa sasa ninavyoiona Serikali kupitia Muswada huu utoe uwezo wa kuziawezesha Halmashauri kujenga miundombinu ya kiuchumi huko Vijijini na Wilayani. Kwa sababu wananchi walio wengi ndio wanaishi huko Vijijini.

Sasa kama tutaongelea kuwawezesha wananchi kuinuka kiuchumi pasipo kuwainua wale walio wengi zaidi ya asilimia 70 kwa kweli itakuwa bado hatujalenga kuleta mageuzi ya kiuchumi katika Taifa letu..

Kwa hiyo, ningeshauri kuwa Serikali kuititia Muswada huu itazame uwezekano wa kuweza kuziwezesha Halmashauri kwa kuzipa vifaa mbalimbali vya kuweza kujengea miundombinu. Nchi nyingi zinafanya hivyo, nchi ya Morocco na Tunisia wanatoa vifaa vingi vya kuwawezesha Halmashauri zao. Isipofanyika hivyo kwa kweli haitawezekana kuleta mabadiliko yoyote kiuchumi kwa wananchi walio wengi Vijijini hasa kwa mfano kujenga barabara Vijijini kwenye mahali ambapo wananchi wanazalisha mazao itakuwa vigumu kwa sababu katika maeneo yale ndiyo ambayo ardhi zao *terrains most complicated* kuna milima, mabonde, mito.

Sasa barabara zenyewe zitajengwa kwa gharama sana lakini sio kwa ruzuku ndogo zinazoendelea kutolewe ambayo *mostly* itakuwa kutumia kwa matumizi mengineyo (*Other Charges*) lakini kwa vyanzo vidogo vya mapato za Halmashauri haviwezi kufanya kazi hizo za kujenga miundombinu ya kiuchumi. Pili, suala la kuhakikisha sasa kilimo kibadilike ni lazima vitu kama mabwawa na malambo yajengwe. Sasa hili ni tatizo ambalo sio kuwa halihusiki na Muswada huu. Kwa sababu ukiwawekea miundombinu kama ile wananchi wanawenza wakafanya shughuli za kuzalisha na wakaondokana na umaskini. Sasa hili lazima liwekwe sawa katika Miswada inayokuja, kama Muswada sio huu basi tuletewe Muswada mwingine amba o utaelekezwa zaidi katika masuala haya. Kwa sababu tunaposema kuwawezesha wananchi wa Vijijini tunazungumzia kinadharia tu hatuzungumzii kwa kimatendo. Matendo sio zaidi ya kuwajengea Miundombinu ya barabara, kwenda Vijijini (*Rural Feeder Roads*). Kuwajengea mabwawa kusudi waanze kulima kwa miezi yote wawe katika shughuli za kilimo, kuwapelekea umeme Vijijini na kuwaleta maji amba o wanawenza kutumia kwa mifugo yao na matumizi ya binadamu. Sasa hii ndiyo mifuko ambayo ningesema kuwa mfuko amba o tunazungumzia hapa ungelenga kufanya kazi hizi. Mfuko amba o utakuwa wa kuwawezesha kiuchumi wananchi wa vijiji asilimia 70 ya Watanzania.

Suala la mikopo mimi ningesema kuwa hata hivyo wananchi wetu wengi ni maskini sana. Nimezungumza mara nyingi hapa Bungeni kuwa kuna Shirika la *International Finance Corporation (IFC)* ilipata kufanya utafiti nchi za Amerika ya Kusini ambayo ikaona kuwa kuna uwezekano kuwakopesha wananchi pasipokutoa dhamana. Sasa hapa taasisi zetu za fedha hasa Benki zinahitaji dhamana ambazo lazima uwe na mali isiyohamishika. Wananchi walio wengi (asilimia 70) hawana mali kama zile.

Mimi ningeshauri katika Mfuko huu unaotajwa katika Muswada huu mojawapo wafanye shughuli ya kufanya utafiti jinsi ya kuwakopesha wananchi wetu pasipo kuweka dhamana zinazotakiwa ambazo haziwezekani wananchi wengi hawawezi kuzipata hizo dhamana. Kwa kufanya hivyo wananchi wanawenza wakakopa wakajiendeleza na wakachangia katika mfumo wa kisasa. Kwa kweli mpaka leo inatisha kwa sababu ni Tanzania nchi pekee ambapo wananchi wengi wanaendesha shughuli zao za kimaendeleo kwa kutumia fedha zao wenyewe. Walio wengi hawawezi kukopa. Lakini pangkuwa na

uwezekano wa kulegeza masharti ambao ndio Mfuko huu sasa ungelenga ingekuwa vizuri sana kwa sababu ungewezesha wananchi wengi. Pia ningeongelea kuwa Mfuko huu utendaji wake uwe wa kimkoa au kikanda. Mfuko huu tunauunda wengi katika viongozi wake na Makao Makuu yake watakuwa Dar es Salaam au kwenye miji mikubwa, lakini vijijini wananchi itakuwa vigumu sana kupata misaada ya mikopo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingewezekana katika Mfuko huu hata uongozi wake uwe Makao Makuu lakini *operations* zao na wataalam wao na ukopeshaji wao ufanywe vijijini. Nashauri kuwa Halmashauri za Wilaya ziwe ndio Makao Makuu ya Mfuko huu ambako wananchi walio wengi wanaweza kufikiwa. Sio suala la kuwa wawepo Dar es Salaam halafu viongozi wafanye ziara kwenda kutembelea vijijini. Ninashauri pia Mfuko huu usiwe mfuko wa kufanya vikao na semina kwa viongozi, uwe mfuko wa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kusudi waelewe jinsi ya kuondokana na umaskini na jinsi ya kujipatia uwezo kiuchumi. Pia Mfuko huu ungeona umuhimu wa kutazama katika taasisi na Mashirika yaliyokufa na kuona tumejifunza nini. Mengi ambayo yamekufa yalikuwa na matatizo ambayo yangeweza kuepukwa. Lakini leo Mfuko huu unaweza ukaanzishwa na ukatumukia kwenye uzembe ule ule au makosa yale yale.

Kwa hiyo, ningeomba Mfuko huu ufanye kazi ya kawaida (*prior studies*) kuona wapi tulikosea na wapi kuna mahali ambapo tumejifunza (*lessons learnt*). Kwa hiyo, mimi ningeshauri kabisa Muswada huu uone umuhimu wa kuelekeza kazi zake kwenye Mikoa na Wilaya na hasa ningeomba pia wafanye kazi moja zaidi. Kazi ya *economic arears zoning* yaani maeneo fulani ni ya ukame kwa hiyo yanatakiwa shughuli fulani ambazo hazitafanana na maeneo yenyenye mvua nyingi. Hapo ndio watafanya wananchi wale walioko katika maeneo yale nao wanufaikie. Sio lazima matatizo ya kiuchumi ya maeneo (*Regions/Districts*) yawe yamefanana. Kuwa na mtizamo wa Kitaifa itafanya vigumu kwa Mfuko huu kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao ambayo ni maalum katika maeneo yao.

Suala la kuona Kitaifa kama picha moja kwa kweli itakuwa vigumu sana kwa sababu maeneo hata Wilaya kwa Wilaya moja zinatofautiana. Kwa hiyo, ningeshauri Mfuko huu katika marekebisho yake usisitize umuhimu wa kwenda zaidi vijijini na *operations* zao zifanywe Wilayani na Halmashauri ziwezeshe kuweka mambo sawa katika vijiji kusudi wananchi walio wengi vijijini nao wapate kuwezeshe na kuingia katika mfumo wa kiuchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia na naunga mkono Muswada huu. (*Makofit*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kujadili Muswada huu muhimu ambao unazungumzia masuala ya umaskini. Nimeuangalia kwa makini nimeona kwamba hii ni *Part Two of PRS Two* na *PRS One*. Sasa ni utaratibu wa muundo wa Serikali iliyo makini katika nchi zote duniani kutoka Afghanistan mpaka Zimbabwe inaangalia nchi iliyopata uhuru wa siasa unafuata uhuru wa uchumi. Unapoomba Uhuru unadhani siasa ni uchumi.

Kwa hiyo, unapotengeneza uchumi si uchumi wa mtu mmoja mmoja au watu wachache kumiliki uchumi huo unakuwa ukoloni mamboleo (*Neo-Colonialism*). Kwa hiyo, nchi ikimilikiwa na uchumi wa watu walio wengi na kuwawezesha walio wengi kwa hiyo, inakuwa umejikomboa katika kujinasua mikononi mle. Nchi za Afrika duniani zilishindwa kufanya vile kwa sababu ya umaskini wake. Kwa hiyo, matokeo ni kwamba aidha, walikwepa kijiita wenyewe kusema kwanza mimi mwengine baadaye. Wakaogopa ili kuwavutia watu waweze kuwawekezea badala yake watu waliowekeza wakaanza kuzipuuza nchi hizo na kuanza kuonekana kwamba maskini vile ni watu ambao hawana kitu. Kumbe wanacho kitu chao wana raslimali zao za nchi zao. Matokeo nchi nyingi duniani katika nchi za Afrika zimesombwa maliasili zao katika sekta za uvuvi, madini na mambo mengine kwa hiyo basi, kukatokea uchumi wa mchupo kiasi kwamba kuna baadhi ya watu wanatumia makoleo kwa kujilisha Watanzania wanatumia vijiko vya kawaida. Huo ulikuwa utangulizi Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwenye Muswada nimefurahi sana kuondoa ile Bodi, kui-delete ile ibara ya 17. Ni kwamba baada ya hapo sasa inakuwa ni *numbered*. Kwa hiyo, sasa namba itakuwa sio 44 itakuwa 43 katika ibara hizo. Niliona kwa sababu hata ile bodi ilikuwa haina hata Mwenyekiti. Imejitokeza tu kama uyoga katika chupa. Kwa hiyo, nilikuwa nashukuru sana kuondoa pale.

Halafu nimesema hivi kwa nini hii isingekuwa *Executive Agency* ikianzia chini ya sheria hiyo. Kwa hiyo, kila kitu inatajwa vitu kama Serikali. Vitu vingine Serikali imekuwa inahodhi mambo mengi sana kwenye Muswada huu. Kwa sababu Serikali tunao Muswada unaohusu *Executive Agency* basi ingekuwa *Executive Agency*, Mfuko ujiendeshe wenyewe. Lakini nikaona kwa sababu Muswada huu unalenga kuunda Mfuko ambao wenyе mfumo wenyе maelekezo ya Waziri katika ibara ya 44 ambayo nitatoa maelekezo kwa kuelekeza *council*.

Kwa hiyo, hebu tuanzie hapo, matatizo yatakapotokea kwa sababu *jet* ikishaanza kutoka huwezi ukasema ningojе, tua sasa. Kuna wakati mmoja mchezaji mmoja wa *Simba Sports Club* alikuwa ameachwa sasa ikawa anapungia, anasema mimi nimechelewa samahani. Sasa ndege haiwezi ikatua tena. Sasa Muswada huu umeshaondoka tayari kwa hiyo, hatuwezi kupungia. Lakini kwa taratibu za Bunge tunaweza tukatoa hoja mahsuswi kwamba kwenye mapungufu katika utendaji tunaweza tukarekebisha baadhi ya mambo fulani fulani. (*Makofі*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kukwepa kuhusu baadhi ya maneno kwa ajili ya kuogopa. Hivi kweli tunaogopa kusema Tanzanian bila kusema *origin a Tanzanian*. Kwa sababu usije ukafanya *globalization* ukawa-globe watu halafu wakajiingiza Watanzania watakuwa nasaba. Kuna *Tanzanian by dissent* akajiingiza hapa, kuna Watanzania wa nasaba. Hapa anaangaliwa Mtanzania ambaye mnyonge ambaye ametajwa kwenye ibara kwenye maelekezo huko ndiyo huyo anazungumzwa na ndiyo maana Mawaziri wa Fedha, Kilimo, Viwanda na Biashara walizungumzia hayo kwenye hotuba zao mbalimbali za Bajeti kumwezesha Mtanzania wa kawaida. Hivi neno kawaida maana yake anaweza kuwa *by dissent* wa kawaida. Mtanzania wa Tanzania,

black ndio wa kawaida ambao walikuwa na uchumi *free* ama sivyo wanaweza watu wakajiingiza, wakajiita maneno ya kawaida, *is too global*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Muswada wenye kwa sababu mtu mmoja alikwenda kuangalia matokeo ya maeneo, matokeo yake akakataa sehemu nzuri kweli. Alikwenda wenye *guest* moja akawaambia naomba vyumba akaambiwa viro. Aina gani? Akasema tatu. *Double, Single* na *Self Contained*. Akasema naomba maelezo. Maelezo akapewa *single* ni kitanda kimoja, *double* vitanda viwili na *self contained* kila kitu hapo hapo. Sasa nataka hiyo *self contained*, kila kitu gani akasema kulala, kuoga na choo. Akasema hilo zizi sitaki. Kwa sababu kila kitu hapo hapo alikataa. Kumbe angekewenda kuangalia angeona mambo yale yalivyo mazuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kutoa *VIP treatment* kwa watu ambao wageni. Kwa kweli tumetunga sheria za uwekezaji hapa tukaweka masharti mepesi mno jinsi mwekezaji wa kutoka nje aliyeingia nchi yaani tumerahisisha mno mambo ambayo ya mgeni, lakini Mtanzania mwenye kwa masharti anayoyaona yanakuwa magumu kweli kweli.

Niliufananisha Muswada huu na Miswada mingine inayowazuia Watanzania na baba mmoja ambaye alikuwa anatoka kuoga anaingia chumbani kwenda kubadilisha nguo alibaki na taulo akaambiwa baba *Isidingo*. Kwa sababu *Isidingo* anaipenda basi akaamua akavaa shati akarudi pale sebuleni kuangalia *Isidingo*. *Isidingo* ni kipindi ambacho kina maajabu maajabu kidogo. Akatokea baba mmoja alikuwa hana nguo. Yule bwana akachukua taulo akaenda kuificha ile *TV* yeze akabaki vile vile. Aliona ahifadhi picha kuliko yeze mwenye heshima yake. Utaratibu huu sio mzuri. Zalisha Watanzania kwanza na wengine baadaye. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja katika nchi zilizoendelea duniani ambazo watu wake sasa hivi wanajua kwamba wamejikomboa kutoka katika mikono ya Wakoloni. Lakini sasa hivi Muswada huu hauleti raha wala karaha wala mustarehe. Unaweka sawa mgao wa mapato ili kuwawezesha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Watanzania wanawezeshwa kuna aina mbili. Kuna kumwezesha Mtanzania moja kwa moja unaambiwa Pato la Taifa linakua lakini uwe la uchumi jumla, lakini Pato la kila mtu linakuwa kwa kweli ni la hafifu. Fanya jaribio siku moja, itisha mkutano kwenye kijiji waulize Watanzania wenzako useme naomba shilingi 1,000/= utakuta wachache. Kwa kweli fedha inapatikana kwa kweli si rahisi kuingia mifukoni. Ikiingia rahisi kutoka. Kwa hiyo, hapo napo kuna mushkeli katika maendeleo ya kifedha kwamba inakuwa sio rahisi kuipata lakini ukiipata rahisi kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta hapo sio kuna mkono wa mtu lazima kuna matatizo katika uendeshaji wa uchumi. Kwa hiyo, Muswada huu utaweka sawa jinsi ya mgao, usimamizi wa fedha na mapato ya wananchi.

Lingine katika *institutions* nilizotaja katika ukurasa wa 6. Zimetajwa *organisation* pale zimeorodheshwa kama 11 lakini nikaona hakuna kitu kinaitwa *NGOs* sijui walijieleza vipi hapa. Halafu vile vile *definition* ya *Minister* najua kabisa kwamba *Minister*, kuna sehemu inasema *Minister charged with*. Sasa ama inakuwa *Minister dealing with* au *Minister charged with*. Sasa ndiyo hicho ambacho nilikuwa nafikiri Kiingereza bahati mbaya mimi sikuchukua *Linguistics* lakini ni Mkemia huwa najua *analysis*. Lakini *I am a word anamnesis*.

Lingine kuhusu kwenye *section 13*, ibara ya 12, kifungu kidogo cha 2 kuna neno limesema *may*. Pale sio *shall*. Sasa nilidhani kama itakuwa *May au Shall. Section 2* katika ukurasa 13.

Halafu lingine katika ukurasa wa 17 *definition* ya neno *Disadvantagehivi* ni watu gani hawa wanaelezwa. Kwa sababu kuna *section* kama walemavu au watu wengine wengine na watoto. Sasa hawa watoto watashiriki hapo au watoto wa mitaani kwa sababu ndio wanaokuwa *disadvantage*. Sasa *definition* ya hii imekuwa *too general reduced generation*.

Halafu lingine orodha iliyopewa katika vyanzo vyta mapato vyta Mfuko huu. Katika *regulation* za Waziri nadhani atapendekeza maeneo ambayo yalitajwa kwenye ibara ya 44. Ataelezea maeneo mahsus ikinsi ya kupata watu hao.

Lingine tunasema kabisa kwamba Muswada huu ni suala la jumla la uendeshaji tu lakini ni Wizara zinazohusika ni mtambuka. Ndiyo maana imewekwa chini ya Waziri Mkuu. Sasa hivi nilikuwa naangalia mahali pa kuuweka ilikuwa ni matatizo kidogo kwa sababu sekta mtambuka ningesema ni Wizara ya Viwanda na Biashara zimo *SIDO* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Vice President's Office*, kuna masuala ya mazingira na nini yote yameshirikishwa. Kwa sababu *Prime Minister* nadhani mfumo wa Mawaziri wa Wizara hizo na vile vile ni Waziri Mkuu wa Nchi na maeneo ya sera na hela sio kudra. Nimesema kabisa kwamba lazima hapa ni *quick fit super impossible and* vile vile ni *congruent* na katika kukaa mahali pale. *It is a same place na it is a safe place*.

Halafu mfano vile vile wa uchumi kuna mambo mengine ambayo visumbufu vyta uchumi vyta nchi hii. Muswada huu ukawawezesha Watanzania. Yako matukio mbalimbali yanatokea katika Halmashauri za Wilaya. Kutafuta utaratibu kuweka mgambo badala ya kulinda ulinzi wanafanya mgambo kunyang'anya wananchi ambao wanauza biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa wakati najadili hoja ya Waziri Mkuu niliwaambia kama kuna Wakuu wa Mikoa ambao wanapenda vurugu na kupenda kufukuzana na Watanzania nilitoa nafasi kwamba kuna jimbo kule Katanga liko wazi. Maeneo ambayo wanapenda vurugu na kupigana pigana kule. Kwa hiyo, *wa-apply* tu kwa Joseph Kabila wapate Mikoa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni watulivu, tumieni utaratibu wa kuwahamisha sio kunyang'anya yale mazao yao, unachukua mali zao, unasomba na hatujui zinapelekwa wapi. Kwa hiyo, naomba tafadhali kupitia njia hii Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wawapelekee majina ambayo watu wameporwa vitu vyao halafu maelezo yale yaletwe kabla ya kikao cha mwezi Aprili ili Bunge lichukue hatua kwa wale ambao waliochukuliwa vifaa vyao kwa sababu tunataka kuondoa umaskini mmejiandaa na mifuko mbalimbali. Serikali yenu imejitahidi kuunda mifuko na kuwakopesheni mkaandaa kufanya biashara ndogo ndogo katika miji hiyo lakini kuna baadhi ya visumbufu vya uchumi wanakuja kufanya vurugu bila utaratibu. Naomba kwa Muswada huu twende sambamba kuwaongoza Watanzania kwa ushauri zaidi sio kwa njia ya kupambana. Tusipambane na maskini tupambane na umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimesema kwamba Muswada huu sio Mfuko wa Maafa wala sio Mfuko wa kuzindua kwamba utatusaidia watu ambao waliopata na majanga. Ni mfuko ambao unaundwa kwa ajili ya uwezeshaji wa Tanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilidhani waliokuwa tayari na uwezo mzuri kwa hiyo wasitegemee hapa kwamba watapata chochote. Tumesema kabisa kuna sehemu inasema kabisa katika uundaji wa *Council* wanasema ni watu wazoefu. Wazoefu wa kufanya nini kwa sababu hawa wazoefu ndio waliokuwa wamewapa fedha hao tunaowalaumu hapa kwenye Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwe wazoefu wa kufanya mambo waliyozoea, wabadilike. Wabadilike kwa sababu katika mchango mara nyingi siku moja walikuwa wamechanga nguruwe, kuku na ng'ombe. Waliambiwa tuchange, nguruwe akatoa wazo akasema tuwachangie maskini. Akasema changa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchanga, kuku amesema anatoa mayai, ng'ombe akasema natoa maziwa na nguruwe akasema nimechangia wazo. Wakasema hapana wewe toa mishikaki. Nguruwe akasema nikitoa mishkaki nitakufa. Kwa hiyo, upo uwezo Watanzania wanachangia mawazo yakubalike. Naomba wazo hili liingizwe katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Baada ya mchango wa Mheshimiwa Semindu Pawa, sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka hapo saa 10.00 jioni. Sasa nasitisha shughuli za Bunge.

(*Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya awali mchana huu, nami ili niweze kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu. Kwanza kabisa natoa pongezi nyingi kwa Waziri wa Nchi kwa niaba ya Waziri Mkuu pamoja na Katibu Mkuu wake na watendaji wa Wizara hii kwa kuleta Muswada huu ambao mimi kidogo nimeuona kwamba ulikuwa umechelewa. Lakini bora uchelewe ila ufile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutanguliza nia ya kuunga mkono moja kwa moja toka mwanzo kwamba naunga mkono Muswada huu. Ingawaje maudhui yake yamechelewa mimi nakubaliana nayo vizuri kabisa. Pia nashukuru kusema kwamba wachangiaji wengi walijikita katika mambo mengi muhimu yanayohusiana na maendeleo katika nchi yetu. Leo hii asubuhi na kazi kubwa imefanyika na watalaamu walioleta Muswada huu na pia mawaidha mengi yamekwisha kutolewa na baadhi ya Wabunge ambao waliopata nafasi ya kuuzungumzia Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika mchango wangu nilitaka tu kusema kwamba Serikali itumie nafasi hii kuyawezesha makundi maalum ambayo kwa muda mrefu katika nchi hii yamekuwa yakishindwa ama kujikomboa kiuchumi au kujiendeleza vizuri. Makundi hayo nilitaka kuanzia na kundi la wastaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina watu waliostaafu wenyewe taaluma mbalimbali ambao wako vijijini. Ukitaka polisi wastaifu wapo, ukitaka wana sayansi wapo, ukitaka wachumi wapo, lakini wengi wao wanaiza kwa kutumia jembe la mkono ni baada ya kustaafu. Sasa mimi nilikuwa nafikiri kwamba mojawapo litakalofanywa na ile Sekretarieti ni kuwa na orodha ya wastaifu wote na kujua wanafanya nini ili waweze kuwezesherwa wao wenyewe kujikomboa kiuchumi na pia wawe nyenzo mojawapo ya kusaidia wenzao katika ukombozi huo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tuna mahali hasa pa kuanzia. Wastaifu wako wengi sana, hawana njia tu ya kuwezesherwa. (*Makofii*)

Halafu la pili, nafikiri ni wakati mzuri kwa kundi la akina mama kuwezesherwa. Akina mama wengi wanajishughulisha na shughuli mbalimbali huko vijijini. Lakini kwa bahati mbaya hawawezeshwi. Sasa hii ni njia mojawapo nzuri sana ya kuhakikisha kwamba tunawawezesha akina mama ili waweze kujikomboa si wao tu, bali hata watoto wao na vizazi vyao. Kwa hiyo, hili iwe ni mojawapo katika mikakati itakayowekwa na ile Sekretarieti. (*Makofii*)

Tatu, vijana ambao ndiyo vijana wetu tunao wategemea wengi wanajitahidi kufanya kazi za kimachinga. Sasa kazi hizi za kimachinga kama tunavyoju si za uzalishaji mali sana. Naamini kama utaratibu wa kuwawezesha hawa pia wanaweza kuwa ni nguvukazi nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba tunapigana na umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa lipo suala la uanzishaji wa huu Mfuko wa Uwezesheraji au taasisi yake. Hapa nilitaka tuwe makini sana, kwa sababu tumekuwa na mifuko mingi ya Kiserikali na isiyo ya Kiserikali ambayo kwa kweli mingi haiwasaidii sana wananchi. Tunayo mifuko mingi hasa ya mashirika au taasisi zisizo za Kiserikali.

Ukiangalia sana pamoja na maudhui yao ya kusaidia kuondoa umaskini utakuta mengi yao yanasadidhia zaidi mifuko ya wale walionacho kuliko kusaidia wananchi. Nilitaka kusema kwamba mfano mzuri wa kuigwa ni Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote unaoendeshwa na Mama Anna Mkapa. Mfuko huu walau unasadidhia sana makundi mbalimbali nchini ili kuhakikisha kwamba hawa wanaondokana na umaskini.

Kwa hiyo, tungekuwa na utaratibu mzuri wa mifuko ya aina hiyo, mimi naamini ingeweza kutusaidia katika kuondokana na umaskini. Umaskini huo huo katika nchi hii tunajua wala hatuna haja ya kutafuta wataalam au watu waliobobea kujua sehemu gani katika nchi hii zimekithiri kwa umaskini. Karibu mikoa yote ya pembezoni mwa Tanzania hali yao ya kipato na mambo mengine ni duni. Hata Mheshimiwa Rais, wakati akitoa hotuba yake hivi majuzi alisema kwamba wakati ambapo kuna baadhi ya mikoa, akatoa mifano, ina shule za sekondari zaidi ya 200, lakini kuna baadhi ya mikoa mingine kama Lindi ina shule za sekondari 19 tu. Sasa hapo iwe ni changamoto kwamba tunavyoanzisha mifuko ya namna hii na taratibu za namna hii tuhakikishe wale walio maskini zaidi wanalengwa na kufikiwa. Hii iwe ndiyo nafasi yao ya mwisho. Lakini kama ikiendelea miaka yote ilimradi anayeendesha mfuko ule anatoka maeneo fulani halafu miradi yote anapeleka katika maeneo ya kwake au karibu na kwake basi mfuko huu hautakuwa na maana yoyote. (*Makofi*)

Sisi tulikuwa tunataka tuwalenge zaidi hasa wale ambao hali zao kwa kweli ni taabani. Mimi naamini kabisa katika miaka kumi, ishirini ijayo tunaweza kuondoa huu umaskini wa kutupwa ili walau katika nchi yetu hali iwe inafanana fanana kidogo. Hizi tofauti tulizonazo kimikoa ni lazima ziondoke. Hizo tofauti hazitusaidii hata kidogo. Tunaoweza kuondoa sasa tumepewa fursa hii kwa ajili ya kuweza kuweka kila aina ya mipango ya kuhakikisha kwamba nafasi hiyo inapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kuzungumzia ni kwamba kuna baadhi ya maamuzi tunayofanya ambayo kwa kweli yanaumiza watu wetu. Kwa mfano, mimi kwetu ni wakulima wa korosho na ukichukua zao lile la korosho, lina faida kwa korosho yenyewe kwa kuitafuna na kadhalika. Lakini tunda lake linafaa sana kwa kutengeneza pombe. Kuna pombe za aina mbili, kuna pombe isiyolevyaa sana na kuna ile gongo inayotokana na mikorosho ambayo kwa kule inapendwa sana. Lakini haikupewa nafasi katika nchi hii kuendelezwa. Mimi nataka kusema kwamba ikiwa wenzetu wa *Scotland* hivi leo wana kijiji kinazalisha *John Walker* wengine wanazalisha *teachers*, kwa nini na sisi tusiwezeshe watu wetu ili kuhakikisha wanapika gongo ya sawa sawa? Gongo nzuri ambayo utajua kwamba hii inatoka Mwena na ile inatoka Chihugu na hiyo Chiwata, namna hiyo?

Watu wajue kwamba kwa kuleta teknolojia yaani kwa mfano katika ile *titillation* ukihakikisha kwamba ile *spirit* unaiondoa inayobaki inakuwa *alcohol* nzuri. Sasa fursa hii ya sasa iletwe kule ili tuhakikishe kwamba gongo linalopikwa linakuwa zuri kama *Brandy*, kama *Whisky* kama kitu chochote kingine kile, kwa sababu *raw materials* zipo. Tutake tusitake watakunywa ingawa leo tunakataza kwamba watu wasinywe gongo na kadhalika, wanakunywa kama nini na ile ndiyo wanayoitegemea zaidi kuliko bia na kadhalika. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa nini tusichukue nafasi hii kuhakikisha kwamba tunatengeneza gongo zuri la kisayansi lenye technolojia ya kisasa katika sehemu mbalimbali? Mfuko utengeneze mambo namna hiyo na wananchi wetu wataona kweli tumewakomboa kwa sababu kipato kitaenea kwa watu wengi, watu wengi ni mafundi wa kupika ile lakini hawana tu teknolojia. Sasa teknolojia ile sisi tunaweza kuileta na vifaa mbalimbali tunaweza kuileta ili kuhakikisha kwamba haya yanakuweko. Gongo bwana limepigwa vita toka enzi za mkoloni na wakoloni walikuwa wanalipiga vita kwa sababu walitakuza *Scorch Whisky* katika nchi hii. Sasa kwa nini sisi wenyewe tusiamke sasa kwamba kama wale walitaka kuuza hebu tutengeneza *ginnery* yetu na sisi?

Mimi nasemea ndiyo kipo Kiwanda cha Konyaji kule Dar es Salaam ni kizuri na kadhalika, lakini tuwe na viwanda vidogo vidogo kwenye vijiji wawe wana- *compete* na tuwe na *standards* za sawa sawa ili baadaye hii kitu isiharamishwe iwe ya halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi katika mchango nilikuwa nasema pesa hii itakayotoka mojawapo la kufanya ni kuwasaidia watu na tutawasaidia watu wengi siyo kwa mikoa ya Kusini tu lakini karibu nchi nzima tutawasaidia, huko Kigoma, Musoma kila mahali tutawasaidia. Kwa hiyo, naomba hili lifanyiwe mkakati maalum wa watalamu kuhakikisha kwamba hili linakuja kuwakomboa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tena kwamba naunga mkono hoja hii na nina uhakika kwamba tukipitisha Muswada huu utatusaidia mambo mengi sana ya maendeleo katika nchi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ISAAC M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ilio mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikikumbuka kule nyuma tulikuja na Azimio la Arusha na wananchi wengi wakaamini kwamba kwa kupitia Azimio la Arusha njia zote za uchumi zilikabidhiwa mikononi mwao. Ilikuwa ni shangwe mitaa yote, tangu kijijini kwangu Bariadi hadi Mtwara watu wote waliunga mkono Azimio la Arusha wakitumaini kwamba lilikuwa na malengo mazuri. Leo hii badala yake Azimio la Arusha kumetokea nini wote hatujui, isipokuwa matokeo yake ambayo watu wengi tunaweza tukakumbuka ni kwamba nchi imekuwa na matabaka ya wenyewe mali na wasio na mali na wengine wale amba walikuwa wanashangilia na kuunga mkono azimio wamebaki ni maskini na wako pale pale.

Sasa malengo yale yalikuwa ni mazuri kama ilikuwa kweli, ni kuwakabidhi njia zote za uchumi wananchi. Leo kumekuja na hii katika madhumuni yake imeandikwa pamoja na malengo na mikakati mizuri iliyowekwa ili kutoa fursa ya kuwawezesha Watanzania, kushiriki kwenye uchumi hali halisi imedhihirisha kwamba Watanzania wengi hawakunufaika na mikakati hiyo. Aidha ushiriki wao katika uzalishaji wa miradi mbalimbali binafsi na uzalishaji wa mali na shughuli za biashara, kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na kadhalika bado ni mdogo. Sasa ukisoma kitu kama hiki unaona kwamba sasa kumetokea nafasi ya Watanzania kupewa njia ya kuweza kujinasua na hali

hiyo ya umaskini ambapo *may be* watatumia *resources* zao walizo nazo ili kujiondosha katika ulingo wa umaskini.

Lakini tutafanyaje kama katika Azimio tulikuwa tume- *target* nchi nzima na hatukufika popote pale leo tunakuja na mfuko wa kuwawezesha Watanzania, waweze kujinasua katika umaskini? *Target* ni nini? Mimi nilikuwa nafikiria kwanza tungeweka katika makundi kwamba *target* iwe kwa wakulima. Mimi naamini kabisa mkulima kumwezesha kujinasua na matatizo ni kumhakikishikia kwanza bei ya mazao yake kama ni pamba imekuwa ni *stable* na kwamba wakati wowote hata kama imeshuka bei ya pamba Serikali iweze kumfidia yule mtu. Kumfidia ile tofauti ya pamba kushuka (bei yake) katika soko la dunia. Hiyo itakuwa ni *empowerment* kwa mkulima kama bei yake ya pamba itakuwa ni *stable*. Lakini pia yule mvuvi akiwa na uhakika kwamba anapovua samaki wake yule samaki ana soko na anaweza akaiza na akapata fedha, hiyo ni *empowerment* ambayo huhitaji kwenda kwenye benki kwenda kukopa wala kufanya nini, lakini akiwa na uhakika tu wa soko lake, mazao yake, itakuwa tumemsaidia.

Lakini *empowerment* nyininge ambayo ingekuwa ni *priority* ya kwanza ni elimu. Nakumbuka katika Azimio la Arusha Mwalimu Nyerere alisema fedha siyo msingi wa maendeleo. Alitaka watu (*ai-invest in brain*) watumie akili zao kuweza kujinasua na matatizo ya umaskini. Sasa mimi nasema *priority* ingekuwa *empowerment* kwa Watanzania wote muiweke katika elimu. Mtoto wa mkulima asome, mtu wa kawaida, mtu ambaye anakaa Ng'wasinasi, Ihusi, Nkindwabiye, Ikinabushu na *elsewhere* waweze kuwa na elimu ya darasa la kwanza mpaka darasa la 12 bure.

Hata kama ni *university* hawa waweze kufika kule mpaka Chuo Kikuu utapata watu wana *brain*, wana elimu hata ukiwakabidhi mradi wa aina yoyote ile wanawenza kuusimamia na kuufikisha pale ambapo watu wengine wanategemea kufika. Hata kule Korea walifanya hivi..

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyininge ya kufanya *empowerment* ni kazi bure kuzungumza juu ya kwamba tuna mfuko wa kwenda kukopa wakati mishahara ya watumishi bado duni. Mimi nilikuwa nafikiria njia ya kwanza ilikuwa ni *generally unempower* watumishi kwanza wawe na mshahara wa kutosha kutoka Jumatatu ya mwanzo wa mwezi mpaka Jumatatu ya mwisho wa mwezi, akawa na hela ya kutosha kulipia chakula chake, kulipia pango, kulipia umeme, kulipia nauli ya kutoka nyumbani mpaka kazini kwake na bado abaki na fedha ya kutosha kuweka kama akiba.

Sasa katika hali ya sasa hakuna *empowerment* ya aina yoyote kwa wafanyakazi. Wafanyakazi wana mishahara midogo kiasi kwamba nauli peke yake ya kumpeleka kazini kwa mwezi mzima ni zaidi ya mara mbili ya mshahara wake. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria kwamba jambo la msingi tungeanzia hapo tukawapa vitu ambavyo ni *basic* wakulima, wasomi na watu wengine wakawa na uwezo wa kuwfikisha mwisho wa mwezi na *ku-make a bit of saving. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu jinsi unavyozungumzwa mimi unanitia mashaka makubwa sana kwa sababu *sources* za *revenues* zilizotajwa hazinipi imani

kwamba tuna dhamira kabisa kutoka Serikalini ya kuweza kuwa na pesa ya kutosha kuja kuwakopesha wale ambao watakuwa wanahitaji. Inanipa pia woga kwamba unafanana na mfuko ule ule kama wa NSSF, PPF ambapo hata wale watumishi tu wa Serikali na mashirika ya umma hawana *accessibility* ya kuweza kupata mkopo, isipokuwa watu wenye majina, naogopa kusema. Siku moja rafiki yangu alikwenda akakopa shilingi milioni 50 kwa ajili ya Ranch yake. Lakini mtu wa kawaida tu kama mkulima ama mchangiaji wa (mfuko ule) wa kawaida hana *access* hata kidogo hata kule kufika kwenye mlango wa PPF na kuomba milioni 20 ili na yeze aweze kujinunulia trekta ndogo.

Sasa na huu mfuko unanielekeza huko huko kufikiria kwamba ni watu wa aina fulani tu wenye uwezo wa kisiasa, wenye majina. Lakini si ajabu ni Wahindi na Mabaniani ndiyo wanaweza kunufaika zaidi kuliko Mtanzania wa kawaida tu ambaye anatoka Bariadi ambako kweli anahitaji na yeze hata mkopo mdogo wa kuweza kununua trekta la miguu mitatu aweze kufanya palizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hali ya nchi tuna madini. Mara nyingi sana tumepiga kelele ndani ya Bunge hili tukizungumza juu ya madini ya Bulyanhulu, Kahama na yote ile dhahabu iliyoko pale Kahama ni *100% owned* na wageni, 100% kwanza ilikuwa *owned* na Saton ikauzwa kwenye masoko ya Toronto, ikahamia kwa Barrick (watu wengine) na leo sasa imeshauzwa tena Resolute lakini 100% ya fedha yote inayopatikana pale inatoka inakwenda nje.

Lilikuwa ni jambo la busara kwamba labda hata tungeweza kufikiria tu achana na asilimia tatu ambayo tunapata kwenye dhahabu kama mrabaha iende kwa Serikali. Tulikuwa tunafikiria labda *tunge-impose* sheria kwamba haya machimbo yote *Kahama Gold Mine, Geita Gold Mine, The East African Mine* na zingine zote ambazo ziko Mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora na sehemu zingine zote *at least 10%* ya *turnover* yao yote iende katika mfuko huu ili uweze kupata fedha ya kutosha kuwasaidia Watanzania wote. Lakini katika hali mimi ninavyoiona ni yale yale ambayo siku moja rafiki yangu wa Shinyanga alitaka wapate hela tu kama asilimia 2 ya kutoka Mwadui. Serikali ikasema ni *criminal* ukifikiria jambo la namna hiyo. Mimi nafikiria *attitude* ya namna hiyo haitufikishi popote pale Watanzania.

Sasa umefika wakati ambapo *tuna-impose* sheria kwamba *resources* zote tulizonazo wote wachangie katika mfuko huu ambapo Mtanzania mwengine anawenza akaenda pale akakopa hela yoyote akawenza kununua kama ni trekta, kama ni basi, na kadhalika ilimradi iweze kumsaidia katika kujinasua na dimbwi hili la umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nashukuru ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kupewa nafasi hii kwa siku ya kwanza leo kuzungumza katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Muswada huu uliopo mbele yetu.

Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia katika mfungo wa mwezi wetu Mtukufu wa Ramadhan na Waislamu wote wanaofunga na wale wote wasio Waislam na

wasiofunga watujalie heri na salama na afya na hasa watu wangu wa Jimbo la Mikunguni na Watanzania wote kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Muswada kwa kweli ni muhimu sana kwa nchi kama Wabunge wenzangu wote walivyotangulia kusema. Mimi mwenyewe binafsi nimekuwa nikifikiria siku nyingi sana kuwepo na kitu kama hiki na imenifanya hivyo kwa sababu kama mnavyojua mimi ni mjumbe wa *council* kule *SUA* na vile vile ni chuo changu ambacho nilisoma kule. Lakini utaona kwamba kuna wanafunzi wanaomaliza kusoma kwa mfano wale wanaosomea mifugo na huku utakuta kuna *Ranch* zetu tunazigawa, tungeweza kuchukua wanafunzi fulani waliosomea mambo ya mifugo, *management*, mambo ya *pasture* wakapewa *ranch* wakaendelezwa na wakapewa mfuko. Sasa ilikuwa kichwani siku zote nilikuwa nafikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Muswada huu umekuja, nadhani hayo ni moja kati ya ambayo nilikuwa naota. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri moja katika tafsiri hizi za *economic activities* ni tafsiri ambayo imewekwa kwamba ni *organization, institution*, hata mtu binafsi nadhani yumo. Ni moja katika *organization* ambayo imetajwa katika tafsiri ya Muswada huu. Kwa hiyo, ina maana vyote hivi *institutions, organizations*, hata mtu binafsi anaweza kusaidiwa katika Muswada huu. Kwa hiyo, hilo tunafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Muswada huu *una -address economic inequality*, nadhani imezungumzwa humu. Kwa hiyo, ipewe umuhimu sana. Wale waliokuwa nacho tena jamani hapa watusamehe, wapewe wale ambao tunataka kuwanyanya kiuchumi. Kwa hiyo, naomba katika utekelezaji lizingatiwe sana na ile *council* itakayokuja izingatie sana jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nijielekeze sasa kwenye Muswada wenyewe. Kwanza, kwenye *composition* ya *council*, kwenye ibara ya 7 (1) (e) inasema kwamba *chairman* atakuwa anateuliwa na Rais sawa. Lakini kwenye 7 (b) wamesema kwamba kuna *maximum* ya wajumbe 8 ambao watateuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ningeomba kwamba ingeongezwa hapo katika hao 8 basi *at least* 3 wangekuwa wanawake, ingetajwa, najua pengine watakuwepo lakini ingetajwa, kila siku tuna *address* hata Bunge tunasema wanawake wawe *one third*. Kwa hiyo na hii si vibaya kwamba katika hawa 8 *at least* wakawa wanawake! Wanaweza kuongezeka! nashukuru kuwa watu wamenisikia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, labda kwenye 7 (2), nadhani kuna matatizo ya sarufi kidogo katika uchapaji. Kwa mfano kwenye *line* ya tatu, *senior officials who possesses* nadhani ingekuwa ile *singular ikaonyeshwa who possess, proven experience in trade, agriculture* halafu *imeandikwa industrial* halafu na *finance*. *Industrial* nadhani inakuwa ni kama si *noun* huku umetajwa *noun* na hapa *noun* kwa hiyo, nadhani hapa kuna makosa ya kisarufi, naomba hapa parekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye ibara ya 10 (6) (e) na (b), Muswada umeeleza kwamba katika hawa watu wa *council* hata ule wakiwa katika *session* yao lakini ikiwa kuna mtu *ame-declare interest* yajambo lile ambalo linazungumzwa inabidi yule atolewe nje na lile jambo ambalo yeze *ana-declare interest* lizungumzwe *in his absence*, hiyo ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wamesema kwamba jambo lile likiamuliwa, wanawenza *ku-consider* kama *quorum* imetimia, pengine wako 4 au 5 au 4 na *chairman* sasa pengine mmoja wao *ame-declare interest* amewekwa nje itabidi wajumbe watatu ndiyo *wana-discuss* ile pamoja na *chairman*. Kwa kweli nadhani itakuwa *quorum* kidogo hapa haikutimia.

Lakini baada ya *discussion* na uamuzi wa jambo lile yule mtu akirejeshwa ndani inakuwa *quorum* imetimia, kwa hiyo, mimi nahisi kwamba hapa kifungu (b) *ku-stand* kwamba *quorum* imetimia kwa sababu hapa anapoondoshwa kuna wajumbe watatu na *chairman*. Pale *quorum* haikutimia kwa sababu linapozungumzwa jambo lile ambalo yeze ana *interest* nalo yuko nje. Lakini likishaamuliwa yule mtu anarejeshwa ndani katika kikao ambayo *quorum* imetimia na uamuzi ule anaambiwa na bila shaka anaukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ina maana inakuwa hapa uamuzi ule umekubalika na *quorum* imetimia. Kwa hiyo, katika vifungu hivi mimi nahisi kifungu (b) tuisimame tuwe na msimamo kuwa kifungu (b) kichukuliwe kwamba *quorum* imetimia wakati ule na jambo lile liwe limepitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 28, hapa amesema kwamba kama mtu ameomba na ameleta maombi yake kwa Sekretarieti wa *Council* anapokuwa satisfied na maombi yale, yule mtu anakuwa *registered*. Lakini kwa mfano mkulima wa Kahawa, nilipokuwa Kijiji cha Lundu huko Mbinga kwa wakwe zangu, mwingine yuko pengine Nzega au Mbeya, analeta *application* yake na pengine *Council* itakuwa Dar es Salaam tu. Je, *Secretary* atahakikisha vipi huyu mtu huko aliko? Unajua nchi hii sasa hivi tuna watu wengine wengi ambao ni wageni sio raia. Pengine yule asiye raia akisikia anawenza kuleta maombi. Je, *Secretary* atahakikisha vipi au mtandao wa hii *Council* uko vipi katika Mikoa ili kuhakikisha yule anayeomba *application* yake itakuwa *considered* itakuja kwa wakati na atajulikana kama huyu ni genuine na huyu sio *genuine*. Vipi na hii *Council* haikuonyesha mtandao wowote katika nchi? Kwa hiyo, kwa hilo, nina wasiwasi kama haya mambo yatakwenda kama inavyotakiwa. Pengine watajaza watu wa Dar es Salaam tu. Au mtueleze vipi mtu kama huyu anawenza kuwa *Secretary* akam-satisfy kwa maombi yake tu.

Lakini hata ile karatasi ya maombi ukiona kwenye *schedule one*, anayeleta tu jina, sijui akina Shangani, mko wapi, watu wangapi saini. Sasa hakuna mtu kule ambaye huyo *applicant* anamwelewa, akakaa naye akatia saini yake kusema huyu kweli namjua ni hivi kweli. Hakuna! Kwa hiyo, inakuja kwa *Secretary* moja kwa moja. Sasa hili jambo kidogo linanitia wasiwasi, inaweza kuwa pengine hapa mambo yakaenda visivyo.

Vile vile nadhani ingekuwa vizuri japo ikatajwa tu kwa kiasi fulani au muda, kwa mfano mtu analeta *application* yake, muda gani utachukua mpaka kuwa anapewa hizi *facilities* ama ikiwa pesa au elimu au kitu kingine chochote cha kumsaidia ku-*empower* katika shughuli zake za kiuchumi. Haukutajwa muda, inaweza kuwa hata mwaka na unajua *activities* nyingine zinakwenda kwa *time* au kwa *season*. Kwa mfano *activities* za kilimo zinakwenda kwa *season*, hata za kiatalii unajua kuna season gani Watalii wanakuja. Kwa hiyo, anaweza kupeleka *application* yake ikafika hata mwaka na pengine kama mtu yuko Ukerewe huko afunge safari kuja kusikiliza *application* yake Dar es Salaam inakuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, nadhani ilikuwa ni vizuri tukazungumza kwamba baada ya kuwa amepeleka ile *application* yake, muda gani upite ili apewe zile fursa za kufanya shughuli zake za kiuchumi. Nadhani hiyo ingeweza kusaidia kuwasukuma Watendaji kufanya haraka haraka ili mtu apate majibu yake kwa yale aliyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *paragraph* iliyokuwa 35 lakini katika hii *amendment* iko *paragraph* ya 31 imesema kwamba: “*Any registered institution organization shall have the duty to prepare and submit performance reports of its economic activities and programs.*” Mimi nadhani hapa *suggestion* yangu ni hivi, kwanza (a) ingelikuwa hiyo *institutional organization to prepare and submit program of its economic activities* kwanza. Baada ya kuonekana pale, halafu baadaye ndiyo inaleta *prepare and submit performance reports of its economic activities*. Huwezi kufanya *program* halafu ukaprepare wakati huo huo pamoja *performance of economic activities*. Inatakiwa unaleta *program* yako na *schedule* yako ya mambo yako, unaangalia unapewa mfuko wako halafu baadaye unakuja kuleta *performance report*. Nadhani hiki kifungu cha (a) kiwe na (a) na (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kwamba mimi sikuelewa. Hapa tunasema kwamba hawa watu wanasaidiwa, inaweza kuwa kwa kupewa elimu, taaluma, inayoweza kukupa mfuko ili kuendesha *economic activities* zake na kukuza. Lakini *mode* ya ulipaji sikuiona. Inaweza kuwa pengine katika hizo *schedule* ambazo Waziri atazifanya au *Council* itatoa labda pengine itakuwa imo humo, lakini kama ni sheria ilikuwa vizuri iwe *mentioned*. Lakini je, wanapewa bure hizi pesa za elimu wanawenza wakapewa bure, *okay*; mwongozo ukawapa bure; lakini je, kama wanapewa pesa hakuna kulipa, haimo humu. Au ndiyo mpaka *Council* itoe sababu, bwana we utalipa hivi, lakini ilikuwa lazima angalau iwe *mentioned* kwenye sheria. Kwa hiyo, naomba kwamba hapo izingatiwe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache hayo naunga mkono hoja hii, lakini naomba hayo marekebisho yazingatiwe kwa manufaa ya Watanzania ambao wamelengwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu kwa uchumi wa Tanzania na wananchi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia Muswada wenyewe, nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Taifa wa Uwezeshaji kiuchumi wakati huu ambapo wananchi wengi wanaonyesha kuwa na ari ya kuleta maendeleo na hasa kujiondolea umasikini ambao umekithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakuja baada ya huko nyuma kuwa na mikakati mbalimbali na sera mbalimbali ambazo zililenga suala zima la kuwezesha wananchi kiuchumi. Hata hivyo, pamoja na mikakati hiyo yote na sera hizo zote, wananchi walio wengi wamejikuta wakiwa nyuma kiuchumi licha ya nchi yetu hii kuwa na raslimali za kutosha kulinganisha na nchi nyingine ambazo ziko mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaonekana na unategemea kuondoa kasoro za huko nyuma ili kuleta yale yote yaliyokusudiwa. Hivyo, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ibara ya 1(1), inaeleza jina la Muswada kwa kifupi kama Muswada wa Uwezeshaji wa Taifa 2004. Lakini kwenye madhumuni na sababu ukurasa wa 28 tunaelezwa kuwa Muswada huu unatoa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji ya Mwaka 2003. Je, Sheria itakayotokana na Muswada huu itakuwa ya 2003 au 2004? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu uanzishwaji wa Baraza la Uwezeshaji wa Kiuchumi. Baadhi ya kazi za Baraza hilo ni kutoa mikopo ya fedha kwa watu binafsi, Kampuni, Shirika, Chama au Taasisi kwa dhamana au bila dhamana kulingana na masharti ya marejesho kama yatakavyoamuliwa na Baraza. Je, kwa watu binafsi hasa wa Vijijini kutakuwa na taratibu ambazo ni rahisi na tofauti na zile zitakazotumika kwa Kampuni au Shirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na taratibu ambazo zitawafanya wananchi walio wengi kunufaika na utaratibu huu, kutafanya lengo kuu la kumwezesha mwananchi kujikwamua na umasikini lishindwe kabisa. Hivyo, hadithi kujirudia ile ile ya miaka ya nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ibara ya sita kuna *option* ya (a) na (b), pale kunapotokea kukosa *quorum* baada ya Mjumbe ambaye ana *interest* kujitoa. Mwenzangu Dr. Omar ameligusia hili, lakini mimi naomba *option* (a) ndiyo itawale na ile ya (b) iondolewe kwani inaweza ikaruhusu Wajumbe wachache wakafanya maamuzi kwa faida yao binafsi badala ya Umma. Siku zote lazima kuwepo *quorum* ya kutosha ili kufanya maamuzi ya Baraza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ibara ya 18(c) neno la kwanza “*proving*” halileti maana nzuri. Pengine neno *providing* badala ya “*proving*” lingeleta maana nzuri zaidi. Kwa hiyo, ningombaa neno hilo likaangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inahusu usajili wa Taasisi na Vyama vinavyojihusika na shughuli za kiuchumi. Je, kwa wakulima wadogo wadogo Vijijini na Wafanyabiashara wadogo wadogo kote Mijini na Vijijini, nao wanatakiwa kujisajili

kulingana na Muswada huu? Kama ndiyo, je, gharama za usajili zitakuwa zile ambazo wananchi wengi watazimudu? Uzoefu unaonyesha jinsi wananchi wengi wanavyoshindwa kujisajili kwa kukosa utaalamu wa kuandika miradi na kulipia gharama zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye uwezeshaji kiuchumi katika Sekta ya Kilimo ambayo ni muhimu sana kwa wananchi walio wengi hasa wa Vijiji. Mara kadhaa nimetolea mfano mkulima wa zao la Korosho ambalo ni maarufu sana katika Mikoa ya Mwambao mwa Bahari ya Hindi hapa Tanzania. Mkulima wa Korosho anahitaji kuwezesha ili aweze kuboresha zao hilo kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, kupalilia mashamba yake vizuri; lakini vile vile kwa wakati. Ili kufanikisha hili anahitaji fedha za kuweza kununua matrekta kwa wale ambaao wana mashamba makubwa, lakini vile vile wengine wanahitaji fedha kwa ajili ya kukodi matrekta na kuajiri vibarua kwa wale ambaao wana mashamba madogo.

Vile vile, mkulima huyu anahitaji fedha za kununua madawa ya kuua wadudu na viuutilifu ambavyo vinasumbua Korosho. Lakini vile vile, mkulima huyu anahitaji kununua mashine za kupulizia madawa mikorosho yake na vile vile anahitaji kuwezesha mkulima huyu kuokota korosho zote ambazo zinaanguka kwa wakati, hivyo kuhitaji vibarua wa kutosha ambaao anaweza akawalipa. Aidha, mkulima wa Korosho anahitaji vibarua wa kusomba Korosho kutoka mashambani kwenda nyumbani, lakini vile vile kutoka nyumbani kwenda sokoni.

Lingine la muhimu ni ulinzi wa mashamba ya mikorosho. Hivi sasa wakulima wa Korosho wanahitaji kulinda mashamba yao. Sasa pale ambapo mkulima ana mashamba mengi, inabidi aajiri wafanyakazi wa kulinda mashamba hayo. Bila hivyo kwa kweli hawezি akaambulia chochote. Kwa bahati mbaya shughuli zote hizi zinafanyika kabla mkulima hajauza korosho. Kwa hiyo, huhitaji kuwezesha ili shughuli hizi ziweze kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kutamka huko nyuma kuwa Masasi peke yake kuna mikorosho inayokaribia milioni tano. Mkorosho ambaao umetunzwa vizuri kwa haya ambayo nimeyaeleza hapa, mkorosho mmoja unaweza ukatoa kilo 50. Kwa hiyo, kwa mikorosho milioni tano Masasi peke yake ingeweza kupata kilo zaidi ya milioni 250. Kwa bei ya korosho ya sasa hivi ya Sh.750/= kwa kilo moja, nina hakika kiasi hiki cha Korosho kingeweza kuongeza pato kubwa kwa wananchi wa Masasi, lakini vile vile kwa Serikali yenyewe kutokana na ushuru na kodi mbalimbali zinazotokana na zao la Korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kusikitisha ni kwamba kwa kipindi chote hiki msaada wa Serikali kwa wakulima wa Korosho haujaonekana. Pamoja na kutambua kuwa mahitaji yote haya yapo, lakini Serikali haijamsaidia mkulima wa Korosho ili aongeze pato lake kutokana na kuongezeka kwa zao la Korosho na vile vile Serikali

yenewe kuongeza pato kutokana na kodi na ushuru mbalimbali ambao unalipwa kutokana na zao la Korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Muswada huu uone hazina tuliyonayo katika zao kama la Korosho katika kukuza uchumi wa Tanzania na mamilioni ya wananchi nchini kwa kuwawezesha kifedha. Nina hakika kwa kufanya hivyo, wananchi wengi ambao wanalima korosho, sio Masasi peke yake, lakini nchi nzima wanawenza wakafaidika na wakaondokana na umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba nirudie kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, lakini vile vile nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuongelea Muswada ambao nafikiri ni Muswada muhimu sana kwa Taifa hili, Muswada ambao kama ukitengenezwa vizuri na ukitekelezwa vizuri utakuwa ni mkombozi wa Mtanzania maskini katika Taifa hili. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuleta Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mwangi tumekuwa tunazungumzia sana juu ya umasikini ambao umekithiri katika Taifa hili na maneno ambayo tumekuwa tunajumia, naomba *ni-quote* jinsi yalivyoandikwa kwa Kiingereza. Niseme hivi; Maneno yenewe yanasema: “*Our poverty is not only a condition of low income and lack of assets; it is a condition of an ability exclusion and powerlessness. It is the erosion of our capability to be free from fear and hunger.*”

Sasa ambacho tumekuwa tunakifanya imekuwa ni kufuata utaratibu uliotufanya tuanzishe Mpango wa Kuondoa Umasikini katika nchi. Sasa ninataka kuangalia huu Mpango wa Kuondoa Umaskini jinsi unavyofanana na huu Mpango wa Uwezeshaji ambao tunauzungumzia hivi sasa. Ule Mpango wa Kuondoa Umaskini unasema, *nita-quote* pia kwa Kiingereza. Unasema: “*Poverty reduction is about enabling poor women and men to transform their lives and livelihoods and supporting government and civil society in creating and maintaining the conditions that allow them to do so.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukiweza kuondoa yale maneno ukaweka maneno “*economic empowerment*” ukayatumia yale yale kwamba “*it is about enabling poor women and men to transform their lives and livelihood*”, utapata maana nzuri ya mambo yanavyokwenda. (*Makofi*)

Sasa ukurasa wa nne, anasema hivi kwenye *preamble*. “*And whereas the Government has resolved to take measures designed to promote and facilitate economic initiatives aimed at empowering Tanzanians;*”

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata maswali. Maswali yangu ni kama yafuatayo:- Je, mikakati ya kumkomboa Mtanzania kiuchumi iko wapi ndani ya

Muswada huu? Je, hizi juhudzi za kiuchumi zitakuwa *facilitated* namna gani? Maazimio ya kumkomboa Mtanzania lazima yawe ya makusudi kabisa na yaelekeze nguvu halisi za kumkomboa huyu Mtanzania *of African Origin* ndiyo nataka kuzungumzia, ambao ndio wamekuwa *historically disadvantaged* kama Muswada unavyosema. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa kama hivi ndivyo, ndani ya Muswada tunapata kigugumizi kusema yale maneno tunayotaka kuyatumia, tunatumia maneno Tanzanians, lakini hapo kwenye kwenye kifungu hicho tunatumia *historically disadvantaged*. Mambo yanayofuata ndani ya Muswada na ambayo yameelezwa mle ndani yanakuwa ni mambo ya jumla jumla. Kama muda ungekuwepo nikauchambua Muswada wenyewe vizuri ndiyo ungeona ya kwamba huu Muswada una mambo ya jumla jumla.

Sasa swalii lingine linalofuata ni je, ni Mtanzania yeoyote? Maana tunasema Tanzanians! Ni Mtanzania yeoyote, au huyu Mtanzania *of African Origin*? Maana hamtaki tuseme uzawa, lakini ni mzawa kusema kweli. Ni mzawa, mimi napenda nilitumie hilo neno. Neno linalofuata pale linasema: “*And whereas economic empowerment is a central means for bringing about economic growth and social justice among our people that is necessary for the promotional peace, tranquility and social stability that has characterized our society.*” (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ni mazuri kama yangeambatana na mikakati mizuri ambayo itaweza kutuletea ukombozi ambao tunauhitaji katika hili. Lakini neno linalofuata pale, kifungu kinachofuata pale kinasema: “*Now, therefore, with a view to promoting rapid economic growth that will facilitate broader economic ownership (“economic ownership”, (I stress), by Tanzanians deliberate measures are taken to establish structures and mechanism to redress the existing economic inequalities among various sections of the population.”*

Maswali mawili yanakuja: *Structures ziko wapi? Where are the structures? Mechanism gani itatumika; ni hii ya ku-open up a fund? Is that the mechanism that is enough* kutoondolea huo umasikini na huko kubaki nyuma kiuchumi ambako tumekuwa nako? Hapana, lazima tuje na mikakati mizuri zaidi ya kumkomboa huyu Mtanzania kiuchumi. Nafikiri Muswada huu lazima umuangalie mkulima katika Taifa hili na mimi nitawaambia wenzetu wanasesmaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matatizo, nimevunja miwani yangu kwa hiyo mtanisamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Malaysia, wanasesma hivi: “*Malaysia practices the system of Parliamentary democracy with Constitutional Monarchy and his royal highness is a paramount ruler. It has three chambers of administration namely the Legislation, Judiciary and Executive.*” Hiyo tunafanana na wao. Lakini wanasesma, *Malaysia is a multiethnic country. The principle ethnic groups are Malays followed by Chinese and Indians. Other significant groups are the indigenous people of Saravok, Sabar including the diacs, cadenzas, bijous, maranous and muruts na wanawataja.*

Lakini moja zuri ninalotaka kulitaja hapa wale Malaysia hawaogopi kusema tunataka kuwakomboa wale indigenous Malaysia walipokuwa wanatengeneza sera yao. Hawaogopi kulisema hilo kwamba tunataka kuwakomboa wale *indigenous Malaysia*, wanalisema wazi wazi. Lakini sisi tunaogopa. Sasa *Tanzanians* watakuwa wote! Sasa wote itakuwaje? (*Makofi*)

Moja ya mambo ambayo lazima tuelewe ni kwamba katika sera ya kuondoa umaskini, ile sera yenyewe, *the poor did not make sense to the IMF nor to the World Bank*. Mtu maskini did not make sense na sera ya umasikini haikuwa sera ya haya Mashirika, *it was not*. Kama haikuwa, sisi wenyewe lazima tuendelee kusaidia sasa na kusaidia kwetu ni kuja na inputs zetu. Watu wetu ni maskini! Leo tunasema hii sera imeongeza kukua kwa uchumi; sisi tunasema, Wabunge wengi nimekuwa nikiwasikiliza wanasema bado uchumi haukukua kama tunavyotarajia.

Lakini mimi juzi niliona niwaambie wenyewe, nikawaambia this economy, hizi sera za *IMF* na *World Bank* zina-serve 20% ya population if it is anything to go by. Lakini 80% they are excluded socially na huu utaratibu wa Mipango ya Kuondoa Umaskini. Haiwagusi! Kwa sababu hii mipango haiwagusi, haiwezekani uchumi wetu uwe umekuwa mpaka kufikia huko.

Sasa ukiuliza kwenye Serikali, tunachoambiwa ni kwamba kwako bwana hakuna barabara. Kama mimi kule kwangu Kasulu, hakuna barabara, hizo benefit za growth haziwezi kufika na kule haiwezekani uchumi ukakua. *There are enough!* Lakini ni kwamba hizi sera zinamgusa mtu wa Mjini tu, hazimgusi mtu wa Kijiji ambaye hafikiwi huko. Haya ndiyo tungeyazungumza kwamba huko kuna matatizo na kwa kuwa kuna matatizo, hii sera lazima ilenge hao Watanzania ambao ni wazawa na ndio wanaoishi huko. Hakuna Mhindi anayeishi huko wala hakuna Mzungu anayeishi huko. Mimi siwi mkabilia kwa kulisema hili. (*Makofi*)

Nilikuwa Executive Director wa Chamber na moja niliyowaambia na Waheshimiwa wako wengi wanaonifahamu nilipokuwa kule, *if I was one of them it is my another problem*. Niliwaambia kwamba tunawasakiwa wale ambao ni disadvantaged na ambao hawakupata nafasi ya access katika haya. Kwa hiyo, ukija na mkakati wa kuanzisha haya lazima uje na mkakati ambao unawalenga hao na unawagusa hao na tuyatumie yale maneno. Hii siasa itatumaliza, maana tutashindwa kuwashudumia watu wetu kwa woga. Maana kivuli kiko nyuma kisha tunaogopa kile kivuli kiko nyuma, huyo tunayemsaidia hatutaki kusema huyo ndiye tunamsaidia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena, mimi nilikuwa Malaysia wiki mbili tatu zilizopita na nilikwenda kujifunza. Kwa hiyo, nikizungumza nikatoa mifano ya Malaysia naomba mnisamehe sana, lakini ni mifano halisi. Ile nchi wamekwenda mbali wenzetu wala sio mchezo. Sasa wao wana planning mechanism ambayo ni nzuri sana. Hapa hatuzungumzii planning, lakini ninachotaka kusema ni kwamba focus yao kwenye kilimo katika utaratibu wao ni kubwa sana.

Sasa nitawasomea wanayoyafanya kwenye kilimo. Wanasema hivi, kazi yao kubwa kwenye kilimo ni ku-review existing a formulating new policies and strategies for the optimum utilization resources to ensure higher contribution by the sectors towards growth and sustainable development. Moja hilo.

Hizi resources sisi tunazo nyingi. Tunayo madini, tunao wachimbaji wadogo, tunao watu kadhaa, tuna kilimo, wako watu asilimia 90 wako huko na ndio wanaoilisha nchi hii. Lakini tunasema kilimo ni uti wa mgongo, hatuwasaki huko. Tunatakiwa tutengeneze mikakati ambayo itakwenda huko ili iwe ndiyo *focal point* ya maendeleo ya Taifa hili na uchumi uanzie huko. Kama uchumi haukuanzia kwenye kilimo, kazi zote hizi tunazofanya ni bure.

Mambo mengine yatafuata, kama ni uvuvi utafuata, kama ni nini itafuata. Kilimo sustains nchi hii kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, mengine kama tunayasema, tunaweza tukasema tu tukajifurahisha, lakini nasema kilimo ni jambo kubwa. (*Makofi*)

Ukurasa wa saba pale ameandika: “*Institutions organizations supporting economic empowerment.* Zimetajwa nyingi, lakini nyingi zile mimi ukiniuliza nyingine sizifahamu.

Kuna *Rural Electrification Fund* hata sijui kama unapenda hata tano. Kuna *Agricultural Finance Bank* mimi sijui. Kuna *Tanzania Credit Agency*, ninafikiri hii ni selective inafanya kazi ya kuwa-select people. Inafanyiwa *development institute, marketing development center*. Zote hizi zinajulikana na wala hawajulikani kama wana-finance. Huwezi kufanya kitu kama huna uwezo.

Ile fund, ndiyo tunataka itumike vizuri tu. Kama ni utaratibu wa *training, training* ziko nyingi, Wabunge wengi hapa tumesoma. Lakini haimahanishi tuko *economic* mbalimbali. Naomba kila Mbunge anijibu aseme yeye ni *economically* kwa kuwa amesoma. Lakini kusoma lazima kuambatane na haya ambayo yametengwa. Tunazungumzia habari za *foreign investment* yaliyokuja hapa. Tunataka *foreigners* wakija hapa waambiwe mnakuja, mkashirikiane na Mtanzania fulani, Mheshimiwa Mzindakaya mtashirikiana naye. Ameyasema vizuri sana Mheshimiwa Mzindakaya. (*Makofi*)

Kwenye mining ni hivyo hivyo. Sisi tunaambiwa hatustahili tena kuitwa, *a poor country, why?* Kwa sababu maana Kenya inatuzidi kidogo. Wanasema hawa wana madini, wana kila kitu, *but what is the gaining? The significance is the gain.* Ndiyo tunataka. Hii *significance gain* hii ndiyo tunayoitaka, ambayo ingeingia kwenye uchumi wetu na kama ingeingia sisi tungkuwa mbali, tungepiga hatua, na umaskini tungeuondo. (*Makofi*)

Nilishashauri Bunge hili kwamba tuanzishe *a small mining development center*, kisha hii *development center* iwe supported by a special fund ya mining, that was not established. Na hii ndiyo ingetusaidia, angalau wetu nao waone faida benefits za mining

sector ambayo imejaa. Hatuwezi kugawa yote, wala hakuna Watanzania wetu wanaoshiriki kule. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema hayo nikijua kwamba ni mambo ya muhimu na ya msingi sana lakini mengi *whether* ni viwanda, *whether* ni kilimo *whether* ni uvuvi, *whether* ni nini, yote haya tunahitaji Watanzania wetu *foreign investor anapokuja tuwe na stake in this economy, if we don't have a stake in this economy*, sote tutabaki ni manamba. (Makofi)

Sina uhakika kama wengi wetu tunapenda kubaki manamba. Tunataka kuonekana tuna *participate* katika nguvu za kuzungumzia maendeleo yetu. Sisi tusiwe on lookers to our own development. Maana ukiwa on looker unakuwa unaangalia unasema wale, wale wanakwenda, wale wanachukua mali, sisi hatutaki hayo. Tunataka tushiriki. Na kama ni uwezo, basi uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalotaka kushauri hapa ni kwamba tunao utaalam mzuri sana katika nchi hii. Na utaalam huo katika sekta hizo zinazotakiwa, bado hatujafanya kazi. Kazi inaendelea. Tulihitaji tuwe na *public hearing* kwenye Muswada huu. Huu Muswada ni wa maana sana. Watu watoe mawazo yao kuhusu wanavyotaka, *destiny* ya maisha yao iwe na hivi ndivyo tunavyoomba Muswada wa *Purchasing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono mia kwa mia. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwa kusema kwamba Muswada umekuja ni Muswada nzuri kwa kweli ni kama chakula kilichoandaliwa wakati una njaa. Lakini kikaja chakula mezani sicho au sivyo ulivyokitegemea kije. Tulitegemea tupate ugali mzuri uliopikwa vizuri, kwa mbaya umekuja ugali haukuiva vizuri. (Kicheko)

Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Naibu Spika, uzito wa jina la Muswada huu, maana yake ukiuangalia jinsi ulivyioletwa huu mimi ni mwaka wa tisa kwenye Ubunge na kwa mara ya kwanza nimepokea Muswada ambao unaanza na *preamble* na *preamble* hiyo inatamka Katiba ya nchi. Unapotamka Katiba ya nchi ni kama Mkristo au Mwislamu anapoanza neno kwa kushika Biblia au kushika Msahafu ni neno zito. Anaanza kwa kiapo huyo. (Makofi)

Muswada huu niliutegemea leo ingekuwa kama vile mwaka 67, wakati Rais, Baba wa Taifa Marehemu alipotangaza Azimio la Arusha, haikuwa rahisi alipotangaza Azimio la Arusha ilibidi avute pumzi ili atamke. Kwa sababu mambo yaliyotamkwa katika Azimio la Arusha iliwakatisha tamaa wengine na ikawapa matumini wengine. Sasa Muswada huu nilitegemea ungekuja hivyo.

Wenzangu waliopita huko nyuma, wengine wamezungumza kwa aibu wakasema labda baadaye mlete, tufanye *amendments* na kama msipoleta tutaleta wenywewe. Nakubaliana nao lakini unapokea ugali uliokufa walete mwingine baadaye. Nasema ni

sahihi, lakini kwa mara ya kwanza nasema Muswada huu ni mzuri, lakini kwa kweli haukutayarishwa kwa vile ulivyotakiwa, malengo ni mazuri. Lakini utekelezaji wa malengo hayo siyo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yametajwa mapungufu yaliyoko katika Muswada huu. Mimi si mtalaam wa Sheria. Lakini nilitegemea baada ya Muswada huu kungekuwa na *Schedule of amendments* katika Sheria mbalimbali. Sheria ambazo zingepata *amendments* kwa mfano, Sheria ya Kodi ingepata *amendments*, kuangalia uwezekano wa kuwasaidia maskini wakuwezeshwa. Sheria ya manunuzi ingefanyiwa marekebisho (*amendments*).

Mheshimiwa Spika, tunapitisha bajeti hapa tunapitisha bajeti ya trilioni 3 katika trilioni 3 zote ni bajeti ya manunuzi. Siyo bajeti ya kuzalisha, ni kidogo sana tunazalisha. Tunapozungumzia, trilioni 3 ni bajeti ya manunuzi ina maana ya kwamba hela hizo zitakwenda kwenye manunuzi. Sasa zinawasaidiaje Watanzania hizo hela kunyanyuka. Mmoja alitamka hili leo asubuhi tuchukue mfano hapa hapa kwenye Bunge aliyepata kandarasi ya kujenga ukumbi wa Bunge kwa bilioni karibu 10 ni nani? Ni mgeni, na si vibaya kwa sababu hatuna uwezo.

Lakini sisi Watanzania tutawezaje kama hatukuwezeshwa. Sasa Sheria kwa mfano, ya *Procurement* ingekuwa na mwelekeo wa kusema kwamba unaponunua kitu au inapofikia tenda kiasi hiki, wakapendeleta hawa. Kwa nini tunalionia aibu. Nasema tumekuwa na woga wa kutamka suala la uzawa sahihi kisiasa na ninajua kigugumizi cha Serikali kinatoka wapi. *Kigugumizi* cha Serikali ni kwamba wanaotufadhili hawataki waonekane kwamba tuna upendeleo. Lakini hii *World Bank* tunayoizungumzia tungeweza kuibana katika Kanuni na Sheria zetu. Maana mwaka jana tulipunguza kodi ya maziwa ili tuweze kuboresha uzalishaji wa maziwa ya hapa ndani nchini kwetu. Waziri yuko hapa. Tilitunga *surcharge* ya *twenty five percent* siyo maziwa ya binadamu, maziwa ya ng'ombe. Tilitunga *surcharge* ili tuweze ku-encourage local production kuwa rahisi kwa kulinganisha na import of products. Hii ni nia nzuri ya kusaidia ku-empower uchumi wetu. Sasa sheria hii haitamki lolote katika kuwasaidia Watanzania katika taratibu za kisheria.

Ninajua zimetungwa Sera. Lakini Sera inapewa nguvu na Sheria. Kama Sheria haikai vizuri haiwezekani ukaweza kuitunga hiyo Sera ikafanikiwa. Hivi leo ukienda Dar es Salaam na bahati mzuri mimi nimelelewa katika biashara kuanzia mwaka 72. Na ni mtu ambaye nimejitahidi na mimi kujiokoa nimejaribu ninavyobanwa mbavu na hawa tunaowasema, inatisha. (*Makofi*)

Leo ukienda Dar es Salaam, Wachina, Wajapan, hasa Wachina, wako mpaka biashara za *ice cream*, biashara za gereji, biashara za kuuza maziwa. Hivi nyinyi kweli mnashindwa hata kuwatetea wananchi na kutunga sheria kwamba biashara hizi hazitaruhusiwa asiyezaliwa hapa nchini, tufike hapo, hivi ni nani anawapa leseni za kufanya biashara nchini kama hatukuweza kuwatungia Sheria, hakukuwepo na Sheria. Lakini sasa ndiyo tunatunga sheria za kuwa-empower Watanzania, mimi sitaki kusema

Watanzania wa namna gani, lakini najua waliolengwa humu ndani na ndiyo maana tumeanza na Katiba.

Tulipotangaza Azimio la Arusha tulisema tutayachukua mabenki, tulijua ni ya mabepari. Kwa hiyo, tunaanza kutunga Sheria ambayo inaelekeea kuwalinda watu wetu bila kumweleza mtu mwingine kwamba hatukutaki hapa nchini. Tulitegemea Sheria hii ndiyo itafanya hiyo kazi. Lakini haimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tuchukue hatua zifuatazo. Kwanza ninajua tumekwishafika hatua ambapo Sheria inapitishwa. Si rahisi, ni ushauri tu. Si rahisi kusema Sheria isipite kwa Kanuni zetu na taratibu za kutunga Sheria. Wale wenzangu waliosema sheria itabidi tuiletu tuifanyie marekebisho nakubaliana nao kimsingi. Lakini tukubaliane kwamba iko kazi kubwa ya kufanya. Kwanza vyombo hivi vilivytajwa vya uwezeshaji kwa mfano mabanki. Leo mabenki yetu yote sheria zake ni za kibepari mtu wa kawaida huwezi kwenda kuchukua mkopo. Mimi nimeomba mkopo, tena benki yetu *Tanzania Postal Bank*, nimeambiwa hawawezi kuchukua hati ya Lushoto wanataka wachukue hati ya Dar es Salaam mimi nina shamba langu na majumba yangu yako Lushoto. Leo wanataka hati ya Dar es Salaam nitaipata wapi.

Ni kunitoa tu nje kwenye uwanja nisifanye biashara. Ni ukweli. Sheria ndivyo zinavyotamka. Sasa tunaunda mfuko. Kwa sababu ya muda. Nitashindwa kuuchambua Muswaada huu kifungu kwa kifungu. Tunaunda mfuko na mfuko mimi nina wasi wasi kwamba utakuwa mfuko tena kama ule wa pembejeo. Huu utaendeshwa kama mfuko wa pembejeo. (*Makofi*)

Na utakwenda kama mfuko wa pembejeo kwa sababu hakuna Sheria na Kanuni zitatungwa *regulations* lakini hata ukiangalia hata hiyo *Schedule of Regulations* ambayo imewekwa kazi za Waziri hazonyeshi wazi kwamba huyu amepewa makali na *limits* kwa Waziri amepewa uwezo wa kutamka kwamba biashara hizi zitafanya na Watanzania tu. Hazikutamkwa humu.

Nakumbuka historia ya humu ndani. Kuna Waziri mmoja alijifanya kwmaba anaelewa kabisa akaanza kutangaza hii na hii na hii akaambiwa nyamaza. Kwa sababu huwezi ukatamka kwamba hizi ni biashara za fulani. Na hiyo itakwenda kwa wakubwa wetu hawataturewa, watatunyima misaada. Sasa ni ukweli usiopingika. Lakini tusifike mahala tuone aibu sana kiasi kwamba tunawasaliti watu wetu au tunashindwa kabisa kuwatetea bila woga. Nategemea Muswada huu ungechukua hatua hiyo.

Nije kwenye kuchangia kidogo, ili niupe nyama Muswada maana sasa hapa ilipo goli limekwishaingia. Hapa goli liko ndani kwa hiyo sasa niupe nyama tu. Kifungu cha 20 ambacho kinatangaza *funding*. Ukiangalia *funding* ya mfuko huu kwa kweli tunaunda kweli kama vile tunavyounda shirika lingine lolote lakini hatujauunda kama mfuko muhimu wa Serikali. Nilitegemea ingetamkwa katika Sheria kwamba kila mwaka wa Bajeti itatengwa pengine 00.2 percent ya *GDP* ili mfuko huu ukue kwa nguvu.

Leo kuna mfuko wa wenye viwanda na waajiri wanachangia kwa upande wa *VETA*. Ni kweli sasa kuna maendeleo makubwa sana kwa upande wa *VETA*. Sasa hapa

tumetamka *grants*, *grants*, mfuko huu utaendeshwa kwa *grants*. *Sub-Version* ya Serikali tunajua siyo rahisi. *Sub-Version* ya Serikali itategemea Bajeti ya Serikali na *balances*. Nilitegemea na naomba kifungu kiongezwe kwamba kwa kweli hela za mfuko huu zinatokana na bajeti kuu na zitatoka na asilimia aidha kutokana na wazalishaji au kutokana na *GDP* yetu kutokana na mfumo wa bajeti nzima, zitengwe katika mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda mimi nafikiri asubuhi kuna mtu aliyesema kwamba labda Muswada huu umekuja kwa kujiandaa kujipanga. Sasa nakubaliana kwamba Muswada huu kweli umekuja kama vile tunajiandaa. Lakini kwa kweli itabidi kwa haraka sana uje Muswada ambao utarekebisha Sheria mbalimbali ambazo zitaonyesha wazi kwamba tunampendelea Mtanzania na si lazima tumweleze Mtanzania wa namna gani aidha Wa rangi lakini tutamke makundi yatakayopendelewa na sheria hizo.

Tunapozungumzia akina mama basi watamkwe. Tunapotamka wafanya biashara wadogo wadogo watamkwe ni wa ngazi gani. Na mwisho, napenda kusema hawa wenzetu wa upande wa pili waliandika mambo yao kiasi fulani. Lakini walikoseakosea pale kuanza kuonyesha kwamba wanajua zaidi kuliko chama tawala. Lakini ziko *points* ambazo wamezieleza za msingi ziangaliwe kwa mfano elimu. Hivi leo tunasema tuwawezeshe watu wetu ni wachache wanajua biashara maana yake nini. Ni wachache wanajua urari, elimu, mfuko huu upewe wajibu. Kwa hiyo, yako maeneo ambayo wameyatamka ya kusaidia, yaangaliwe tusiyachukie tu kwa sababu yanatoka kwa wapinzani. Hapana, tuyachukueni maneno ambayo yatajenga msingi wa kujaribu kuboresha Sheria hii. Baada ya kusema hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, baada ya kujua kwamba tutaleta marekebisho mapema iwezekanavyo. (*Makofit*)

MHE. LEONARD N. DEREFA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Napenda tu nipende kusema kwamba kwa kweli sheria hii ilitakiwa ije mapema zaidi. Na ningelipenda ninukuu usemi wa Marehemu Baba wa Taifa alisema, *You can't address poverty without addressing the poor*.

Kwa hiyo, tuijilize kwanza maskini ni akina nani katika nchi hii. Kwa hiyo, ni kwamba *we can only address poverty* lazima tuwajue akina maskini ni akina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuuleta Muswaada huu muhimu sana na napenda niseme tu kwamba Waziri Mkuu wetu sasa hivi *is the long serving Prime Minister*, amekaa muda mrefu sana ana *experience* ya kutosha. Ninaamini kabisa kwamba uzoe fu aliyoupata huu atautumia kwa haki katika kutatua tatua suala la umaskini ambao ni kero kubwa kabisa. Ukiwa maskini hata nyumba yako inakuwa ni balaa. Hata mama hawezi kukusikiliza ukiwa maskini. Unachanganyikiwa. (*Kicheko*)

Sheria hii itatufanya wanaume tuwe na heshima. Kwa sababu hela ikikosekana ndani ya nyumba kuna mfarakano wa hali ya juu sana. Ukitu anakuona kama tapeli, au kama mpumbavu. Kwa hiyo, mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Sheria na ilitakiwa iwe imeletwa mapema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwamba India, wenzetu Wahindi walipata nafasi nzuri sana na kwamba ukitaka kuwaondosha watu kwenye umaskini hasa wakati wa *Green Revolution* lazima ufanye vitu kama vitano hivi, uboreshe miundombinu, uwajulishe kwamba miundombinu ya maji, kila mahala kuna maji ya kufanya kazi. Kuna maji ya kazi, maji ya kunywa, maji ya viwanda, maji ya kilimo. Shinyanga kama tunavyosema mara nyingi tunayo almasi lakini ukienda kuchimba almasi kama maji hayapo haionekani, hata dhahabu haionekani bila maji. Hata pamba, hata wewe mwenyewe bila maji, hata gari haiendi bila maji. Kwa hiyo, miundombinu ya maji ni muhimu kama tunataka kuwakomboa wananchi wetu. India walihakikisha kwamba kila mahala kuna *power*. Kuna umeme, India mahala panaendeka kwa barabara, kwa reli, kwa ndege, kwa miguu hata kwa punda, wale wanatumia kila aina ya usafiri. (*Makofi*)

Halafu *communication* napenda nitumie nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Sasa hivi hata kijiji *brother* tunasema. Kwa hiyo, nampongeza sana. Hii ndiyo mojawapo ya miundombinu. Miundombinu nyingine ambayo hata wengine hata wataalam wa *economy* hawausemi ni muundombinu wa fedha. Tunalo tatizo hapa nchini Tanzania, hatuna muundombinu wa fedha na ukitaka kufanya kitu hata kama una akili namna gani unakuja unakwama kwenye hela. Ukienda kwenye benki ambazo tumeziuza unaonekana kama unataka kuwaibia. (*Kicheko*)

Kwanza hata ukiingia tu kwenye benki ile kukuona tu wanaona, *the thief is coming here. Tunatakiwa tuboreshe miundombinu ya fedha. Sasa nafikiri tumejikoki zaidi, National Bank of Commerce tulifiki itatusaidia.* Lakini inakataa ku-*finance* kilimo ambacho ni kitu muhimu. Watu waliotuleta hapa asilimia 80 ni wakulima kama wasingetupigia kura tungekuwa tumechemsha, hawa watu wamekataa ku-*finance agricultural activities* na wamewaachia watu wa CRDB ambao hawana hela za kutosha halafu nimesikia hata *Microfinance* tumewauzia. Tunajikoki, unajua ukijikoki ni kama risasi kwenye bunduki aidha uipasue ama upige risasi.

Kwa hiyo, nasema kwamba tatizo miundombinu na fedha lazima tuifkirie kuliko miundombinu hata ya barabara. Kama kuna umeme, kama kuna maji, kama kuna barabara, kama kuna simu, kama kuna hela, nani atakuwa maskini katika nchi hii. Kwa hiyo, mimi naomba hata wale watu ambao kwa kweli wameweza kununua *actually they have bought us.* Suala lingine limesemwa sana la uwekezaji. Tunapenda ile Kamati iliyoundwa iletu hapa yale mapendekezo halafu tuyajadili, tupewe muda wa kutosha. Msituletee tena yale mambo ya masaa halafu baadaye mkisema imepitwa na wakati. Tumesema kwamba hizi Sheria za Madini zirekebishwe. Ninaomba kwamba zitakapoletwa tupewe muda wa kutosha ili tujaribu kujadili ili turekebishe kwa sababu ni balaa. Suala lingine ni suala la mazao ya wakulima. Wakulima ni asilimia 80. Ninaamini kabisa kura zote zilizotuleta hapa ni za wakulima lakini leo utaratibu wa

mazao yao yanavyonunuliwa inatisha. Wakulima wa pamba Serikali ilitangaza kwamba watanunuliwa, lakini lile tangazo halikusaidia, na inavyoonekana ni kwamba wafanyabiashara wamejiunga ili kuhakikisha kwamba wakulima wamekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la pamba mwaka huu wakulima walilima sana zao la pamba, kwa sababu ya bei ya mwaka jana, lakini jinsi ilivyonunuliwa pamba mwaka huu haiku-*recover* hata ile gharama ya uzalishaji. Sasa hivi ukitazama ile *rural poverty* ni ya hali ya juu kabisa. Kwa hiyo, nasema kwamba kama tunao wataalam wa uchumi washughulikie namna ya ku-*reverse rural poverty* kwa watu na dawa muhimu ni ushirika. Kwa bahati nzuri Serikali ya Mheshimiwa Rais Mkapa imeweka mkakati mzuri na inawapa hela Ushirika. Lakini, we *don't see the change*. Kule kwangu *SHIRECU is a limping Co-operative* labda mahali pengine. Lakini najua Mwanza vile vile napo imekufa. Nilikuwa naomba kwamba wataalam wetu watusaidie kabisa katika suala la kilimo kwamba kama tunataka kuwasaidia watu wetu, wataalam wawepo kule, zile *services*. Wakati mimi nikiwa mtoto mdogo, nilikuwa kila dakika namwona *Agricultural Advisor* na alikuwa ana uwezo, alikuwa anapita kila shamba, anatazama. Lakini wakati wa *retreachment tume-retreach* hata Mbwana Shamba na nasema kwamba wakulima wetu bila kuwawekea utaratibu nzuri wa kuhakikisha kwamba kilimo chao kinasaidia ule umaskini hatuwezi kuukabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisamehe. Lingine tunaomba kitu ambacho wawekezaji waliopewa leseni hapa wawawezeshe Watanzania. Tunao wawekezaji ambao wamepewa hapa viwanda halafu hawatumii bidhaa za hapa *as a result*, mimi nakunywa bia, zamani nikinywa *bia I finance* mkulima wa Kilimanjaro anayelima *barley*, *I finance* mkulima wa Mbeya anayelima *barley*, *I finance*, mkulima wa Arusha anayelima *barley*, *I finance*, ipo Mikoa minne ambayo ilikuwa inalima *barley*, lakini leo *barley* hii inatoka nje (Afrika ya Kusini). Mimi nasema kwamba kama inawezekana, mtu anayetaka kutuletea maendeleo hapa lazima atumie bidhaa za kwetu hapa. Sasa huu utapeli ni kwamba sasa hivi nikinywa bia, *I am helping the farmer* ninamsaidia mkulima wa Afrika ya Kusini. Sasa hiyo, sidhani kama ni mwelekeo nzuri na inaonekana kwa kweli tutajiletea matatizo. Baadaye naomba kwamba Serikali lazima ielete, kwa mfano, mkulima yuko Wizara ya Kilimo na Chakula. Masoko yako Masoko na Ushirika. Ni kama mguu huu mwingine uko tofauti na mwingine. Hivi kweli tutawasaidiajaje hawa?

Kabla sijagongewa kengele, nilitaka niseme kwamba kitu kingine tunatakiwa tufanye suala la elimu, mafunzo. Kwa bahati mbaya *policy* zetu za huko nyuma, hazikumruhusu Mtanzania kufanya biashara. Mtanzania alikuwa anapambana na Serikali asifanye biashara. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kwamba hela ziwepo za kutosha katika kuwaelimisha Watanzania ili waweze kufanya biashara. Kwa sababu hakuna Watanzania wafanya biashara. Na sera zetu zamani huko zilikuwa zimekwamisha wafanya biashara.

Lingine nilitaka niseme kwamba kwa kweli tunatakiwa vile vile kuwa-*involve* hata *social scientist and anthropologist* na wataalam mbalimbali, kwa mfano nikiuliza kwamba wakati wa *RTC*, Ofisi nyingi zilikuwa na wataalam wengi sana unakuta *Marketing Manager* ana *Masters*, lakini duka linamshinda. Lakini ukimwona Mchaga amesoma darasa la saba. Sasa hapo, hata Msukuma kwa mfano, Shinyanga, siongelei

ukabila. Shinyanga ni Wasukuma lakini wenyewe maduka siyo Wasukuma. Kwa hiyo, yale mambo ya *sociology* lazima na mwenyewe asome. Kwa nini Msukuma anashindwa kushughulikia duka. Na akitengeneza duka, wale ndugu zake wana-*throne*, wanajua kwamba *wasabile*, amekuwa tajiri. Vile vile *we have to look on the social structure*. Mchaga anaacha mke wake Moshi. Hakuna ile *chain of relationship*. Kwa hiyo, nasema kwamba hata ile *social structure*, haya mambo ni kama wewe ni mvuvi unakwenda mtoni kwenda kuvua samaki usifikiri kwamba kule mtoni kuna samaki tu, kuna na mamba hata nyoka wapo kule na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu mdogo kuhusu muswada wa Sheria Uwezesaji Kiuchumi Wananchi wa mwaka 2004. Awali ya yote napenda kusema wazi kabisa kwamba naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, napenda sana kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wake wa Nchi-Mambo ya Sera, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao kwa wenyewe kujiwezesha na kuweza kuwasilisha Muswada huu. Nasema hivyo kwa sababu waliweza kuwasilisha sera ya uwezesaji wa wananchi kiuchumi mwanzoni mwa mwaka huu na chimbuko nililoliona la Muswada huu wa leo ni hiyo sera ambayo tuliidai kwa muda mrefu sana. Kwa sababu kulikuwa na lugha nyingi ambazo zinatumika lakini zilikuwa haziendani na hali halisi ya Utanzania. Kulikuwa na maneno kama Mzawa, Mzalendo, Mtanzania halisi, Mtanzania kweli-kweli lakini tunazungumzia Wananchi. Tuna sheria ya uraia hiyo ndio inayopambanua nani ni Mwananchi wa Tanzania.

Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilivyoona ni kwamba huu muswada kwa kweli unaweka mfumo wa sheria wa kutekeleza sera au wanaita “*legal frame-work*”. Kwa sababu kuna vyombo huwezi kuvianzisha bila kuvitungia sheria ili viweze kufanya kazi sawasawa. Mimi nilikuwa nadhani ni rahisi zaidi kama vitu hivi viwili vitasomwa pamoja; ile sera ya Uwezesaji pamoja na muswada wa sheria ambayo inaweka *Legal frame-work* ya kutekeleza hiyo sera. Nasema hivi kwa sababu ungesikiliza wenzetu wengine upande wa Upinzani wanasema hamna lolote

Lakini ukisoma hii sera humu utakuta mazingira yameainishwa na mikakati imeelezwa. Kwa hiyo, sheria hii ni ya kusaidia kutekeleza yaliyomo humu. Sasa mimi nadhani ni vizuri tukawa *fair* tusome hivi vitabu vyote viwili. Huu Muswada na hii sera ambazo zinaeleza nini kinachotakiwa kufanyika. Sasa hapo baadaye nadhani kinachotakiwa kwa kweli ni *plan of action*. *Plan of Action* kwa kutegemea muda wa utekelezaji ndiyo ambayo nadhani inakosekana, na wakati wake bado maana sheria ndio tunaijadili sasa.

Sera tunayo na sheria tunaitunga na baadaye *plan of action* na Bajeti ndio utekelezaji wenyewe unavyokwenda. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka tu kutoa hayo. Kwa mfano ukiangalia katika Ibara ya 3.3 ya hii Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ibara ndogo ya 6 inasema: "Kurahisisha upatikanaji wa mitaji na kuwawezesha Wananchi kukopesheka". Sasa sheria hii inatekeleza hiyo kwa kuanzisha vyombo na mifuko ambayo itasaidia kukopesheka kwa Wananchi ambaao ni tofauti na Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mimi kwenye Tume inayoitwa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano na wiki mbili zilizopita tulipata nafasi ya kutembelea India kuona mfumo wao wa Fedha wa *Federation* pamoja na *States* zake. Lakini tukapata bahati ya kuonana na Balozi wetu, Balozi Eva Nzaro, ambaye alieleza masikitiko yake jinsi wawekezaji ambaao wanataka kuja huku kutoka India ambavyo hawapati mawasiliano mazuri.

Kwa bahati nzuri mimi nilikuwa na Mtanzania mmoja ambaye yuko kwenye sekta binafsi, Dr. Eddy Mndolwa. Tukamwomba kama kuna ambaye yuko tayari aje tuonane naye mimi kwa wadhifa wangu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Bunge, anieleze ni kitu gani anachotaka kuhusu nia yake ya kuwekeza hapa Tanzania. Mwekezaji huyo alieleza kwamba Serikali ya India imechagua nchi nane (8) hapa Afrika ambazo imeziwekea *Soft Loans*. *Soft Loans* hizo zinataka ziwe na *guarantee* ya Serikali lakini siyo kwamba zitumiwe na Serikali. (*Government guarantee*) kwamba itasimamiwa hivyo. Hizi *soft loans* zimeainisha maeneo kama 24. Lakini India wanachotaka ni kwamba wana vitu vingi sana kwa mfano, ukitaka *Laboratory Equipments*, ziko nyingi.

Kwa hiyo, ili waongeze mauzo nje katika biashara ya Kimataifa wanataka kutoa hizo *soft loans* kwa Tanzania ili Wahindi kule walio na vifaa wapate mahali pa kuuzia vitu vyao. Na mkataba ni *Turn Key Project* na wanatoa muda wa miaka mitano (5) *grace period* wa kutekeleza na muda wa miaka kumi na mitano (15) wakukamilisha kurejesha hizo *soft loans*. Hizo ndio *opportunities* ambazo ziko India. Kwa hiyo, sisi tutajitahidi kufutilia na Wizara ya Mambo za Nje ili kwa kweli tutumie fursa hiyo. Wenzetu wengine katika hizo nchi nane (8) za Afrika wanaitumia hiyo fursa vizuri sana.

Sasa nilikuwa nasema hivi vyombo tunavyounda leo pengine ndio Vyombo vizuri zaidi vya kupitishia hizo *Soft loans*. Wao wanasema hawatatoa *soft loans* kwa watu ambaao siyo Watanzania. Ndugu Naibu Spika, mimi naunga mkono kwamba vyombo hivi viundwe, viimarishwe ili viweze kufanya kazi nyingine ambazo Serikali haiwezi kuzifanya na kutumia misaada mingi ambayo inakuja. Mimi sioni kwa nini tunakubali kutumia fursa ya *AGOA* na tuwache hizi *soft loans* za Wahindi ambazo ni wenzetu wako karibu zaidi na sisi kufuatana na hali ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dhamana ya mikopo. Suala hili limenifurahisha sana katika kile kifungu cha tano (5) kifungu kidogo cha pili (2) kifungu kidogo zaidi (O) kwamba sasa hivi ukimtaka Mtanzania aweke dhamana kwa kweli unamsumbuwa. Ndugu yangu Shekiffu alieleza kwa uchungu sana kwamba ijapokuwa

una dhamana lakini dhamana hiyo unaambiwa iwe mahali fulani. Sasa vitu kama hivyo vinatuchelewesha. Kwa hiyo, hili la kuweka wazi suala la dhamana liwe wazi kwamba Halmashauri yenyewe ndio iamue kwamba huyu anaaminika kwa hiyo hakuna haja ya kumwambia alete dhamana. Kitu ambacho kinatakiwa ni *trust*. Kama Mwanachi ana shamba alionyeshe shamba hilo na Hati yake. Pengine hakuna haja ya kuchukua Hati isipokuwa apewe miongozo ambayo inatakiwa kumwendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tano (5) kifungu kidogo cha tatu (3) kinazungumzia kutenga maeneo maalum ya uwekezaji. Uwezesaji kwa ajili ya uwekezaji ndio suala kwa kweli tunalozungumzia hapa. Ndio maana mimi nadhani asubuhi tulikuwa tunazungumza mambo ya zamani kwamba mtu anachukua mkopo anakwenda kuula au kula mtaji. Kuna wengine hata hivyo wanakejeli wanasema tutakwenda kuoa wanawake. Si sawa, Watanzania wamebadilika siku hizi. Walikuwa hawajaonyeshwa njia tu. Lakini sera hii inawaonyesha njia kwamba wanaweza kuzalisha na kuondoa umaskini. Kwa hiyo, haya maeneo yakutenga mimi nadhani tusiyaonee aibu hata kidogo.

Kwa mfano kwenye madini kabisa kabisa Ndugu Naibu Spika, eneo la uchimbaji wa vito, vito vyta thamani, *Gemstones* hilo ni eneo mojawapo lingetamkwa wazi kwamba ni la Watanzania tu wachimbe, hayo madini, wakubwa waende kwenye madini ya almasi, dhahabu na kadhalika.

Kwa hiyo, kazi bado ipo kwenye hizo *actions* na Kanuni ndio zitamke hayo. Hii sheria tukitaka itamke yote hayo kwa kweli itakuwa ni sheria ambayo ni nzito kutekelezeza, lakini katika Kanuni zitamke hivyo kwamba maeneo ambayo yatakuwa kwa Wananchi ni haya yafuatayo. Mimi napenda kulisema kabisa hili kwa sababu Kamati ninayoongoza inasimamia eneo la Nishati na Madini. *Gemstones* ziwe ni kwa Wawekezaji Watanzania tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, kifungu cha kumi (10) kifungu kidogo cha sita (6) na kifungu kidogo zaidi (b), hiki kitaleta matatizo. Kifungu hiki kinasema, ukurasa wa 12 nitaanza juu kabisa: "Or where there is no quorum for the continuation of a meeting only because the exclusion of a member from the deliberations on a matter in which he has disclosed a personal interest, the other members present may

(a) *post-pone consideration of the matter until the a quorum is realized; or*

(b) *proceed to consider and decide the matter as if there was a quorum.*

Kifungu hiki ni kigumu sana. Kitazua matatizo kwa sababu huyo mtu ambaye ana *personal interest* kwenye suala fulani labda liamuliwe kwa upande wake kwa yeye kupata lakini akikosa ataomba rufaa. Kwa hiyo, mimi nadhani hiki kingeondolewa kwa kweli. "*Quorum*" lazima iwepo. *Minimum quorum* iwepo kisiachwe kwa sababu kuna uwezekano unaweza kutisha watu ambao wanaunga mkono hiyo hoja na ukatumia kifungu hiki na ukawa umetekeliza kisheria lakini kwa kweli si jambo zuri sana ya

kuliweka katika sheria hii nzuri. Mimi nadhani hili lingetazamwa na tungeweza kuliondoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi hapa tulimsikiliza Msemaji wa Upinzani. Alizungumza maneno nadhani siyo ya kweli. Mheshimiwa Shekiffu aliyozungumza pia. Kwa kweli Serikali imefanya marekebisho katika *Amendment Schedule*. Ukitizama hii, *Amendment Schedule*, kifungu (5) (2) by deleting paragraph (k) of sub clause (2) substituting for it the following paragrap:

(b) Identify training opportunities in economic and investment issues and to coordinate the relevant training programmes.

Sasa mnataka nini tena hii si ndio *training* au kuna *training* nyingine? Mimi naona hii ndio *training* ambayo tulikuwa tunazungumzia.

Kwa hiyo, ule ukosoaji kwa kweli mimi sikubaliani nao. Serikali imekubali imeshauri nadhani na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri sana tunaongojea humu ndani labda mtu mwenyewe tu asitake, lakini haujabagua mtu yeote. Unasema Mwanachi isipokuwa napenda kupendekeza kwamba kwa kuwa Wananchi wanatofautiana kufuatana na uwezo walionao, basi ni vizuri wakawekwa katika makundi ili kusiwe na kunyang'anywa kwamba kundi fulani halikufanya vizuri kwa sababu mtu mmoja ambaye ni mkubwa amechukua fedha zote. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mimi napendekeza kuwa Kundi (A) Liwe wale wasio na uwezo kimitaji, Kundi (B) Wenye uwezo mdogo, Kundi (C) Wenye uwezo wa kati au wastani, na Kundi (D) Wenye uwezo mkubwa. Kundi hili la Wenye uwezo mkubwa ndio hilo ambalo lingeweza kuingia ubia na wawekezaji wakubwa wa nje halafu hatimaye waweze kununua hisa zao. Kwa hiyo, hawa tukiwaacha nje kwa kweli tutapata tabu. Wapewe hiyo nguvu lakini nguvu hiyo ya mtaji isiumize wale wengine ambaa hawana uwezo wa kushindana nao.

Hili ndio pendeleko ambalo ningependa lifanyiwe kazi ni *very raw or unprocessed*. Lifanyiwe kazi litenge vizuri. Wasio na uwezo kabisa kimitaji. Wenye uwezo mdogo Wenye uwezo wa kati na Wenye uwezo mkubwa lakini wanataka kutafuta mitaji ya kuweza kununua hisa au kuingia ubia na wakubwa wa nje na hata hatimaye waweze kununua hisa za hao wanaotoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sera ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuleta ukombozi huu ambaa sasa utapata nguvu ya kisheria na nadhani Waheshimiwa Wabunge kazi yetu tutakayofanya ni kuangalia Bajeti kwamba inazingatia utekelezaji wa sera hii pamoja na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika naunga tena mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumemaliza wale walioomba kuchangia, lakini na mtoa hoja atajibu hoja zenu kesho baada ya kipindi cha maswali. Sasa kabla ya sijaahirisha shughuli cha Bunge kuna tangazo moja.

Mheshimiwa Joel Bendera, Mwenyekiti wa Chama cha Wanamichezo ya Wabunge, anawatangazia Wabunge kwamba kuanzia kesho asubuhi saa kumi na mbili kamili, kutakuwa na mabasi yanawapitia wale wanaokwenda kwenye mazoezi, kwenye uwanja wa mpira. Haya ni maandalizi wa ule mchezo wetu wa mpira kati ya Waheshimiwa Wabunge na CRDB ili kuchangia Watoto Yatima wa Makete. Kwa hiyo, kesho asubuhi kuanzia saa kumi na mbili mabasi yatazunguka kuwachukua kwenda kwenye mazoezi.

Baada ya tangazo hilo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.45 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
tarehe 3 Novemba, 2004 saa tatu asubuhi)*